# Historia ya Tanzania na Maadili

## Kiongozi cha Mwalimu
## Kidato cha Pili




Taasisi ya Elimu Tanzania

*Mali ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Hakiuzwi*

# i to ia a anzania na Maadili

## Kitabu cha Mwanafunzi

## Kidato cha Pili

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI
NA TEKNOLOJIA

*Cheti cha Ithibati*

Na. 1598

Jina la Chapisho: Historia ya Tanzania na Maadili Kitabu cha Mwanafunzi Kidato cha Pili

Mchapishaji: Taasisi ya Elimu Tanzania

Mwandishi: Taasisi ya Elimu Tanzania

ISBN: 978-9912-756-29-8

Kitabu hiki kimeidhinishwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia tarehe 11 Septemba 2024 kuwa Kitabu cha Kiada kwa ajili ya Mwanafunzi wa Kidato cha Pili katika Ngazi ya Elimu ya Sekondari nchini Tanzania kulingana na Muhtasari wa mwaka 2023.

Dkt. Lyabwene M. Mtahabwa

Kamishna wa Elimu

Taasisi ya Elimu Tanzania

FOR ONLINE READING ONLY

© Taasisi ya Elimu Tanzania 2024

Toleo la Kwanza 2024

ISBN 978-9912-756-29-8

Taasisi ya Elimu Tanzania

Eneo la Mikocheni

132 Barabara ya Ali Hassan Mwinyi

S.L.P 35094

14112 Dar es Salaam.

| | |
|---|---|
| Simu: | +255- 735041168/ 735041170 |
| Baruapepe: | director.general@tie.go.tz |
| Tovuti: | www.tie.go.tz |

FOR ONLINE READING ONLY

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kunakili, kurudufu, kuchapisha, kutafsiri wala kutoa kitabu hiki kwa namna yoyote ile bila idhini ya maandishi kutoka Taasisi ya Elimu Tanzania.

# Yaliyomo

**Orodha ya vifupisho** .......... v

**Orodha ya vielelezo** .......... vi

**Shukurani** .......... vii

**Dibaji** .......... viii

**Sura ya Kwanza** .......... 1

**Ukoloni katika jamii za Kitanzania** .......... 1

himbuko na ukuaji wa ukoloni .......... 1

Mifumo ya kikoloni ya mataifa yaliyozitawala jamii za Kitanzania .......... 3

Utawala wa Waarabu .......... 4

Utawala wa Wajerumani .......... 10

Utawala wa Waingereza Tanganyika na Zanzibar .......... 15

Mchango wa ukoloni katika uhusiano wa Tanzania na mataifa yaliyoitawala .. 21

**Sura ya Pili** .......... 23

**Athari za ukoloni katika maadili ya Kitanzania** .......... 23

Dhana ya maadili wakati wa ukoloni .......... 23

Maadili ya jamii za Kitanzania wakati ukoloni unaingia .......... 24

Athari za mfumo wa ukoloni katika maadili ya Kitanzania .......... 30

Maadili ya Kitanzania yaliyodumishwa wakati wa ukoloni .......... 37

**Sura ya Tatu** .......... 42

**Mapambano ya awali dhidi ya uvamizi wa kikoloni** .......... 42

Dhana ya uvamizi wa kikoloni .......... 42

Sababu za kuupinga uvamizi wa kikoloni na maadili yake .......... 44

FOR ONLINE READING ONLY

Upinzani dhidi ya uvamizi wa kikokoni katika jamii za Kitanzania ..........45

Changamoto zilizokabili mapambano dhidi ya uvamizi wa kikoloni.........52

Matokeo ya kupinga uvamizi wa kikoloni..................................................54

**Sura ya Nne .......................................................................................56**

**Harakati za kudai uhuru wa Tanganyika na Zanzibar ..........................56**

Dhana ya uhuru na harakati za kudai uhuru.............................................56

Misingi ya kudai uhuru wa Tanganyika na Zanzibar.................................57

Mbinu zilizotumika kudai uhuru wa Tanganyika na Zanzibar ..................59

Mchango wa harakati za kupinga uvamizi na ukoloni...............................69

**Sura ya Tano .......................................................................................75**

**Ujenzi wa taifa baada ya ukoloni.........................................................75**

Dhana ya ujenzi wa taifa...........................................................................75

Mifumo iliyojengwa kati ya mwaka 1961 hadi 1966 ...............................75

Mikakati ya ujenzi wa taifa........................................................................84

Changamoto za ujenzi wa taifa..................................................................86

**Sura ya Sita.........................................................................................89**

**Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar .......................................................89**

Dhana ya mapinduzi .................................................................................89

Chimbuko la Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar........................................90

Sababu za Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar ............................................92

Mchango wa Mapinduzi wa Matukufu ya Zanzibar ..................................96

**Faharasa...........................................................................................101**

**Bibliografia .......................................................................................102**

FOR ONLINE READING ONLY

# Orodha ya vifupisho

| | |
|---|---|
| **AA** | African Association |
| **AMNUT** | All Muslim National Union of Tanganyika |
| **ANC** | African National Congress |
| **ASP** | Afro-Shirazi Party |
| **BAKITA** | Baraza la Kiswahili la Taifa |
| **BASATA** | Baraza la Sanaa la Taifa |
| **BMT** | Baraza la Michezo la Taifa |
| **JKT** | Jeshi la Kujenga Taifa |
| **JWTZ** | Jeshi la Wananchi wa Tanzania |
| **KAR** | King's African Rifles |
| **KCMC** | Kilimanjaro Christian Medical Centre |
| **KNCU** | Kilimanjaro Native Cooperative Union |
| **LEGCO** | Legislative Council |
| **NAM** | Non-Alignment Movement |
| **TAA** | Tanganyika African Association |
| **TAGSA** | Tanganyika African Government Servants Association |
| **TANU** | Tanganyika African National Union |
| **TET** | Taasisi ya Elimu Tanzania |
| **TEHAMA** | Teknolojia ya Habari na Mawasiliano |
| **TR** | Tanganyika Rifles |
| **TTCSA** | Tanganyika Territory Civil Servants' Association |
| **UTP** | United Tanganyika Party |
| **VFCU** | Victoria Federation of Cooperative Union |
| **ZNP** | Zanzibar Nationalist Party |
| **ZPPP** | Zanzibar and Pemba People's Party |

FOR ONLINE READING ONLY

# Orodha ya vielelezo

**1.1:** Gavana Sir Horace Byatt ........ 4
**1.2:** Maeneo ambayo Waarabu walizoweka ngome za utawala wao ........ 5
**1.3:** Sultani Seyyid Said ........ 6
**1.4:** Njia kuu za biashara ya masafa marefu wakati wa utawala wa Waarabu ........ 8
**1.5:** Miundombinu ya reli wakati wa utawala wa Waingereza ........ 20
**2.1:** Vazi la asili katika jamii ya Wasukuma ........ 29
**2.2:** Mitindo ya nywele katika jamii ya Wanyamwezi ........ 29
**2.3:** Vazi la baibui ........ 35
**2.4:** Vazi la suti na kanzu ........ 35
**3.1:** Abushiri bin Salim ........ 46
**3.2:** Mtwa Mkwawa ........ 48
**3.3:** Mnara wa kumbukumbu walipouwawa askari wa Kijerumani ........ 48
**3.4:** Mwene Machemba ........ 49
**3.5:** Mangi Meli ........ 49
**3.6:** Liti anka ........ 50
**3.7:** Jamii zilizopinga utawala wa Wajerumani ........ 51
**4.1:** George Kahama (kushoto) na Paul Bomani (kulia) ........ 60
**4.2:** Rashid Mfaume Kawawa ........ 61
**4.3:** Abdulwahid Kleist Sykes ........ 63
**4.4:** Gazeti la Sauti ya TANU ........ 65
**4.5:** Bibi Titi Mohamed ........ 66
**4.6:** Thabit Kombo Jecha ........ 67
**4.7:** Mwalimu Nyerere akiwa na mawakili wakielekea mahakamani ........ 68
**4.8:** Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na Sheikh Abeid Karume ........ 72
**4.9:** Wananchi wakisherehekea uhuru wa Tanganyika mwaka 1961 ........ 73
**5.1:** Baraza la Kwanza la Mawaziri la Tanganyika mwaka 1961 ........ 77
**5.2:** Brigedia Mirisho Sam Hagai Sarakikya ........ 78
**5.3:** Nuta Jazz Band ........ 83
**6.1:** Sheikh Abeid Amani Karume ........ 92
**6.2:** Baadhi ya viongozi walioshiriki Mapinduzi ya Zanzibar mwaka 1964 ........ 93
**6.3:** Baraza la Kwanza la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar mwaka 1964 ........ 97

FOR ONLINE READING ONLY

# Shukurani

Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) inatambua na kuthamini mchango muhimu wa washiriki kutoka taasisi mbalimbali za serikali na zisizo za kiserikali zilizoshiriki kufanikisha uandishi wa kitabu hiki cha mwanafunzi. Kipekee, TET inatoa shukurani kwa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Chuo Kikuu cha Dodoma, Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar, Kituo cha Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU).

Vilevile, TET inatoa shukurani za dhati kwa mchango uliotolewa na wataalamu mbalimbali kama ifuatavyo:

**Waandishi:** Dkt. Jerome S. Machange, Bw. Bonaventura A. Bazira, Bw. Gwido Kalobona na Bi. Sophia J. Amasi

**Wahariri**: Dkt. George K. Ambindwile, Dkt. Abdallah R. Mkumbukwa na Dkt. Valerius W. Mjuni

**Msanifu:** Bi. Rehema A. Hamisi

**Mchoraji:** Bw. Hance E. Wawar

**Mratibu:** Dkt. Jerome S. Machange

Aidha, TET inatoa shukurani kwa walimu wote wa shule za sekondari walioshiriki katika ujaribishaji wa kitabu hiki. Mwisho, TET inaishukuru Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutoa rasilimali fedha iliyofanikisha uandishi na uchapaji wa kitabu hiki.

Dkt. Aneth Komba

Mkurugenzi Mkuu

**Taasisi ya Elimu Tanzania**

FOR ONLINE READING ONLY

# Dibaji

Kitabu hiki cha Historia ya Tanzania na Maadili, Shule za Sekondari kimeandikwa mahususi kwa ajili ya mwanafunzi wa Kidato cha Pili katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kitabu hiki kimeandaliwa kulingana na Muhtasari wa Somo la Historia ya Tanzania na Maadili uliotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia wa mwaka 2023.

Kitabu hiki kina sura sita: Ukoloni katika jamii za Kitanzania, Athari za ukoloni katika maadili ya Kitanzania, Mapambano ya awali dhidi ya uvamizi wa kikoloni, Harakati za kudai uhuru wa Tanganyika na Zanzibar, Ujenzi wa Taifa baada ya ukoloni na Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar. Maudhui ya kitabu hiki yamewasilishwa kwa njia ya matini, kazi za kufanya, vielelezo, pamoja na picha zinazochochea ujenzi wa umahiri unaokusudiwa kwa kila sura. Vilevile, katika kila sura kuna mazoezi yenye lengo la kupima na kujenga uelewa pamoja na ujuzi katika somo hili. Hivyo, unapaswa kufanya mazoezi na kazi zote zilizopo kwenye kitabu hiki, pamoja na kazi nyingine utakazopewa na mwalimu.

Jifunze zaidi kupitia maktaba mtandao https://ol.tie.go.tz au ol.tie.go.tz

**Taasisi ya Elimu Tanzania**

FOR ONLINE READING ONLY

## Sura ya Kwanza

# Ukoloni katika jamii za Kitanzania

## Utangulizi

*Kipindi ukoloni unaingia, jamii nyingi za Kitanzania zilikuwa zimepiga hatua katika maendeleo ya kisiasa, kiuchumi na kijamii. Katika sura hii, utajifunza kuhusu chimbuko, ukuaji, mifumo na mchango wa ukoloni katika uhusiano wa Tanzania na mataifa yaliyoitawala. Umahiri utakaoujenga utakuwezesha kuthamini maendeleo ya jamii za Kitanzania katika kipindi cha ukoloni. Pia, utaweza kushiriki vyema katika juhudi za kuleta maendeleo ya Tanzania.*

**Fikiri**

*Hali ya jamii za Kitanzania wakati ukoloni unaingia.*

### Chimbuko na ukuaji wa ukoloni

Ukoloni ni hali ya nchi moja huitawala nchi nyingine katika nyanja zote za kiuchumi, kisiasa na kiutamaduni. Katika muktadha huu, uchumi, siasa na utamaduni wa nchi zinazotawaliwa hutumiwa kwa malengo ya wakoloni. Ukoloni ulitokana na kustawi kwa mfumo wa ubepari, ambao ulifikia hatua ya ubeberu huko Ulaya Magharibi. Ubeberu huu uliwalazimu wakoloni kuvuka mipaka ya nchi zao ili kutafuta rasilimali na masoko mapya ya bidhaa zao na sehemu za kuwekeza mitaji.

Ukuaji wa ubepari katika robo ya mwisho ya karne ya 19 uliambatana na mapinduzi na maendeleo ya viwanda katika nchi za Ulaya Magharibi. Maendeleo hayo ya viwanda yalisababisha ongezeko kubwa la mahitaji ya malighafi hasa za kilimo na madini kwa ajili ya uzalishaji viwandani. Katika kipindi hicho, malighafi kutoka makoloni mengine kama vile Australia, Kanada na Bara la Asia hasa India ya Uingereza (*British India*) hazikutosheleza mahitaji ya viwanda. Baada ya nchi za Ulaya Magharibi kutuma wapelelezi miaka ya 1850 hadi 1870 waligundua kuwa Bara la Afrika lina uwezo wa kuzalisha malighafi za kutosha kwa ajili ya viwanda vya Ulaya Magharibi. Mataifa kama Uingereza, Ufaransa, Ujerumani, Ubelgiji na Ureno yalivutiwa na rasilimali hasa ardhi yenye rutuba, misitu, mito, wanyama pori na madini barani Afrika.

FOR ONLINE READING ONLY

Wakati huo huo, mataifa haya yalihitaji masoko mapya kwa bidhaa zilizozalishwa na viwanda vyao na hivyo makoloni yalionekana kama masoko mapya ya bidhaa za viwandani. Pia, mataifa haya yalihitaji maeneo ya kuwekeza mitaji yao ili kupata faida kubwa. Hivyo, Bara la Afrika lilionekana kuwa suluhisho kwa uwekezaji huo wa kibiashara. Kulikuwa pia na ushindani wa kisiasa na kijeshi kati ya mataifa ya Ulaya Magharibi kutawala maeneo makubwa. Lengo lilikuwa ni kudhihirisha nguvu zao za kiuchumi na kijeshi na hasa kutawala sehemu muhimu za kimkakati. Sehemu hizo ni kama vile njia za bahari za Atlantiki na Mediterania kupitia Bahari ya Shamu hadi Bahari ya Hindi na mabonde muhimu kama Kongo, Naili, Niger na Zambezi.

Vilevile, kulikuwa na matamanio makubwa ya kueneza dini ya Kikristo, kwani wamisionari waliona ni wajibu wao kueneza maadili ya Kikristo katika maeneo mbalimbali, hasa barani Afrika. Wamisionari wa kwanza wa madhehebu ya Kikristo katika jamii za Kitanzania walikuwa Ludwig Krapf na Johan Rebman. Katika kupeleleza jamii za Kitanzania, wamisionari hawa walijifunza mila, desturi, maadili na mazingira ya Kitanzania. Walijifunza pia fikra za wananchi na viongozi wa jadi, ili kujua namna ya kuzitawala jamii hizo.

Ukoloni ulishamiri barani Afrika katika karne za 19 na 20. Wakoloni walitumia mbinu mbalimbali kuanzisha na kuimarisha tawala zao. Mbinu hizo ni pamoja na mikataba ya kilaghai, kutumia viongozi wa jadi ili angalau kupata ushawishi na hatimaye kuzitawala jamii hizo. Moja ya mikataba ya kilaghai iliyosainiwa ni ule wa kati ya Chifu Mangungo wa Usagara na Karl Peters, mwakilishi wa Wajerumani mwaka 1885. Mkataba huo uliruhusu matumizi ya ardhi ya Usagara na uliweka msingi wa kukua na kuenea kwa ukoloni wa Kijerumani katika maeneo yaliyoitwa Afrika Mashariki ya Kijerumani.

Mikataba iliyosainiwa kati ya viongozi wa jadi na mawakala wa wakoloni ilikuwa na masharti magumu na iliwanyima wenyeji haki ya kuihoji kabla ya kuisaini. Wakati mwingine ukoloni ulikuwa na kuenea kwa kutumia nguvu za kijeshi. Maeneo ambayo wenyeji walipinga uvamizi walishindwa kutokana na sababu mbalimbali, ikiwemo ubora wa silaha za wakoloni ukilinganisha na silaha za jadi zilizotumiwa na jamii za Kitanzania. Njia hii ya matumizi ya nguvu za kivita ndiyo iliyotumiwa zaidi kwani jamii nyingi za Kitanzania hazikuwa tayari kuupoteza uhuru wao kirahisi.

Pia, wakoloni walitumia mbinu ya kuungana na baadhi ya jamii za Kitanzania dhidi ya jamii nyingine. Hii ilitokea katika maeneo yaliyokuwa na uhasama kati ya jamii za Kitanzania. Kwa mfano, Wajerumani waliungana na Chifu Merere wa Wasangu na baadhi ya viongozi wa Wabena kuwapiga Wahehe waliokuwa chini ya utawala wa *Mtwa* Mkwawa. Vilevile, Wajerumani waliungana na Mangi Mandara wa Moshi kumpiga Mangi Sina wa Kibosho. Mara nyingi, wakoloni waliungana na jamii dhaifu

FOR ONLINE READING ONLY

Waingereza walitawala Tanganyika kuanzia mwaka 1919 hadi 1961. Baada ya Vita Kuu ya Kwanza ya Dunia, Tanganyika iliwekwa chini ya udhamini wa Jumuiya ya Mataifa (League of Nations) na baada ya Vita Kuu ya Pili ya Dunia, chini ya Umoja wa Mataifa (United Nations Organisation). Hata hivyo, taasisi hizo ziliipa Uingereza mamlaka ya kuitawala Tanganyika na kuiandaa kujitawala yenyewe. Hivyo, kuanzia mwaka 1919, Tanganyika ilikuwa chini ya utawala wa Waingereza, ambapo Sir Horace Byatt alikuwa Gavana wa kwanza. Kielelezo 1.1 kinaonesha picha ya Gavana Sir Horace Byatt.



**Kielelezo 1.1:** Gavana Sir Horace Byatt

Kuanzia mwaka 1919 hadi 1925, Waingereza waliendeleza muundo wa utawala waliourithi kutoka kwa Wajerumani. Hata hivyo, kuanzia mwaka 1926, chini ya uongozi wa Gavana Sir Donald Cameron, Waingereza walibadilisha mfumo huo na kuanzisha utawala wa kiuwakala. Katika mfumo huu mpya, walitumia mamlaka za jadi kutekeleza sera za kikoloni. Tofauti na utawala wa Wajerumani, mfumo huu haukuwa na ukatili mkubwa. Mifumo na utawala wa Waarabu, Wajerumani na Waingereza imefafanuliwa kwa kina katika sehemu zinazofuata.

**Zoezi la 1.1**

1. Kwa nini Waingereza walibadilisha mfumo wa utawala kutoka utawala wa moja kwa moja hadi mfumo wa uwakala?
2. Eleza jinsi mifumo ya utawala wa Waarabu, Wajerumani na Waingereza ilivyoyaathiri maendeleo ya jamii za Kitanzania.
3. Tofautisha mifumo ya utawala wa Waarabu, Wajerumani na Waingereza katika Tanzania.

## Utawala wa Waarabu

Waarabu kutoka Oman walifika Zanzibar na Tanganyika mwishoni mwa karne ya 18. Kwa madhumuni ya kutawala, walijenga makazi yao katika maeneo ya Unguja, Pemba na pwani ya Tanganyika, hususani katika miji ya Kilwa, Tanga na Bagamoyo, kama inavyoonyeshwa kwenye Kielelezo 1.2.

FOR ONLINE READING ONLY

ili kuzipiga jamii zenye nguvu na hivyo kujipenyeza na hatimaye kuimarisha tawala zao.

Mkutano wa Berlin wa mwaka 1884 – 1885, pamoja na mambo mengine, ulilenga kuligawanya bara la Afrika miongoni mwa mataifa ya Ulaya bila kujali mipaka ya asili ya Waafrika na hivyo kuharakisha ukuaji wa tawala za kikoloni. Hii ilileta madhara makubwa kwa jamii za Kiafrika zilizokuwa zimejengwa katika misingi ya utu, umoja, uzalendo na amani. Kukua na kuenea kwa ukoloni kulianza kusababisha kuporomoka kwa maadili ya jamii nyingi za Kitanzania. Tamaduni nyingi za asili zilianza kufifia kutokana na athari za ukoloni. Kwa mfano, lugha, mila na desturi za asili zilianza kupotea au kubadilika kutokana na kuingiliwa, kudumazwa na kubezwa na tamaduni za kikoloni.

**Kazi ya kufanya 1.1**

Umeteuliwa kuwa miongoni mwa wanafunzi watakaoshiriki mdahalo wenye mada isemayo "Ukoloni ulikuwa na manufaa katika maadili ya jamii za Kitanzania." Soma vitabu na matini mbalimbali kisha andaa dondoo utakazozitumia wakati wa mdahalo huo.

### Mifumo ya kikoloni ya mataifa yaliyozitawala jamii za Kitanzania

Mifumo ya utawala ya Waarabu, Wajerumani na Waingereza katika jamii za Kitanzania ilitofautiana kwa kiasi kikubwa, ingawa lengo kuu la mifumo hiyo lilikuwa kunyonya na kupora rasilimali watu na rasilimali asilia za jamii za Kitanzania. Waarabu wa mwanzo waliofika pwani ya Afrika Mashariki kabla ya karne ya 18, hawakuja kama wakoloni bali kama wafanyabiashara. Hata hivyo, Waarabu kupitia utawala wa Sultani wa Zanzibar kuanzia karne ya 18, walijikita zaidi katika biashara, hususani biashara ya pembe za ndovu, watumwa, karafuu na nazi. Mfumo huu wa utawala ulitengeneza tabaka la juu katika jamii, yaani tabaka la Waarabu na Wahindi waliojihusisha na kilimo cha mashamba makubwa na biashara, huku Waafrika wengi wakibaki katika hali duni ya kiuchumi, kisiasa na kijamii.

Wajerumani walitawala jamii za Kitanzania kuanzia mwaka 1885 hadi 1919 baada ya Vita Kuu ya Kwanza ya Dunia. Katika utawala wao, Wajerumani walitumia mfumo wa utawala wa moja kwa moja, uliokuwa na matumizi ya nguvu za kijeshi na sheria kali dhidi ya watawaliwa. Jamii nyingi za Kitanzania ziliporwa ardhi na kulazimishwa kufanya kazi katika mashamba na miradi ya kikoloni kama vile ujenzi wa reli na miundombinu mingine kwa ujira mdogo. Wajerumani walitawala nyanja zote za maisha ya Waafrika huku wakiendeleza miundombinu kwa ajili ya masilahi yao.

FOR ONLINE READING ONLY




**Kielelezo 1.2:** *Maeneo ambayo Waarabu waliweka ngome za utawala wao*

FOR ONLINE READING ONLY

Watawala wa Kiarabu waliotawala pwani ya Afrika Mashariki walifika nchini katika vipindi mbalimbali. Wengi wao walivutiwa na utajiri wa rasilimali uliokuwapo katika eneo hili. Utajiri huo ulijulikana kutokana na uhusiano wa kibiashara wa muda mrefu kati ya pwani ya Afrika Mashariki na nchi za bara la Asia kama vile Omani, Uhindi, Uchina na Uajemi.

Mtawala wa kwanza wa Kiarabu katika eneo hili alijulikana kama Sultani Seyyid Said bin Sultan. Sultani huyu alikuwa Mwarabu wa kwanza kutawala kwa pamoja dola za Omani na Zanzibar, kuanzia mwanzoni mwa miaka ya 1800 hadi alipofariki dunia mwaka 1856. Sultani alivutiwa sana na hali ya hewa ya Zanzibar, pamoja na kustawi kwa biashara katika ukanda huo, kina kirefu cha bandari ya Zanzibar na udongo wenye rutuba uliostawisha mazao mbalimbali, kama vile mikarafuu na minazi. Hivyo, kiongozi huyu aliwahimiza matajiri wa Kiarabu kutoka Omani kuhamia Zanzibar na kuanzisha mashamba makubwa ya mikarafuu. Mnamo mwaka 1840, Sultani Seyyid Said alihamisha rasmi makao yake kutoka Muscat, Omani hadi Zanzibar na kuifanya

Zanzibar kuwa makao makuu ya utawala wake. Baada ya kifo chake mwaka 1856, urithi wa utawala ulifuata kwa watawala wengine, akiwemo Sultani Seyyid Majid, Sultani Barghash na hatimaye Sultani Jamshid bin Abdullah Al Said. Jamshid bin Abdullah Al Said alizaliwa tarehe 16 Septemba 1929 na kuwa Sultan wa Zanzibar baada ya kifo cha baba yake, Abdullah Bin Khalifa mwezi Julai 1963. Yeye alikuwa Sultan wa mwisho wa Zanzibar kutoka kwa familia ya al Busaid wa Oman waliotawala kwa miaka 91.

**Mabadiliko ya kisiasa wakati wa utawala wa Waarabu**

Jamii za pwani ya Tanganyika na Zanzibar zilikuwa na mfumo madhubuti wa uongozi, utoaji wa uamuzi na umiliki wa ardhi kabla ya kuja kwa Waarabu wa Oman. Hivyo, ardhi katika jamii nyingi ilimilikiwa kwa pamoja na jamii nzima. Kila mwanajamii alikuwa na uhuru wa kuchagua sehemu za kulima, kukata miti au kufuga. Ardhi ambayo haikutumiwa kwa wakati huo ilikuwa ikihifadhiwa kwa matumizi ya baadaye ya jamii nzima. Hata hivyo, baada ya kuja kwa Waarabu, mabadiliko yalitokea. Kwa mfano, Waarabu walianzisha mtindo mpya wa kilimo cha mazao ya biashara, ambao ulisababisha baadhi ya jamii za pwani ya Tanganyika na Zanzibar kuporwa ardhi yao yenye rutuba na kugawiwa kwa wakulima wa mazao ya biashara wa Kiarabu.

Kama ilivyokuwa kwa wakoloni wengine, Waarabu walitekeleza sera za kuchukua sehemu kubwa ya ardhi yenye rutuba kwa ajili ya kilimo cha mikarafuu na minazi. Ili kufanikisha mpango huo, Sultani Seyyid Said alihamasisha kwa kiasi kikubwa kilimo cha mikarafuu na minazi. Sehemu kubwa ya ardhi ya Zanzibar, ambayo awali ilitumiwa kwa kilimo cha mazao ya chakula, ilichukuliwa na mamwinyi wa Kiarabu na kuanzishwa mashamba makubwa ya mikarafuu na minazi. Mfumo huu mpya wa uongozi na siasa kwa ujumla, uliruhusu ardhi yenye rutuba kumilikiwa na Waarabu, uliwafanya wananchi kuwa watumwa katika nchi yao. Katika mazingira haya, heshima, uwezo, haki na mali za Wazanzibari zilinyakuliwa na utawala wa Sultani. Kielelezo 1.3 kinaonesha picha ya Sultani Seyyid Said.



**Kielelezo 1.3:** *Sultani Seyyid Said*

Mtindo mpya wa ugawaji ardhi uliathiri mfumo wa kisiasa wa jadi wa umiliki wa ardhi kwa wanajamii wote, hali iliyosababisha kuibuka kwa matabaka katika jamii. Tabaka la kwanza lilikuwa la wanyonyaji, likiongozwa na viongozi wa serikali, wafanyabiashara wa kihindi na mamwinyi hasa wa Kiarabu. Tabaka la pili lilijumuisha

FOR ONLINE READING ONLY

wakulima wadogo wadogo, raia wa kawaida, huku tabaka la tatu likiwa la watwana na watumwa. Kuja kwa Waarabu kulibadilisha mfumo wa utawala wa kidemokrasia ya kijadi na umoja uliokuwa ukiendeshwa na tawala za kijadi. Mfumo huu mpya ulileta mgawanyiko katika jamii. Mfano wa mgawanyiko huo ni jamii za Kizanzibari zilipoteza mifumo yao ya kiuongozi ya kijadi na badala yake, mfumo wa kiutawala wa Kiarabu kushika hatamu visiwani humo. Hivyo, Waarabu walisababisha migogoro katika jamii za pwani ya Tanganyika na Zanzibar.

Miongoni mwa mbinu walizozitumia na Waarabu ni kuwagawa watawala wa jadi kwa kumuunga mkono mtawala aliyeonekana kuwa na nguvu zaidi kuliko wenzake na wale walioonekana kuwa wasaliti. Kwa upande wa Zanzibar, watawala wa jadi kama Mwinyi Mkuu alifanywa kuwa mshirika mwenza katika utawala. Waarabu walitumia uongozi wa mabavu, unyanyasaji na ukandamizaji kwa wananchi. Kwa mfano, wananchi walifanyishwa kazi ngumu bila malipo, walinyang'anywa ardhi yenye rutuba na Waafrika wengi walichukuliwa na kupelekwa sehemu zingine kama watumwa.

**Kazi ya kufanya 1.2**

Soma vitabu na matini mbalimbali kwenye mtandao, kisha fanya uchunguzi katika mfumo wa umiliki wa ardhi kabla na baada ya ujio wa Waarabu visiwani Zanzibar na Pemba. Uchunguzi wako ujikite katika maeneo yafuatayo:

(a) Namna mfumo wa umiliki wa ardhi ulivyokuwa kabla ya ujio wa utawala wa Waarabu;

(b) Mabadiliko yaliyoletwa na utawala wa Waarabu katika mfumo wa umiliki wa ardhi; na

(c) Athari zilizoletwa na mabadiliko katika mfumo wa umiliki wa ardhi.

### Mabadiliko ya kiuchumi wakati wa utawala wa Waarabu

Kuongezeka kwa mahitaji ya pembe za ndovu, karafuu, mafuta ya nazi na mpira katika viwanda vya Ulaya na Marekani kulimhamasisha sana Sultani wa Zanzibar pamoja na wafanyabiashara wa Kiarabu kuendeleza biashara ya bidhaa hizo. Hali kadhalika, mashamba makubwa ya mikarafuu na mpira yalianzishwa visiwani, jambo lililosababisha ongezeko la mahitaji ya nguvukazi hasa vibarua wa kupalilia, kuchuma karafuu na kuangua nazi.

Waarabu walifanya biashara na wenyeji wa pwani ya Tanganyika na Afrika Mashariki kwa ujumla. Katika biashara hiyo, walitafuta dhahabu, shaba, pembe za ndovu, magogo ya mikoko, nta na ngozi za wanyama pori kama vile chui na pundamilia. Vingine ni magamba ya konokono na kobe, pamoja na watumwa. Waarabu nao walileta bidhaa mbalimbali kama manukato, vyombo vya nyumbani, viungo vya

FOR ONLINE READING ONLY

chakula kama vile karafuu, mdalasini na tangawizi. Bidhaa nyingine zilikuwa shanga, majambia, bunduki, vioo vya kujitazamia na nguo. Kutokana na ustawi wa biashara hiyo, Zanzibar iliimarika na kuwa dola kuu ya kibiashara katika eneo la Afrika Mashariki likijumuisha pwani wa Bahari ya Hindi, mashariki mwa Kongo, Malawi and kaskazini mwa Msumbiji.

Biashara za masafa marefu katika ukanda wa Afrika Mashariki na Kati zilifanyika kwa kutumia njia kuu tatu zilizoanzia pwani kuelekea bara, kama inavyooneshwa kwenye Kielelezo 1.4. Njia ya Kaskazini ilianzia Saadani kuelekea Pangani hadi Mlima Kilimanjaro, kisha kuingia nchini Kenya. Njia ya kati ilianzia Bagamoyo kupitia Morogoro hadi Tabora. Ilipofika Tabora, iligawanyika katika matawi mawili: tawi la kwanza lilianzia Tabora kuelekea kaskazini huko Karagwe, Buganda na Bunyoro. Tawi la pili lilianzia Tabora kuelekea magharibi huko Ujiji, Burundi, Rwanda, Katanga na Umanyema huko Kongo. Njia hii ilimilikiwa zaidi na Wanyamwezi na Wasumbwa.




**Kielelezo 1.4:** *Njia kuu za biashara ya masafa marefu wakati wa utawala wa Waarabu*

FOR ONLINE READING ONLY

Mfanyabiashara maarufu wa Kiarabu katika njia hii ya kati alikuwa Hemed bin Muhammad bin Juma bin Rajab el Murjebi, maarufu kama "Tippu Tip". Njia kuu ya tatu ilikuwa ya Kusini. Njia hii ilianzia Kilwa Kivinje kuelekea Ziwa Nyasa, kaskazini mwa Msumbiji, Malawi na mashariki mwa Zambia. Njia hii ilitawaliwa na Wayao. Njia hizi zilitumika kupitisha bidhaa mbalimbali pamoja na misafara ya watumwa.

Ukuaji wa kilimo cha mazao ya biashara kama karafuu katika visiwa vya Pemba na Unguja na kilimo cha miwa huko Komoro, Ngazija, Mauritius na Reunion, ulisababisha ongezeko kubwa la mahitaji ya watumwa kutoka maeneo mbalimbali, hasa Tanganyika. Hii ilichangia kukua kwa biashara ya utumwa katika maeneo mengi ya eneo hili.

Kwa ujumla, katika kipindi cha utawala wa Waarabu, uchumi ulikuwa wa kinyonyaji, kwani Waarabu walikuwa wanufaika wakuu wa mapato, huku Waafrika wengi wakinyonywa kwa kufanya kazi kwa ujira mdogo na wengine wakigeuzwa kuwa watumwa. Watumwa hawa waliuzwa na wengine kutumikishwa katika mashamba makubwa ya mikarafuu na minazi ya Waarabu huko visiwani Unguja na Pemba.

**Zoezi la 1.2**

1. Fafanua namna ambavyo kushamiri kwa biashara kulivyoifanya Zanzibar kuwa dola kubwa na kitovu cha biashara katika ukanda wa Afrika Mashariki.
2. Eleza mabadiliko ya kiuchumi yaliyoletwa na Waarabu katika jamii za pwani ya Tanganyika na Zanzibar.
3. Linganisha thamani ya bidhaa zilizobadilishwa kati ya wafanyabiashara wa Kiarabu na jamii za pwani ya Tanganyika na Zanzibar.

### Mabadiliko ya kijamii wakati wa utawala wa Waarabu

Kabla ya kuwasili kwa Waarabu, jamii za pwani ya Tanganyika na Zanzibar zilijengwa juu ya maadili yaliyotokana na dini zao za jadi, ambapo baadhi yao waliabudu Mungu kupitia miti mikubwa, majabali na mapango makubwa, mito, maziwa na bahari na walitoa kafara kwa malengo mbalimbali kulingana na imani zao. Aidha, jamii hizi zilijikita katika kutoa elimu ya jadi ambayo ililenga kumpatia kijana maarifa na ujuzi wa kukabiliana na mazingira yake. Hii ilimwezesha kuishi vyema kwa kufuata maadili na mila za jamii yake. Kuja kwa Waarabu kulileta mabadiliko makubwa katika masuala ya elimu, maadili na utamaduni katika jamii hizi.

Jamii za pwani ya Tanganyika na Zanzibar zilijifunza lugha ya Kiarabu ili kuimudu dini ya Kiislamu na kuendana na matakwa na tamaduni za Waarabu. Hali hii ilisababisha watu wengi kujiunga na madrasa kwa ajili ya kujifunza dini ya Kiislamu na lugha

FOR ONLINE READING ONLY

ya Kiarabu, huku lugha ya Kiswahili ikiendelea kutumika kama lugha ya biashara na mawasiliano ya kila siku.

Mwingiliano baina ya Waarabu na jamii za pwani ulisababisha mabadiliko makubwa ya kitamaduni. Kwa mfano, uvaaji wa mavazi kama vile kanzu, baibui, baraghashia na makubadhi ulienea sana. Lugha ya Kiswahili pia ilianza kupata maneno mapya baada ya kutohoa baadhi ya msamiati kutoka lugha ya Kiarabu ili kurahisisha mawasiliano. Mfano wa baadhi ya maneno hayo ni kama vile *marhaba*, *shukrani*, *sheria*, *heshima*, *nzuri*, *labeka* na *hayati*. Jamii zilizoathiriwa zaidi na tamaduni za Kiarabu ni pamoja na Wahadimu, Watumbatu, Wapemba,Wazaramo na Wakwere kutokana na mwingiliano wao wa karibu katika shughuli za kila siku.

**Kazi ya kufanya 1.3**

Soma matini mbalimbali katika vitabu na mtandao kuhusu mabadiliko ya kijamii wakati wa utawala wa Waarabu kisha; tengeneza vibonzo vinavyoonyesha namna utamaduni, maadili na elimu vilivyobadilika baada ya ujio wa Waarabu.

## Utawala wa Wajerumani

Utawala wa Wajerumani katika Afrika Mashariki ya Kijerumani ulisukumwa na mabadiliko ya kiuchumi yaliyokuwa yakijitokeza barani Ulaya, ikiwemo nchini Ujerumani. Mabadiliko hayo yalitokana na kuongezeka kwa teknolojia iliyochochea mapinduzi ya viwanda yaliyoshika kasi kuanzia mwaka 1750 nchini Uingereza. Mapinduzi hayo yalisababisha uzalishaji mkubwa wa bidhaa na hivyo kuongeza mahitaji ya malighafi kwa ajili ya uzalishaji pamoja na masoko mapya na makubwa kwa ajili ya kuuza bidhaa hizo. Ili kukabiliana na changamoto hii, Wajerumani, pamoja na mataifa mengine ya Ulaya, walitafuta njia za kupata suluhisho kupitia nchi za nje.

Bara la Afrika lilionekana kuwa eneo muafaka kwa uwekezaji na utatuzi wa changamoto za upatikanaji wa malighafi na masoko. Katika robo ya mwisho ya karne ya 19, Wajerumani walifika Afrika Mashariki ya Kijerumani baada ya kupata taarifa kuhusu uwapo wa malighafi na soko la bidhaa. Taarifa hizo walizipata kutoka kwa wamisionari, wafanyabiashara na wapelelezi waliotumwa na makampuni ya Kijerumani hapa nchini. Hii iliwasaidia sana kuyatambua maeneo muhimu ya kuwekeza na kuanzisha mashamba makubwa ili kupata malighafi mbalimbali zilizohitajika katika viwanda vya Ujerumani.

Utawala wa Wajerumani katika eneo hili unaweza kugawanywa katika vipindi vifuatavyo: Kati ya mwaka 1886 hadi 1891. Kipindi hiki, Afrika Mashariki ya Kijerumani ilitawaliwa na Kampuni ya Kijerumani ya Afrika Mashariki chini ya uongozi wa mfanyabiashara Karl Peters. Kuanzia mwaka 1891 hadi 1918, serikali ya

FOR ONLINE READING ONLY

Ujerumani ilichukua rasmi mamlaka ya kutawala Afrika Mashariki ya Kijerumani. Wajerumani walikusudia kuimarisha utawala wao katika koloni hili kwa kuzitumia mbinu mbalimbali. Mbinu hizo zilijumuisha matumizi ya vyombo vya kiitikadi kama vile elimu na dini. Mbinu nyingine ilikuwa ni kuunda vyombo vya dola kama jeshi, magereza na mahakama za kikoloni ili kuhakikisha wananchi hawaupingi utawala wa kikoloni na wanazitii sheria zilizowekwa. Aidha, walitumia mbinu ya kuwapeleka watawala wazungu katika ngazi za uongozi na kuondoa tawala za jadi. Kwa ujumla, ujio wa Wajerumani ulileta mabadiliko makubwa ya kiuchumi, kisiasa na kijamii katika jamii za Kitanzania.

**Mabadiliko ya kiuchumi wakati wa utawala wa Wajerumani**

Kama ilivyosemwa awali, lengo kuu la Wajerumani kuja katika Afrika Mashariki ya Kijerumani lilikuwa kutafuta suluhisho la changamoto za kiuchumi zilizotokana na mapinduzi ya viwanda, kama vile upungufu wa masoko na malighafi, kwa viwanda vyao barani Ulaya. Kwa hivyo, kupitia ukoloni, wakoloni waliweza kuzipunguza changamoto hizo kwa kuanzisha uchumi wa kikoloni ambao ulileta mabadiliko makubwa kwenye jamii za Kitanzania. Shughuli za uzalishaji mali zilitegemea sana uzalishaji wa mazao ya biashara kama vile kahawa, chai, mkonge, pamba, tumbaku na mpira. Mazao haya yalilimwa katika maeneo mbalimbali ya Afrika Mashariki ya Kijerumani. Kwa mfano, kahawa ililimwa Bukoba, Kilimanjaro, Arusha na Tukuyu; pamba ilianza kulimwa katika maeneo ya Mwanza, Shinyanga, Morogoro, Bagamoyo, Rufiji na Lindi; katani ililimwa huko Tanga, Morogoro, Lushoto, Lindi, Dar es Salaam na Pwani; mpira ulilimwa maeneo ya pwani hasa katika bonde la mto Pangani huko Tanga na bonde la mto Rufiji hasa maeneo ya Mohoro. Walowezi wa Kijerumani walianzisha mashamba ya katani yenye ukubwa wa ekari zaidi ya 100,000 (hekta 40,000). Walowezi wengine walipanda zaidi ya miche milioni mbili ya kahawa, ekari 200,000 (hekta 81,000) za miti ya mipira na mashamba ya pamba. Maeneo ya Rukwa, Kigoma, Mtwara, Dodoma na Singida hayakuruhusiwa kuanzisha kilimo cha mashamba makubwa kwa sababu yalitengwa maalumu kwa ajili ya kutoa wafanyakazi na vibarua (manamba) watakaofanya kazi katika mashamba makubwa ya walowezi na migodi ya madini hasa dhahabu huko Chunya, Sekenke na Mwanza.

Kwa upande wa viwanda, Wajerumani hawakuanzisha viwanda vikubwa bali walijenga viwanda vidogo, hasa vya kuchakata malighafi ili kupunguza uzito wake kabla ya kusafirishwa kwenda Ujerumani. Kwa mfano, walijenga vinu vya kukoboa kahawa, kuchambua pamba na kusindika mkonge. Wajerumani walijenga viwanda vidogovidogo vya kuzalisha viatu, viberiti, baruti na risasi. Hivyo, Wajerumani hawakujenga viwanda vikubwa vya kuzalisha bidhaa mbalimbali za viwandani kama vile nguo, kamba na mazulia, bali walilenga kurahisisha usafirishaji wa malighafi tu.

Vilevile, Wajerumani waliendesha biashara ya kinyonyaji, kwani koloni hili lilitumika kama soko la kuuzia bidhaa za viwandani kutoka Ujerumani, kama vile nguo, baiskeli,

FOR ONLINE READING ONLY

mapanga, majembe, viatu na sigara. Bidhaa hizi zote ziliuzwa kwa bei kubwa, wakati malighafi zilizotumika kuzalisha bidhaa hizo zilinunuliwa kwa bei ndogo sana.

**Zoezi la 1.3**

1. Fafanua sababu zilizowafanya Wajerumani kuanzisha utawala wa kikoloni katika jamii za Kitanzania.
2. Kwa nini Wajerumani walijenga viwanda vidogo badala ya viwanda vikubwa katika Afrika Mashariki ya Kijerumani?
3. Eleza athari ambazo zingetokea iwapo Wajerumani wangejenga viwanda vikubwa vya kuchakata malighafi katika Afrika Mashariki ya Kijerumani.

FOR ONLINE READING ONLY

### Mabadiliko ya kijamii wakati wa utawala wa Wajerumani

Wajerumani walilazimika kujenga na kutoa huduma kadhaa ili kufanikisha malengo yao katika Afrika Mashariki ya Kijerumani. Huduma hizi zilijumuisha elimu, afya, maji na umeme, pamoja na miundombinu ya mawasiliano.

*Elimu*

Elimu iliyotolewa na Wajerumani ililenga kukidhi mahitaji ya shughuli zao za kikoloni. Mfumo wa elimu uliundwa mahususi ili kuandaa wasaidizi watakaowasaidia Wajerumani katika shughuli hizo. Elimu hiyo ililenga zaidi wananchi wachache ambao wangeweza kuzalisha malighafi kwa ajili ya kukidhi mahitaji ya uchumi wa kikoloni. Malengo ya elimu hiyo yalikuwa yafuatayo:

(a) Kueneza utamaduni wa Kijerumani;

(b) Kuandaa watumishi wa ngazi za chini;

(c) Kufundisha uadilifu na maadili ya kazi; na

(d) Kuandaa wazalishaji mali kwa ajili ya uchumi wa Kijerumani.

Ili kutimiza malengo hayo, mtaala wa elimu ya Kijerumani ulifundisha stadi kama vile uashi, useremala, ukarani, upigaji picha, ufundi wa kushona na utengenezaji wa viatu. Shule mbalimbali zilianzishwa na kugawanywa katika makundi mawili: shule za Wamisionari na shule za serikali. Hata hivyo, mtaala wa shule za serikali ulipingwa na Wamisionari ambao walitaka utumike mtaala wa shule zao. Elimu ilitolewa kwa lugha ya Kiswahili, huku shule za serikali zikihudumia zaidi wavulana na wasichana wakibaguliwa. Mfumo huu wa elimu ya kikoloni ulikuwa na idadi ndogo ya wanafunzi wa Kiafrika.

*Afya*

Huduma za afya katika kipindi cha ukoloni zilitolewa kwa ubaguzi wa rangi, ambapo huduma hizo zilipatikana katika maeneo ambayo wakoloni walianzisha shughuli kubwa za uzalishaji mali kama vile mashamba na makazi yao. Wazawa walipata matibabu ya kiwango cha chini ukilinganisha na Wazungu na Waasia. Matibabu haya yalilenga kuwawezesha Waafrika kuzalisha malighafi bila kusumbuliwa na magonjwa hasa ya kitropiki au kuumia wakiwa kazini. Aidha, huduma za afya zilitilia mkazo matibabu badala ya kinga dhidi ya magonjwa. Madhumuni ya kueneza huduma hizi yalikuwa ni kuhakikisha kwamba wazalishaji mali katika maeneo hayo wanakuwa na afya njema ili waweze kufanikisha malengo ya kikoloni.

Athari hasi za huduma hizi zilikuwa ni kupotea kwa umaarufu kwa waganga na matabibu wa jadi, pamoja na dawa zao kushuka thamani. Hii ilisababishwa na ongezeko la vituo vya matibabu na matumizi ya dawa za kigeni. Hata hivyo, bado waganga wa jadi waliendelea kutoa matibabu, hasa katika maeneo ya vijijini.

*Huduma za maji na umeme*

Katika kipindi cha ukoloni, huduma za maji na umeme zilitolewa kwa ubaguzi na upendeleo, kwani huduma hizi zilielekezwa zaidi katika maeneo yenye umuhimu wa kiuchumi. Kwa mfano, usambazaji wa huduma hizi ulifanyika katika migodi, viwandani, maeneo ya mijini, mashamba makubwa ya wakoloni na makazi ya walowezi wa Kizungu na Kiasia.

*Miundombinu ya mawasiliano*

Wakoloni walijenga njia za uchukuzi na mawasiliano kama vile barabara, reli na bandari. Miundombinu hii ilikuwa muhimu kwa usafirishaji wa malighafi, bidhaa na watu. Reli na barabara zilijengwa kutoka maeneo ya uzalishaji wa malighafi hadi bandarini. Malighafi kutoka makoloni ilisafirishwa kwenda Ulaya na bidhaa za viwandani kutoka Ulaya kama vile nguo, vyombo vya nyumbani na zana za chuma ziliingizwa kupitia bandari hizo na kuletwa Afrika Mashariki ya Kijerumani.

**Kazi ya kufanya 1.4**

Kwa kusoma matini katika vitabu na mtandaoni, fanya utafiti mdogo kuhusu tiba za jadi wakati wa ujio wa Wajerumani. Utafiti wako ujikite katika maeneo yafuatayo:

(a) Namna tiba za jadi zilivyokuwa kabla ya ujio wa Wajerumani;

(b) Magonjwa yaliyotibiwa kwa kutumia tiba za jadi;

(c) Namna Wajerumani walivyoathiri tiba za jadi; na

(d) Toa ushauri kuhusu umuhimu wa tiba za jadi kwa jamii za sasa za Kitanzania.

FOR ONLINE READING ONLY

**Jamii zilivyoathirika na utawala wa Wajerumani**

Wajerumani walijenga himaya yao ya kikoloni katika Afrika Mashariki ya Kijerumani kuanzia mwaka 1885. Ili kufanikisha malengo yao ya kiuchumi, Wajerumani walianza kutafuta njia mbalimbali za kiuchumi zilizoweza kuwaletea faida. Miongoni mwa njia hizo, walitafuta maeneo mapya ya kibiashara, ambapo walijipenyeza katika maeneo ya bara kwa kufuata njia za biashara ya masafa marefu zilizotumiwa na jamii za Kitanzania kabla ya ukoloni. Wakati huohuo, walijenga ngome za kijeshi na vituo vikubwa huku wakiwabadilisha au kuwaondoa kwa nguvu watawala wa jadi waliokuwepo. Walianzisha mfumo wa utawala uliokuwa chini ya liwali na maakida, ambao aghalabu walikuwa Waarabu na watu kutoka sehemu nyingine za Afrika, hususani Waswahili. Kwa ujumla, karibu jamii zote katika Afrika Mashariki ya Kijerumani ziliathiriwa na utawala wa Wajerumani. Kwa mfano, baadhi ya jamii zilizoathirika ni pamoja na Wanyamwezi, Wazigua, Wayao, Wangindo, Wamatumbi, Wambunga, Wahehe, Wachaga, Wameru na Waha.

Jamii za Kitanzania zilizokuwa zimezoea kujitawala, zilivurugwa na kuja kwa utawala wa Wajerumani. Wajerumani waliweka vibaraka waliotii sheria na matakwa yao. Katika maeneo fulani au wilaya, walianzisha utawala wa kijeshi na kuondoa kabisa utawala wa jadi, kama ilivyokuwa Iringa na Mahenge. Hivyo, wazawa walipoteza nguvu yao ya kujitawala.

Wajerumani waliwataka wenyeji kulipa kodi, lakini wenyeji walikataa na hatimaye machafuko na vita kadhaa vilizuka. Kwa mfano, mwaka 1898, kulizuka Vita ya Maboga ambapo Wamatumbi walishindwa. Wamatumbi wa Kilwa na Wangindo wa Liwale pia waliathirika kutokana na kulipwa ujira mdogo, kufanya kazi za sulubu, kulipa kodi ya rupia tatu na kuadhibiwa vikali kwa makosa mbalimbali. Vilevile, utawala wa Kijerumani ulisababisha kutothaminiwa kwa utu wa wanajamii wengi. Wazazi au watu wazima walidhalilishwa mbele ya watoto wao, kwa mfano, kuchapwa viboko pale waliposhindwa kulipa kodi ya kichwa au walipotenda makosa madogo madogo.

Utawala wa Kijerumani ulisababisha utengano miongoni mwa jamii za Kitanzania. Kwa mfano, Mangi Marealle wa Wachaga wa Marangu aliungana na Wajerumani kumpiga Mangi Meli wa Moshi. Kwa ujumla, jamii za Kitanzania zilipata athari katika uchumi na hata kisiasa, kwani mfumo wao wa kujitawala ulibadilishwa. Hali hii iliwapa ujasiri wa kudai uhuru wao kwa njia na mbinu mbalimbali, ikiwemo vita.

FOR ONLINE READING ONLY

**Zoezi la 1.4**

1. *Fafanua namna mabadiliko katika mfumo wa utawala wa jadi kufuatia kuja kwa Wajerumani yalivyoathiri jamii za Kitanzania.*
2. *Kwa nini jamii za Kitanzania zilipinga ulipaji wa kodi ulioanzishwa na utawala wa Kijerumani?*
3. *Unajifunza nini kutoka kwa mababu na mabibi zetu waliopinga mfumo na utawala wa Kijerumani?*

## Utawala wa Waingereza Tanganyika na Zanzibar

*Afrika Mashariki ya Kijerumani ilikuwa sehemu ya koloni la Ujerumani hadi kumalizika kwa Vita Kuu ya Kwanza ya Dunia mwaka 1918. Wakati wa vita hivyo, koloni la hili lilitekwa na majeshi ya Uingereza na Ubelgiji. Mkataba wa Amani wa Versailles wa mwaka 1919 uliamua kwamba makoloni yote yaliyokuwa ya Wajerumani yakabidhiwe mataifa yaliyoshinda vita hivyo. Hivyo, Afrika Mashariki ya Kijerumani ilikabidhiwa rasmi kwa Waingereza chini ya udhamini wa Jumuiya ya Kimataifa (League of Nations).*

*Kwa upande wa Zanzibar, utawala wa Waingereza ulianza baada ya kutiwa saini kwa mkataba wa pili kati ya Wajerumani na Waingereza. Mkataba huo ulisainiwa tarehe 1 Julai, 1890, unaojulikana kama Mkataba wa Heligoland. Kulingana na mkataba huo, Uingereza ilipewa mamlaka ya kuiweka Zanzibar chini ya himaya yake kwa makubaliano na mtawala wa wakati huo, Sayyid Ali bin Said.*

*Jamii za Tanganyika na Zanzibar wakati huo zilifuata mwelekeo wa kiuchumi, kisiasa na kijamii ulioanzishwa na Waingereza. Ili kuimarisha ukoloni, Waingereza walibadilisha mfumo wa utawala uliokuwapo na kuanzisha mfumo wa kiuwakala ambao ulibadilisha pia uchumi, siasa na utamaduni wa Tanganyika. Jambo muhimu la kufahamu ni kwamba, ni utawala wa Kiingereza uliobadilisha jina la koloni hilo kutoka Afrika Mashariki ya Kijerumani na kuwa Tanganyika.*

### Mabadiliko ya kiuchumi wakati wa utawala wa Waingereza

*Mabadiliko ya kiuchumi wakati wa utawala wa Waingereza yalilenga kuendeleza kilimo, biashara na viwanda vidogovidogo. Kwa upande wa kilimo, utawala wa Waingereza ulihamasisha kilimo cha mazao ya biashara kama vile kahawa, pamba, mkonge, chai na pareto. Serikali hiyo pia iliwahimiza walowezi kufufua mazao ya biashara ambayo yalikuwa yameathiriwa na vita. Walowezi hawa walitoka mataifa mbalimbali kama Uingereza, Afrika Kusini, Ugiriki na India. Lengo kubwa la kufufua* mazao haya ya biashara lilikuwa kupata malighafi za kutosha kwa ajili ya viwanda *nchini kwao Uingereza.*

FOR ONLINE READING ONLY

Hata hivyo, wakati Waingereza walipopewa idhini ya kutawala Tanganyika na Zanzibar, wananchi walikuwa tayari wanajishughulisha na kilimo cha mazao ya biashara, kama vile buni iliyolimwa Moshi na Bukoba. Pamba nayo ilikuwa ikilimwa katika maeneo ya Mwanza, Shinyanga, Morogoro na Pwani. Shughuli za biashara wakati wa utawala wa Waingereza zilifanywa na watu wa jamii ya Kiasia, hasa Waarabu na Wahindi. Jamii hii ilijihusisha na biashara ya kununua mazao kutoka kwa wakulima na kuyauza kwa makampuni ya kibepari ya Wazungu. Pia, walifanya biashara ya kuuza bidhaa mbalimbali zilizoagizwa kutoka Ulaya magharibi na Marekani. Watanganyika na Wazanzibari hawakuruhusiwa kushiriki katika biashara wakati wa utawala huo. Waingereza, Wagiriki na Wahindi ndio waliofanya biashara ya kuagiza na kusafirisha nje ya koloni bidhaa mbalimbali. Waarabu na Wahindi walifanya biashara ya maduka ya rejareja maeneo ya mijini na vijijini.

Kwa upande wa viwanda, Waingereza hawakuwekeza sana katika viwanda vikubwa ila walianzisha viwanda vidogo vidogo. Serikali ya Waingereza ilikusanya malighafi kama vile mazao ya kilimo, madini na mifugo na kuzisafirisha kwenda kwenye viwanda vyao huko Uingereza. Bidhaa zilizozalishwa huko zililetwa na kuuzwa kama bidhaa za viwandani hapa nchini. Viwanda vilivyokuwa hapa vilijikita zaidi katika kuchakata malighafi ili kupunguza uzito kabla ya kusafirishwa. Kwa mfano, viwanda vya kusindika buni, katani, karanga na pamba, pamoja na viwanda vya kukaushia tumbaku vilianzishwa. Waingereza pia waliendeleza uchimbaji wa madini kwa kupanua migodi iliyoachwa na Wajerumani na kuanzisha mingine mipya, kama migodi ya chumvi huko Uvinza na Ulanga na migodi ya dhahabu huko Chunya na Geita.

Usafirishaji na uchukuzi ni baadhi ya shughuli za kiuchumi zilizopewa kipaumbele na serikali ya Waingereza. Juhudi za kufufua miundombinu iliyoharibiwa na vita zilifanyika, ikiwemo kukamilisha ujenzi wa reli katika baadhi ya maeneo kama vile reli kutoka Tabora hadi Mwanza na reli kutoka Moshi hadi Arusha. Pia, bandari na usafiri wa meli katika Ziwa Tanganyika na ziwa Viktoria uliimarishwa. Lengo la kuimarisha usafirishaji na uchukuzi lilikuwa kurahisisha usafirishaji wa malighafi kutoka maeneo ya uzalishaji hadi bandari za Dar es Salaam, Tanga na Mtwara tayari kwa kusafirishwa Ulaya. Vilevile, njia hizi za usafirishaji ziliwezesha bidhaa za viwandani kusafirishwa kutoka bandarini kuelekea masoko ya maeneo ya bara.

Kwa upande wa Zanzibar, Waingereza waliwatumia Waarabu na Wahindi kuendeleza masilahi yao ya kiuchumi. Waarabu walipewa ardhi yenye rutuba kwa ajili ya kilimo cha mikarafuu na minazi, wakati Wazanzibari wengi walipewa ardhi isiyo na rutuba. Wahindi walipewa jukumu la kusimamia biashara, hivyo walijenga shule ili kuendeleza uzoefu wao. Mnamo mwaka 1923, shule kwa ajili ya watoto wa Kihindi zilianzishwa.

FOR ONLINE READING ONLY

**Kazi ya kufanya 1.5**

*Shule yako imealikwa kushiriki mdahalo katika shule ya jirani; andaa hoja utakazotumia katika mdahalo huo kuhusu mada inayosomeka, "Utawala wa Waingereza ulikuwa na manufaa makubwa ya kiuchumi katika jamii za Tanganyika na Zanzibar."*

## Mabadiliko ya kisiasa wakati wa utawala wa Waingereza

*Baada ya Waingereza kukabidhiwa rasmi madaraka, serikali iliimarisha misingi ya utawala kwa kuweka taratibu na sheria ili kurejesha hali ya utulivu iliyotoweka wakati wa vita. Awali, Waingereza waliendelea kutumia mtindo wa utawala uliokuwa ukitumiwa na Wajerumani. Hata hivyo, baadaye walibadilisha mfumo wa utawala kwa kuanza kuwatumia viongozi wa jadi katika shughuli za utawala. Viongozi hawa walikuwa na majukumu ya kusimamia maagizo ya serikali, kukusanya kodi, kufanya sensa ya watu na mifugo, kuwa na daftari la walipa kodi na kuamua kesi* zilizofikishwa katika mahakama zao. Majukumu haya yalitekelezwa chini ya *usimamizi wa mabwana shauri wa Kiingereza waliokuwa na jukumu la kufafanua sheria za kikoloni kwa wananchi.*

*Mtindo wa kisiasa wa kuwatumia machifu ulikuwa ni chombo cha kuendeleza mipango ya ukoloni ya kuwakandamiza na kuwanyonya wananchi. Waingereza walisisitiza sana ukabila katika mipango yao ili kuwagawa na kuwadhibiti wananchi. Kwa mfano, kwenye mashamba na migodi, vibarua walipangiwa mabweni ya kulala kwa misingi ya kikabila. Aidha, ubaguzi ulionekana katika shule na hata kwenye mashindano ya ngoma na michezo ya jadi.*

*Ili kuimarisha utawala wa Waingereza, sheria na kanuni mbalimbali zilitungwa kwa lengo la kuwakandamiza wananchi. Sheria zote hizi zililenga kuwanufaisha Wazungu na Waasia. Wakoloni walitumia mbinu za kuwalaghai machifu kwa kuunda shirikisho la machifu kwa kila kabila na kumteua chifu mmoja kuwa kiongozi mwandamizi wa wengine. Kwa mfano, Marealle aliteuliwa kuongoza machifu wa Kichaga, Fundikira aliteuliwa kuongoza machifu wa Kinyamwezi, Makwaia aliteuliwa kuongoza machifu wa Kisukuma na Chifu Luther Kingu alichaguliwa kuongoza machifu wa Iramba.*

*Waingereza walitumia mtindo wa utawala uliokuwa ukijulikana kama utawala wa kiuwakala ulioanzishwa na Gavana Sir Donald Cameron mwaka 1926. Mtindo huu uliendeshwa kwa kutumia makamishna wa majimbo na wilaya. Makamishna wa wilaya ndio waliokuwa kiungo kati ya serikali ya kikoloni na serikali za mitaa zilizoongozwa na machifu wakisaidiwa na majumbe.*

FOR ONLINE READING ONLY

Baada ya Vita Kuu ya Pili ya Dunia, Waingereza walipanua Baraza la Kutunga Sheria. Baraza hili lilikuwa na kazi ya kumshauri Gavana kuhusu masuala mbalimbali yanayohusu utawala. Jukumu jingine la baraza lilikuwa ni kutunga sheria ambazo zilihitaji idhini kutoka serikali ya Uingereza kabla ya kutumika. Wajumbe wa Baraza la Kutunga Sheria waliingia kwa kuteuliwa na Gavana mwenyewe, huku wengine wakiteuliwa kutokana na nyadhifa zao serikalini. Baraza hili kwa mara ya kwanza lilijumuisha machifu wa Kitanganyika, wakiwemo Chifu Abdieli Shangali na Chifu Kidaha Makwaia.

Zanzibar ilikuwa na uhusiano maalumu na Waingereza, lakini kwa hali halisi, siasa ya Waingereza iliifanya Zanzibar kuwa koloni. Ingawa Waingereza waliutumia utawala wa Sultani katika kuitawala Zanzibar, utawala wa Kisultani haukujitegemea hata mara moja. Mwanzoni mwa mwaka 1914, Baraza la Ushauri lilianzishwa kwa lengo la kumshauri Sultani na serikali yake kuhusu masuala ya serikali. Unguja na Pemba ziligawanywa katika wilaya, *mudiria* na *shehia*. Kila wilaya ilikuwa chini ya afisa wa serikali ambaye alikuwa Mwingereza, huku *Mudir* na *Sheha* wa Kiarabu wakisimamia mudiria na shehia. Hata hivyo, kulikuwa na Waafrika wachache waliokuwa wakisimamia shehia, lakini walipewa jukumu la kuwahimiza wenzao kuwatumikia Wazungu, Waarabu na Wahindi.

**Zoezi la 1.5**

1. Tofautisha mfumo wa utawala wa Waingereza na ule wa Wajerumani katika kuzitawala jamii za Kitanzania.
2. Eleza kwa kifupi majukumu ya viongozi wa jadi katika serikali ya Kiingereza.
3. Linganisha majukumu ya viongozi wa sasa wa serikali za mitaa na yale ya viongozi wa jadi wakati wa utawala wa Waingereza Tanganyika.
4. Tofautisha utawala wa Waingereza Tanganyika na Zanzibar.

FOR ONLINE READING ONLY

### Mabadiliko ya kijamii wakati wa utawala wa Waingereza

Mabadiliko ya kijamii wakati wa utawala wa Waingereza yalijikita zaidi katika utoaji wa huduma za msingi kama elimu, afya, maji, umeme na miundombinu. Huduma hizi zilitolewa kwa madhumuni ya kuiwezesha serikali ya Waingereza kurahisisha utekelezaji wa malengo ya kikoloni, ikiwemo kupata nguvukazi ya kutosha miongoni mwa wananchi ili kuwezesha uzalishaji wa malighafi muhimu kwa viwanda vyao huko Ulaya. Kwa kiasi kikubwa, huduma za jamii zilizoanzishwa na serikali ya kikoloni hazikulenga kuwahudumia wananchi bali kutimiza masilahi ya wakoloni.

*Elimu:* Shughuli za utoaji wa elimu ziliathirika sana wakati wa Vita Kuu ya Kwanza ya Dunia. Serikali ya Uingereza, kwa kushirikiana na mashirika ya dini, ilianza kutoa elimu kwa wananchi kwa kufuata mipango na mahitaji ya wakoloni. Sehemu

zilizopewa kipaumbele ni zile zilizozalisha mazao ya biashara, hususani kahawa na pamba, pamoja na vituo vya wamisionari. Kwa mfano, shule nyingi katika Tanganyika zilijengwa katika maeneo ya Kilimanjaro na Bukoba.

Malengo ya elimu iliyotolewa na Waingereza yalikuwa kuwapatia wananchi maarifa yatakayowasaidia kuendeleza mipango na mikakati ya kikoloni. Hii ilifanywa kwa kuwapa wananchi elimu ya mbinu bora za kilimo na ufugaji na elimu ya afya. Pia, iliwaandaa mabwanyenye uchwara ambao walisaidia kuongoza na kufundisha utii na unyenyekevu ili kutekeleza maagizo na maelekezo ya serikali ya kikoloni. Elimu ilitolewa katika ngazi zifuatazo: elimu ya msingi (darasa la 1- 4), elimu ya kati (darasa la 5-8) na elimu ya sekondari (darasa la 9-12). Mtaala wa elimu ulijikita zaidi katika kufundisha mambo ya kigeni, hivyo maudhui yaliyofundishwa shuleni hayakuwasaidia wananchi kutatua matatizo yao ya kila siku. Kwa mfano, wanafunzi walifundishwa kuhusu mila, tamaduni na desturi za Kiingereza badala ya mila zao za asili.

Kwa upande wa Zanzibar, Waingereza walitoa elimu iliyoendeleza matabaka ya kijamii. Wazanzibari walifundishwa jinsi ya kuwa watiifu na waaminifu kwa Sultani na viongozi wao, ambao wengi walikuwa Waarabu. Waarabu walipewa elimu maalumu iliyowawezesha kuendelea kujiona kuwa bora kuliko Waafrika. Ubaguzi huu katika utoaji wa elimu ulikuwa kikwazo kikubwa kwa Watanganyika na Wazanzibari.

Aidha, ubaguzi wa kikanda na kimaeneo ulikuwa dhahiri katika mfumo wa elimu, ambapo shule nyingi zilijengwa katika maeneo ya uzalishaji mali kama Moshi, Bukoba, Mbeya na Mwanza. Maeneo ya Rukwa na Kigoma yalikuwa na shule chache kwa kuwa hayakuwa maeneo ya uzalishaji mali. Hivyo, wananchi wa maeneo haya walinyimwa fursa za elimu. Wananchi hawa waliendelea kwenda kufanya kazi za manamba katika mashamba na migodi ya kikoloni. Hivyo, elimu iliyotolewa iliwafaidisha wachache pekee kwani hata shule zilikuwa chache na zilitoa elimu kwa watoto wa machifu. Kwa mfano, Shule ya Wavulana Tabora ilikuwa maalumu kwa watoto wa machifu.

*Afya:* Huduma za afya wakati wa utawala wa Waingereza zilitolewa kwa lengo la kuziendeleza na kuzilinda afya za wananchi ili wawe na nguvu za kushiriki kikamilifu katika shughuli za kuendeleza uchumi wa kikoloni. Pamoja na kwamba Waingereza walihitaji nguvukazi yenye afya, bado huduma za afya zilikuwa chache na duni. Sehemu zilizopata huduma za afya ni zile zilizo kwenye maeneo ya uzalishaji mali, makazi ya walowezi na vituo vya wamisionari.

Kama ilivyokuwa katika elimu, huduma za afya pia zilitolewa kwa misingi ya ubaguzi wa rangi. Huduma bora zaidi zilitolewa kwa Wazungu, wakifuatiwa na Waasia, huku Waafrika wakipewa huduma za kiwango cha chini. Waingereza hawakuwaandaa Waafrika kuwa matabibu wa ngazi za juu, bali walifundishwa kuwa matabibu wa ngazi za chini. Vilevile, hospitali na vituo vya afya vilifuata misingi hiyo ya ubaguzi,

FOR ONLINE READING ONLY

ambapo kulikuwa na hospitali maalumu kwa Wazungu na nyingine kwa ajili ya watu wenye rangi nyingine. Kwa mfano, Hospitali ya *Ocean Road* ilikuwa maalumu kwa Wazungu, kwa kuwa ilitoa huduma bora zaidi.

*Miundombinu:* Katika kutekeleza mpango wa ukoloni wa kupata malighafi muhimu kwa ajili ya viwanda vya Ulaya, Waingereza waliendelea kufufua na kuanzisha miundombinu kutoka maeneo ya pwani hadi maeneo ya uzalishaji mali kama migodi na mashamba ya pamba, mkonge na kahawa. Miundombinu iliyojengwa ni pamoja na barabara, reli na bandari. Reli kutoka Tabora hadi Mwanza ilikamilishwa mwaka 1928. Pia, usafiri katika Ziwa Tanganyika na Viktoria uliimarishwa. Bandari za Tanga na Dar es Salaam, ambazo zilikuwa zimeathiriwa na vita, zilikarabatiwa. Waingereza pia walijenga bandari ya Mtwara. Aidha, miundombinu mingine ya reli iliongezwa kwa lengo la kusafirisha malighafi na vibarua kutoka sehemu mbalimbali za nchi, kama inavyoonekana kwenye Kielelezo 1.5.




**Kielelezo 1.5:** *Miundombinu ya reli wakati wa utawala wa Waingereza*

Miundombinu ya barabara, reli na usafiri wa majini ililenga kuunganisha maeneo muhimu ya uzalishaji mali, kama vile mashamba ya mkonge, pamba, karanga na

FOR ONLINE READING ONLY

kahawa na yale maeneo waliyotokea manamba. Hivyo, miundombinu hiyo wakati wa utawala wa Waingereza ilisaidia katika kuwasafirisha manamba kwenda kufanya kazi kwenye mashamba na migodi. Pia, miundombinu ya barabara na reli ilitumika kusafirisha malighafi kutoka bara hadi bandarini, kusambaza bidhaa za viwandani kutoka bandarini hadi bara. Vilevile, kusafirisha askari kwenda maeneo yaliyokuwa na upinzani na hatimaye, kusafirisha watawala kwenda kusimamia shughuli katika maeneo mbalimbali. Huduma za usafirishaji wakati wa utawala wa Waingereza hazikulenga moja kwa moja kuwanufaisha Waafrika kama abiria, bali zililenga kurahisisha mipango na matakwa ya kikoloni ya unyonyaji na ukandamizaji wa wananchi, pamoja na kusafirisha malighafi kwenda Ulaya kwa ajili ya viwanda vyao.

*Huduma za maji na umeme:* Serikali ya Uingereza ilijitahidi kuwapa wananchi wa Tanganyika na Zanzibar huduma za maji na umeme ili kuwawezesha kuwa na afya bora ili kuendelea kuzalisha malighafi. Baada ya Vita Kuu ya Pili ya Dunia, serikali ilipanua huduma hizi, upanuzi ambao ulifanyika zaidi katika maeneo ya mijini na ya uzalishaji. Maeneo hayo ni kama vile mashamba ya kikoloni, migodini na mahali walipoishi watawala wa kikoloni.

Ubaguzi wa rangi ulijitokeza katika utoaji wa huduma za maji na umeme. Ubaguzi huu ulidhihirika zaidi katika maeneo ya mijini. Huko huduma bora za maji na umeme walipatiwa kwanza Wazungu, wakifuatiwa na Waasia na hatimaye Waafrika. Kutokana na hali hii, baadhi ya maeneo ya miji mikubwa kama Dar es Salaam na Mwanza yalijulikana kama Uzunguni na Uhindini. Maeneo ya mjini walipokaa Waafrika wengi yaliitwa maeneo ya Uswahilini. Maeneo ya vijijini yalipatiwa huduma duni zaidi ikilinganishwa na yale ya mijini, hali iliyosababisha watu wa vijijini kuhangaika kutafuta huduma za maji na umeme. Maeneo ya vijijini yaliendelea kutumia kuni, koroboi na taa za chemli kutoa mwanga wakati wa usiku.

## Mchango wa ukoloni katika uhusiano wa Tanzania na mataifa yaliyoitawala

Kabla ya ujio wa wakoloni, jamii za Kitanzania zilikuwa na uhusiano wa kuheshimiana na kushirikiana na jamii nyingine za Afrika na kwingineko. Uhusiano huu ulijengwa kwa misingi ya biashara, ambapo jamii hizo zilibadilishana bidhaa kama vile dhahabu, pembe za ndovu na vyakula. Ushirikiano huu ulizingatia maadili ya kutegemeana, kusaidiana na kuaminiana. Biashara iliyofanyika kati ya jamii hizi ilichangia kuchochea maendeleo ya kijamii na kiuchumi.

Hali hii ya ushirikiano ilianza kubadilika baada ya ujio wa wakoloni kutoka Ulaya Magharibi. Mataifa ya Ulaya, hususani Ujerumani na Uingereza, yalitawala maeneo mbalimbali kwa lengo la kunyonya rasilimali za jamii za Kitanzania. Wakoloni walivunja uhusiano wa asili uliokuwepo kwa kuanzisha mipaka mipya na kuleta maadili ya kikoloni. Pia, waliweka sera mpya zilizovuruga maadili ya kijamii ya Kitanzania, ambayo yalijengwa katika misingi ya utu, upendo, umoja, kusaidiana na kuheshimiana kama jamii huru.

Baada ya ukoloni kushamiri, uhusiano kati ya jamii za Kitanzania na wakoloni uliingia katika hali ya uhasama mkubwa. Mataifa ya kikoloni ya Ulaya Magharibi yalitumia

FOR ONLINE READING ONLY

mbinu za kijeshi na kisiasa kutawala jamii za Kitanzania. Hali hii ilileta migongano ya mara kwa mara. Wazawa walilazimika kupigania na kulinda ardhi zao, utu na uhuru wao dhidi ya utawala wa kigeni. Hali hii lilisababisha uadui kati ya wakoloni na jamii mbalimbali za Kitanzania.

Ukoloni uliathiri kwa kiasi kikubwa uhusiano wa kijamii na kiuchumi wa jamii za Kitanzania. Uhusiano wa kibiashara uliokuwa na mafanikio zamani sasa ulibadilika na kuwa wa kiunyonyaji. Wakoloni walipora rasilimali kama vile ardhi na madini na kuwanyonya wafanyakazi wa Kitanzania katika mashamba na migodi yao. Hii ilisababisha kuongezeka kwa umasikini na ukosefu wa haki miongoni mwa Watanzania.

Mbali na uhasama, ukoloni pia ulileta athari kubwa kwenye utamaduni na mifumo ya kijamii. Utamaduni wa kigeni ulienea katika jamii za Kitanzania na kudhoofisha utamaduni na maadili ya asili. Hali hii ilichangia kuvunjika kwa mshikamano wa kijamii na kuendeleza uhusiano hasi kati ya jamii za Kitanzania na wakoloni.

Ingawa ukoloni ulisababisha uhusiano mbaya baina yake na jamii za Kitanzania, pia ulisababisha mwamko mpya wa utaifa wa kudai uhuru. Harakati za kudai uhuru na kujikomboa zilichochea umoja miongoni mwa jamii za Kitanzania. Baada ya Tanganyika kupata uhuru mwaka 1961, uhusiano mpya ulijengwa kati ya Tanganyika huru na mataifa ya kigeni, yakiwemo mataifa yaliyokuwa yakiitawala. Uhusiano huu ulijengwa katika misingi ya kimaadili iliyolenga kuimarisha umoja wa kitaifa, kulinda uhuru, kujitegemea na kuheshimu haki za binadamu. Katika kipindi hicho cha uhuru wa Tanganyika na mara baada ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, Tanzania ilijipambanua kama taifa lenye msimamo huru katika uhusiano wake na mataifa mengine.

## Zoezi la marudio

1. Eleza sababu za wakoloni kutoanzisha viwanda vya kuzalisha bidhaa katika maeneo ya Tanzania wakati wa ukoloni.
2. Linganisha hali ya utoaji wa huduma za jamii wakati wa utawala wa Wajerumani na Waingereza katika jamii za Kitanzania.
3. Fafanua namna ambavyo sera za utawala wa Wajerumani na Waingereza zilivyokinzana na maadili ya jamii za Kitanzania.
4. Jamii za sasa za Tanzania zinaweza kujifunza nini kuhusu usimamizi wa rasilimali na utawala kutoka kwa Wajerumani na Waingereza?
5. Kwa kurejelea utoaji wa huduma za kijamii wakati wa ukoloni, pendekeza namna bora ya kuboresha utoaji wa huduma za kijamii katika Tanzania ya sasa.
6. Tofautisha utoaji wa huduma za jamii wakati wa sasa na ule wa utawala wa Wajerumani na Waingereza.

FOR ONLINE READING ONLY

Sura ya Pili

# Athari za ukoloni katika maadili ya Kitanzania

## Utangulizi

Kuingia kwa ukoloni mwishoni mwa karne ya 19 kulisababisha kuanza *kupenya kwa maadili ya kikoloni, ambayo yaliidhoofisha mifumo asilia ya* maadili ya jamii za Kitanzania. Katika sura hii, utajifunza kuhusu dhana ya maadili katika kipindi cha ukoloni na maadili ya jamii za Kitanzania wakati wa kuingia kwa ukoloni. Vilevile, utajifunza athari za mfumo wa ukoloni katika maadili ya Kitanzania na maadili ya Kitanzania yaliyodumishwa katika kipindi cha ukoloni. Umahiri utakaoujenga utakuwezesha kuishi kwa kuzingatia maadili ya Kitanzania.

**Fikiri**

Maadili ya sasa ya jamii za Kitanzania.

FOR ONLINE READING ONLY

### Dhana ya maadili wakati wa ukoloni

Dhana ya maadili wakati wa ukoloni inahusisha mifumo ya kiutawala, kisiasa, kiuchumi na kiutamaduni ambayo ililetwa na wakoloni pamoja na ile iliyokuwepo kabla ya ujio wa wakoloni katika jamii za Kitanzania. Kwa kiasi kikubwa, Waafrika waliendelea kuziishi na kuzifuata mila na desturi zao, ingawa pia waliyapokea maadili mapya kama vile imani za kiroho, mifumo ya kiutawala na tamaduni za kigeni. Kanuni za kikoloni zilisisitiza uwajibikaji wa kila mtu, umiliki binafsi wa mali na heshima kulingana na nafasi ya mtu katika jamii. Hata hivyo, kanuni hizi kwa kiasi kikubwa zilikinzana na maadili ya Kitanzania yaliyokuwapo kabla ya ujio wa wakoloni. Hii ni kwa sababu jamii nyingi ziliamini katika uwajibikaji wa pamoja, umiliki wa mali kwa pamoja na heshima kwa wote bila kujali nafasi ya mtu katika jamii. Kwa ujumla, maadili ya jamii za Kitanzania kabla ya ujio wa ukoloni katika jamii nyingi yaliongozwa na mfumo wa usawa.

Jamii za Kitanzania ziliundwa na makabila mbalimbali, kila moja likiwa na mila, desturi, maadili na miundo ya kijamii ya kipekee. Hivyo, jamii hizi zilijikuta zikikinzana na mifumo ya maadili ya kikoloni, ambayo ilikuwa na madhumuni ya kudhoofisha mila na imani za wenyeji, kama vile imani za jadi, sherehe za kimila kama ndoa na tohara na elimu ya jadi kama jando na unyago. Pia, taratibu na mienendo ya kimila kama kuishi kijamaa, uwajibikaji, heshima na uongozi wa kijadi vilidhoofishwa.

Ukoloni ulipoingia na kujiimarisha, uliingiza mifumo mipya ya kimaadili na kijamii, ambayo mara nyingi ilikinzana na mila za wenyeji. Mifumo hiyo ya kikoloni ililenga kuzidhoofisha mila na imani za kiasili, zikiwemo dini za jadi na mila na desturi zao. Mtazamo wa kikoloni ulipuuzia vipengele vya kuishi kidugu katika jamii za wenyeji na badala yake ulisisitiza ubinafsi na maadili mengine ya kikoloni ambayo yalikuwa mapya kwa jamii za Kitanzania.

**Kazi ya kufanya 2.1**

Umealikwa kuwakilisha shule yako katika semina kuhusu mada isemayo Vijana na Maadili. Andaa muhtasari utakaoutumia kuwasilisha mawazo yako kwa kutumia dondoo zifuatazo:

(a) Umuhimu wa maadili katika jamii; na

(b) Nafasi ya vijana katika kuyaenzi na kuyaendeleza maadili katika jamii.

### Maadili ya jamii za Kitanzania wakati ukoloni unaingia

Katika jamii za Kitanzania, misingi ya maadili ilijengwa juu ya umoja, ushirikiano na mshikamano miongoni mwa wanajamii. Vilevile, utunzaji wa mazingira, heshima kwa wazee na viongozi na utunzaji na ulezi wa familia na jamaa vilikuwa ni sehemu muhimu ya maadili hayo. Aidha, nidhamu, uaminifu na utii kwa mila, miiko na desturi za jamii zilikuwa nguzo kuu za maadili. Hata wakati wa ukoloni, misingi hii iliendelea kudumishwa kwa kiasi kikubwa na jamii za Kitanzania licha ya changamoto zilizokuwepo.

Ukoloni ulipoingia katika jamii za Kitanzania mwishoni mwa karne ya 19, mfumo wa maadili uliokuwepo, ambao ulilenga kujenga mshikamano wa kijamii, kuheshimu tamaduni na kuishi kwa amani na utulivu. Mfumo huu ulijikita katika mila na desturi zilizorithishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine, ukizingatia ushirikiano, utu, haki na heshima. Ingawa kulikuwa na makabila mbalimbali Tanzania, mila na desturi za makabila hayo zilifanana kwa kiasi kikubwa.

FOR ONLINE READING ONLY

## Zoezi la 2.1

1. Bainisha misingi mikuu ya maadili ya jamii za Kitanzania wakati ukoloni unaingia.
2. Eleza umuhimu wa kujifunza maadili ya jamii za Kitanzania ya wakati uliopita.
3. Linganisha mfumo wa maadili wa jamii za Kitanzania kabla na baada ya ukoloni.

Hali ya maadili ya jamii za Kitanzania wakati ukoloni unaingia imejipambanua katika nyanja mbalimbali ikijumuisha vipengele mbalimbali.

**Mila na desturi**: Wakati wa kuingia kwa ukoloni, jamii za Kitanzania zilikuwa na mifumo thabiti ya maadili iliyoongozwa na kanuni, miiko, mila na desturi zao. Maadili kama vile uvumilivu, ukarimu, heshima kwa wazee na mamlaka, uadilifu, kujitolea, usawa na uwajibikaji yalikuwa sehemu muhimu ya maisha ya kila siku. Kila jamii ilikuwa na taratibu zake za kimaadili ambazo zilisimamiwa na viongozi wa jadi pamoja na wazee wa ukoo.

Vilevile, jamii za Kitanzania zilikuwa na utajiri mkubwa wa mila, desturi, kanuni, miiko na utaratibu uliorithishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Kwa mfano, kundi la wazee wa ukoo liliheshimiwa sana na lilitegemewa katika kufanya uamuzi, ushauri, kupitisha ujuzi wa kitamaduni na kudumisha umoja wa familia. Wazee walikuwa na wajibu wa kurithisha mila na desturi kwa kizazi kijacho. Walitumia njia mbalimbali kama vile masimulizi, nyimbo, ushairi, uelimishaji, malezi, ngoma na mbinu nyingine zilizolenga kuyalinda na kuyakuza maadili ya jamii iliyohusika.

Pia, jamii zilijikita katika maisha ya jumuiya na uwajibikaji wa pamoja, ambapo imani ilikuwa ni suala la jamii nzima na si la mtu mmoja mmoja. Ustawi wa jamii haukuangalia masilahi ya mtu binafsi, bali uliangazia maadili ya kijamii kama vile ushirikiano na msaada wa pande zote, ambayo yalikuwa msingi wa maisha ya jamii. Shughuli za uzalishaji mali kama kilimo, uvuvi, uwindaji na uchungaji wa mifugo zilifanywa kwa pamoja katika jamii nyingi. Aidha, kulikuwa na mgawanyo wa majukumu kati ya wanaume na wanawake, ambapo wanaume walikuwa na jukumu la kutunza familia na wanawake walishiriki katika malezi ya watoto, kazi za nyumbani na wakati mwingine kilimo au shughuli nyingine za kiuchumi. Malezi ya watoto yalikuwa ni jukumu la jamii nzima.

Maadili haya yaliimarishwa kupitia matambiko, sherehe na shughuli za kila siku. Vilevile, maadili yalisisitiza umuhimu wa kudumisha maelewano, ushirikiano na mshikamano wa kijamii. Hii iliwawezesha Watanzania kuendeleza mila na desturi zao kwa njia za vitendo na kujijenga kwenye misingi ya maisha yao.

FOR ONLINE READING ONLY

Kadhalika, uvumilivu ulikuwa msingi muhimu wa maadili ya jamii za Kitanzania. Watu walifundishwa umuhimu wa kuvumiliana na kuheshimu tofauti za watu wengine, iwe ni za kikabila, kidini au kiutamaduni. Hivyo, mila na desturi zilikuwa na nafasi kubwa katika kuyaunda maadili ya jamii. Sherehe za kijamii kama vile harusi, jando na unyago, imani za kidini na mila zilitumika kama fursa za kujenga mshikamano wa kijamii na kufundisha maadili kwa vizazi vipya.

**Dini za jadi:** Wakati ukoloni ulipoingia, dini za jadi zilikuwa na nafasi muhimu katika kuunda maadili ya jamii. Watu waliamini katika nguvu za asili, mizimu na miungu. Imani hizi ziliathiri na kukuza imani za watu na jinsi watu walivyoheshimu mazingira, walivyotekeleza shughuli za kilimo na walivyoishi kwa maelewano. Maadili ya dini za jadi yalisisitiza ushirikiano, upendo, heshima, umoja kwa wanajamii, pamoja na kudumisha, kukuza na kufuata mila na desturi zilizorithiwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Dini za jadi pia zilitumika kama njia mojawapo ya kusimamia maadili katika jamii. Kwa mfano, waliokaidi miiko, maagizo na taratibu za jamii waliadhibiwa kwa njia mbalimbali kama vile mizimu na wazee kwa utovu wa nidhamu. Vilevile, matatizo mbalimbali katika jamii yalitatuliwa kwa njia za kiimani kupitia matambiko na mbinu nyingine zilizohusiana na dini za jadi.

**Utawala wa jadi:** Wakati ukoloni ulipoingia, jamii za Kitanzania zilikuwa zikiongozwa na mifumo ya jadi iliyotofautiana baina ya kabila moja na lingine. Mifumo hii mara nyingi ilijikita katika kufanya uamuzi kijamii, ambapo majukumu ya uongozi yalitekelezwa na machifu, wazee, au mabaraza ya wazee. Uamuzi wa viongozi hawa uliheshimiwa na wanajamii wote kutokana na hekima na uwezo wao wa kudumisha maelewano ndani ya jamii. Uongozi huo ulifanya uamuzi kwa faida ya jamii nzima na si kwa masilahi ya watu wachache. Dhana ya utawala ilikuwa imefungamana kwa karibu na utamaduni na maadili ya jamii, ikisisitiza uwajibikaji wa pamoja, heshima na utii kwa mamlaka, uzalendo na ustawi wa jamii nzima.Vilevile, kila jamii ilikuwa na mfumo wake wa utawala wa kijadi, unaoongozwa na machifu, wazee wa ukoo, au viongozi wa kimila. Kwa mfano, katika jamii za Kitanzania kulikuwa na mifumo thabiti iliyojengeka na kuwa na nguvu kubwa kama vile Nyarubanja, Ubugabire na Umwinyi. Mifumo hii ya kiutawala ilijitokeza katika jamii kama Wahaya, Waha na jamii za pwani mtawalia. Mifumo hii ilifungamanishwa mno na nguvu ya kiuchumi hasa umiliki wa ardhi na ng'ombe. Pamoja na mambo mengine, viongozi katika jamii hizi waliheshimiwa sana na walikuwa na jukumu la kuhakikisha haki, usalama na mshikamano wa jamii iliyohusika.

Katika jamii ya Wanyamwezi mathalani kulikuwa na wasaidizi wa Mtemi walioitwa *Wanyampala*. Mmoja wa wasaidizi wake aliitwa *Mgawe* aliyekuwa kiongozi wa matambiko, *Mtwale* alikuwa kiongozi wa jeshi lililohakikisha usalama wa Utemi

FOR ONLINE READING ONLY

dhidi ya maadui wa ndani na nje. *Mteko* alikuwa kiongozi msaidizi wa jeshi. Pia, alikuwa mkuu wa huduma za siri na ujasusi. *Kikoma* alikuwa mkuu wa habari na *Minule* alikuwa mkuu wa kukusanya kodi katika misafara iliyopita katika eneo la Unyanyembe.

Sheria na kanuni za kijadi ziliweka maadili na miongozo kuhusu ushirikiano, haki na nidhamu. Familia zilikuwa ndio msingi wa jamii na watu walihusishwa na familia zao pana, ikijumuisha koo au ukoo. Mfumo wa ukoo ulikuwa na umuhimu mkubwa, ambapo jamii nyingi zilikuwa na mifumo ya kikabila na kiukoo iliyosimamia na kuratibu masuala muhimu kama ndoa, rasilimali, urithi, jando na unyago, pamoja na tiba za asili. Vilevile, mfumo wa miiko ulisimamia matendo mema kama vile heshima, ukarimu, upendo, uadilifu na uzalendo.

Pia, sheria za kijadi zilisimamia mienendo ya watu na zilitekelezwa na wazee wa kimila. Sheria hizi zilitungwa kwa misingi ya haki, usawa na kulinda masilahi ya jamii nzima. Adhabu kwa kuvunja sheria na miiko ya kijadi zilikuwa kali, lakini zililenga zaidi kurekebisha, kurudisha na kudumisha amani ndani ya jamii.

**Lugha na mawasiliano:** Jamii za Kitanzania zilikuwa na aina nyingi za lugha za asili, ambazo kwa kiasi kikubwa zilitokana na makabila ya jamii iliyohusika. Mathalani, lugha za asili zilikuwa sehemu muhimu ya utambulisho wa jamii moja na nyingine na zilitumika kuwasilisha maarifa, maadili na utamaduni kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Kwa mfano, methali, hadithi na nyimbo za jadi zilikuwa na jukumu kubwa katika kufundisha maadili ya kijamii na kurithisha maarifa na historia. Pia, mawasiliano ndani ya jamii yalifungamana sana na mila na desturi. Kwa mfano, jamii ya Wachagga, walioishi kandokando na kwenye miteremko ya Mlima Kilimanjaro, walizungumza lugha ya Kichagga, ambayo ilitumika katika mawasiliano ya kila siku, matambiko na desturi za kitamaduni, hivyo kubeba jukumu muhimu katika kudumisha umoja na mshikamano katika jamii nzima.

Lugha katika jamii nyingi za Kitanzania ilikuwa na uhusiano wa karibu na mtindo wa maisha yao pamoja na shughuli za uzalishaji mali kama vile kilimo na ufugaji. Lugha ilitumika kama chombo cha kuhamasisha watu kushiriki katika shughuli mbalimbali za uzalishaji mali. Kulikuwa na aina mbalimbali za ngoma kulingana na jamii iliyohusika; kwa mfano, Wasukuma walikuwa na ngoma ya *Bugobogobo*, Wanyasa walikuwa na ngoma ya *Mganda*, Wamakonde walikuwa na ngoma ya *Sindimba* na Wazaramo pamoja na Waluguru walikuwa na ngoma ya *Mdundiko*. Ngoma hizi zilichezwa katika matukio muhimu ya kijamii kama vile harusi, msimu wa mavuno, au kuashiria kuanza kwa msimu wa kilimo. Muhimu zaidi, ngoma hizi zilikuwa ni zao la lugha na zilitumika pia kama njia ya mawasiliano. Kupitia ngoma

FOR ONLINE READING ONLY

hizo, wanajamii waliweza kujenga uzalendo, ujasiri, upendo, fahari na mshikamano wa kijamii.

**Simulizi na hadithi:** Simulizi na hadithi zilikuwa nguzo muhimu za mawasiliano katika jamii za Kitanzania. Kila jamii ilikuwa na aina zake za masimulizi yaliyoakisi tamaduni zao. Baadhi ya masimulizi hayo ni kama vile hekaya, methali, vitendawili na hadithi, ambazo zilitumika kufundisha, kuendeleza na kurithisha maadili ya kitamaduni kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Kwa mfano, hadithi zilikuwa na masimulizi ya matukio mbalimbali ya kijamii yaliyotokea katika vipindi vya nyuma ndani ya jamii husika. Hivyo, hadithi hizi ziliwafundisha, ziliwaburudisha na kuwaonya na kwa njia hiyo ziliweza kusaidia katika ujenzi wa maadili ndani ya jamii. Mathalani, jamii ya Wahehe ilitumia ushairi kama njia ya kuwasilisha ujumbe, kuwaelimisha vijana na kuwaburudisha. Simulizi hizi zilikuwa muhimu sana katika kuudumisha utambulisho wa kitamaduni na maadili ya kijamii. Wazee wa jamii walikuwa wahusika wakuu katika utoaji wa simulizi na hadithi hizi.

**Kazi ya kufanya 2.2**

Tafuta taarifa kutoka vyanzo mbalimbali ikiwemo mitandao kuhusu lugha ya kabila mojawapo la Tanzania. Kisha, bainisha misemo au methali au vitendawili vya makabila hayo ambavyo vinalenga kudumisha maadili ya Kitanzania.

**Mavazi:** Wakati wa kuingia kwa ukoloni, jamii za Kitanzania zilikuwa na mavazi ya asili yaliyotengenezwa kwa kutumia malighafi za kiasili kama vile ngozi za wanyama, majani na magome ya miti. Vilevile, walivaa mapambo kama hereni na bangili. Mavazi haya yalikuwa sehemu ya utambulisho na yaliheshimu utamaduni wa kabila au jamii iliyohusika. Vitu hivyo vilikuwa zaidi ya mavazi kwani viliashiria umuhimu wa utamaduni uliowakilisha, hadhi, umri na hali ya ndoa ndani ya jamii.

Vilevile, jamii za Wachaga wanaoishi kwenye miteremko ya Mlima Kilimanjaro walikuwa wakivaa mavazi yaliyotengenezwa kwa ngozi ya wanyama au vitambaa vilivyofumwa kienyeji. Mavazi haya mara nyingi yalikuwa rahisi na yalifaa kwa hali ya hewa ya mlima. Hata hivyo, baada ya kuwasili kwa ukoloni, mavazi ya mtindo wa Kimagharibi yalianza kuathiri mavazi yao, hasa miongoni mwa vijana na wale waliojihusisha na biashara au shughuli za kimisionari. Hii ilikuwa ni sehemu ya harakati za wazungu kutafuta masoko kwa bidhaa za viwanda vyao vya Ulaya.

FOR ONLINE READING ONLY

Halikadhalika, miongoni mwa jamii ya Wasukuma, mavazi ya kitamaduni yalitengenezwa kwa ngozi ya wanyama na nyuzi za mimea kabla ya kuanzishwa kwa nguo za kufuma. Wanawake pia walivaa sketi za nyasi zilizotengenezwa kwa nyuzi za mimea. Mavazi haya yalikuwa rahisi lakini yalilingana na mazingira na hali ya hewa ya Usukumani. Aidha, nguo hizo ziliakisi shughuli za kilimo na ufugaji ya jamii ya Wasukuma. Mavazi pia yaliendana na mitindo ya urembo mathalani mitindo ya kusuka nywele kwa wanawake na kunyoa nywele kwa wanaume kwa mfano kwa jamii ya Wanyamwezi kama inavyoonekana katika Kielelezo 2.2. Kwa ushawishi wa kikoloni, nguo za pamba zikawa za kawaida zaidi na mavazi ya jadi kama vile kaniki yalianza kuhifadhiwa kwa matukio maalumu. Kielelezo 2.1 kinaonesha vazi la asili la kaniki la jamii ya Wasukuma.



**Kielelezo 2.1:** *Vazi la asili katika jamii ya Wasukuma*



**Kielelezo 2.2**: *Mitindo ya nywele katika jamii ya Wanyamwezi*

Jamii za Wanyamwezi, Wasukuma, Wahehe, Wachaga, Wahaya na Wasambaa zilikuwa na utofauti wa mavazi kati ya wananchi na watawala wao. Kulikuwa na nguo maalumu zilizovaliwa na watawala ili kuonesha mamlaka yao. Mavazi hayo ni pamoja na nguo za ngozi za wanyama hasa simba na chui, kofia, regalia, taji, mapambo na mkoba. Mavazi haya yaliandamana na vifaa kama usinga, ngao na mkuki kama alama za nguvu, mamlaka na utawala wa eneo la kiongozi. Pia, kulikuwa na nguo maalumu zilizovaliwa na wazee walioongoza kufanya matambiko ya kijamii. Nguo hizi zilikuwa na rangi maalumu. Nguo nyeupe na nyeusi ndio ziliruhusiwa kwa ajili ya matambiko. Nguo nyekundu hazikuruhusiwa kutumika katika matambiko.

Mavazi na mitindo ya kikoloni iliingia na kuenea katika jamii za Kitanzania. Wamisionari, maofisa wa kikoloni na wafanyabiashara walileta aina mpya za nguo kama vile suruali, mashati, gauni na suti. Vilevile, katika maeneo ya pwani na vituo vya kibiashara kama Ujiji na Tabora, ambako biashara zilifanyika kati ya jamii za Kitanzania na Waarabu, mavazi kama kanzu, baibui, makubadhi na vikoi yalikuwa

FOR ONLINE READING ONLY

maarufu. Hata hivyo, mavazi ya kitamaduni yaliendelea kutumika, hasa katika maeneo ya vijijini na miongoni mwa wale waliopinga ushawishi wa wakoloni na tamaduni za Ulaya Magharibi.

Aidha, maadili ya Kitanzania wakati wa kuingia kwa ukoloni yalikuwa na nguvu kubwa katika maisha ya watu na yalidumishwa kwa umakini na viongozi wa jadi pamoja na wazee wa mila. Kanuni hizi za kimaadili zilifanya kazi kama misingi imara iliyojenga jamii. Jamii pia ilionesha uwajibikaji mkubwa katika kutekeleza wajibu wao kwa familia na jamii kwa ujumla. Maadili haya yaliziwezesha jamii za Kitanzania kujiendeleza na kusaidia kuunda jamii zenye utulivu, mshikamano na maendeleo endelevu.

**Kazi ya kufanya 2.3**

Tafuta taarifa kutoka vyanzo mbalimbali ikiwemo mtandao na eleza jinsi mavazi yanaweza kutumika katika kudumisha maadili ya Kitanzania.

**Zoezi la 2.2**

1. Ainisha maadili yanayopaswa kudumishwa katika jamii yako.
2. Pendekeza mikakati ya kudumisha maadili katika jamii yako.
3. Eleza jinsi teknolojia inavyoathiri maadili katika jamii unayoishi.
4. Ni kwa namna gani hadithi na masimulizi yanaweza kutumika katika kujenga uzalendo katika mazingira ya sasa.
5. Eleza umuhimu wa lugha za asili katika kudumisha maadili katika mazingira ya sasa.

FOR ONLINE READING ONLY

## Athari za mfumo wa ukoloni katika maadili ya Kitanzania

Kuingia kwa mfumo wa kikoloni katika jamii za Kitanzania kuliathiri mifumo ya maadili ya kijamii, kiutamaduni, kisiasa na kiuchumi. Athari hizi zinaelezwa kwa upana katika sehemu zinazofuata.

### Athari za kijamii

*Elimu:* Kabla ya ukoloni, elimu katika jamii za Kitanzania ilitolewa kulingana na mazingira yao na ilijikita katika mila na desturi. Kulikuwa na mfumo rasmi wa

utoaji elimu katika kila jamii, ambapo elimu hiyo ilitolewa wakati wote na kwa vitendo. Mafunzo ya jando na unyago yaliandaliwa kwa madhumuni ya kuwaandaa vijana kwa maisha ya utu uzima na kuchukua majukumu ya kijamii. Mafunzo haya yalitolewa kwa njia mbalimbali kama vile kilimo, ufugaji, uwindaji, mapishi, ujenzi na uvuvi. Vilevile, elimu ilitolewa kupitia hadithi, methali na uzoefu wa vitendo. Hii iliwawezesha wanajamii, hususani watoto na vijana, kupata maarifa stahiki na ujuzi muhimu.

Mamlaka za kikoloni zilianzisha mifumo rasmi ya elimu iliyofuata mfumo wa elimu na maadili ya kimagharibi ya Ulaya. Shule za wamisionari zilifundisha masomo yanayohusu maadili ya kwao, huku mara nyingi zikikataa na kupinga mila, tamaduni na desturi za Kitanzania kuendelea kutumika miongoni mwa wanajamii. Kwa mfano, wanafunzi mara nyingi waliadhibiwa kwa kuzungumza lugha zao za asili shuleni na walisisitizwa kujifunza na kufuata desturi na maadili ya kimagharibi yaliyohifadhiwa na wazungu kupitia mfumo wa ukoloni.

Hali kadhalika, mfumo wa elimu ya kikoloni ulisababisha mabadiliko makubwa ya kiutamaduni. Watanzania wengi waliosoma shule hizi walifuata njia za kufikiri, kuvaa na kuenenda Kizungu, ambazo zilipingana na mila, desturi na maadili ya Kitanzania. Watumishi wa serikali ya kikoloni walilazimika kuvaa mavazi maalumu kama sare kwa mfano maaskari na manesi. Watumishi wengine walivaa mavazi yaliyoelekezwa na idara zilizohusika kama ya elimu, mahakama na wahudumu wa ofisi. Hali hii ilijenga matabaka kati ya wasomi walioelimika, ambao walikuwa wameshikamana zaidi na maadili ya kikoloni na wale ambao hawakupata elimu ya kikoloni na waliodumisha njia za maisha za jadi. Kuwagawa Watanzania lilikuwa moja ya malengo makuu ya wakoloni katika sera yao ya "wagawe ili uwatawale". Hivyo, hali hii ilichangia mmomonyoko wa kimaadili na kiutamaduni na hivyo kusababisha kuenea na kukua kwa kanuni za kiutamaduni za kimagharibi na hivyo kudunisha maadili ya Kitanzania.

*Afya:* Kabla ya ujio wa wakoloni, jamii za Kitanzania zilikuwa na mifumo mbalimbali ya utoaji huduma za afya, kulingana na tamaduni na mila za jamii iliyohusika. Ingawa hakukuwa na hospitali au vituo vya afya kama vilivyo sasa, hii haimaanishi kuwa huduma za afya hazikuwepo. Kulikuwa na matumizi ya dawa za asili zilizotokana na mimea na vifaa vingine kama vile mafuta au maji, ambazo zilitumika kutibu magonjwa mbalimbali. Dawa hizi zilipatikana kwa urahisi katika mazingira yao. Kulikuwa na wataalamu waliobobea katika masuala ya afya kama vile waganga wa mitishamba, wakunga na ngariba waliokuwa na jukumu la kutibu na kuzuia

FOR ONLINE READING ONLY

magonjwa. Vilevile, huduma za afya za jadi zilihusishwa na imani za jadi, ambapo matambiko yalifanyika kutibu baadhi ya magonjwa.

Ujio wa wakoloni ulileta mabadiliko makubwa katika mfumo wa afya, kwani walianzisha hospitali na vituo vya afya katika maeneo mbalimbali nchini kwa kutumia mtindo na mfumo wa Ulaya magharibi. Walileta pia dawa mbalimbali za kutibu magonjwa ambazo zilikuwa tofauti na zile za asili zilizotumika kabla ya ukoloni. Aidha, wakoloni walibeza na kudunisha mfumo wa tiba za asili kwa kutumia mbinu mbalimbali kama vile dini, kugawa dawa za kimagharibi kwa jamii za Kitanzania na kueneza propaganda kuwa tiba za asili hazina msaada wowote, ni uchawi na ushirikina na ni alama ya umasikini na ukosefu wa maendeleo. Zaidi ya hayo, serikali ya kikoloni ilizuia na kuwakamata wataalamu wa tiba za asili, hatua ambayo iliathiri kwa kiasi kikubwa imani na maadili ya mfumo wa afya wa jadi. Ukweli unabaki kuwa dawa za Ulaya magharibi pia zilitokana na mimea na wanyama kama za Waafrika ila wazungu walizichakata viwandani, kuzifungasha katika vifungashio na waliziwekea vipimo maalumu ili kutibu ugonjwa unaohusika.

**Athari za kiutamaduni**

Ujio wa wakoloni ulileta athari mbalimbali za kiutamaduni kwa jamii za Kitanzania kama inavyoelezewa hapa chini.

*Dini za jadi:* Kabla ya kuja kwa dini za kigeni kama Ukristo na Uislamu, jamii za Kitanzania zilikuwa na imani za kiasili zilizokita mizizi katika utamaduni wa jamii iliyohusika. Dini hizi mara nyingi zilihusisha ibada za kuabudu Mungu kupitia miungu, mababu na mizimu katika maeneo mbalimbali kama vile mapango, mito, mabwawa, milima, majabali makubwa na miti mikubwa. Imani za dini za jadi zilijikita katika kulinda na kudumusha maadili mema ya jamii.

Ujio wa ukoloni nchini uliathiri na kuleta mifumo mipya ya imani na dini, ambayo iliendana na utamaduni wa Ulaya Magharibi. Kwa mfano, wamisionari wa Kikristo walileta mafundisho mapya yenye mila, desturi na maadili mapya, huku wakilenga kubadilisha imani za jamii za Kitanzania. Aidha, dini za jadi za Kitanzania zilidharauliwa na kupigwa vita na wakoloni kama sehemu ya juhudi zao za kueneza mila na desturi za nchi za Ulaya Magharibi. Hii ilisababisha jamii nyingi za Kitanzania kuukubali mfumo wa dini za Kikristo na hivyo kuwa na maadili ya Ulaya Magharibi au maadili mseto. Maadili ya asili yalishambuliwa kuwa si bora, yaliwakandamiza, kuwabagua na kuwadunisha wanawake. Hivyo maadili ya asili yalipata mtikisiko mkubwa kutoka kwenye imani hii mpya ya Kikristo.

Kwa ujumla, imani za asili zilichukua sura mpya, zikichanganywa na mafundisho ya Kikristo na utamaduni wa wakoloni. Matokeo yake, dini ya Kikristo ilipata msukumo

FOR ONLINE READING ONLY

mkubwa ikienea maeneo mengi nchini na idadi ya waumini ikaongezeka. Waumini wapya walionekana kujitolea kwa imani yao, wakichukua nafasi za uongozi katika jamii na kusaidia kuendeleza mafundisho mapya.

Mbali na Watanzania wengi kuingia kwenye dini ya Kikristo, mabadiliko ya dini yalisababisha pia mabadiliko katika maadili na taratibu za Kitanzania, kama vile masuala ya ndoa, tohara, mavazi, vyakula na muziki. Desturi na mila za Kitanzania zilipuuzwa na badala yake, desturi na mila za kigeni zikapewa umuhimu mkubwa. Hii ilisababisha mkanganyiko katika kulea watoto kati ya utamaduni wa Kitanzania na mafundisho ya Kikristo.

Muingiliano na uhusiano wa dini na ukoloni pia ulisababisha mgawanyiko katika jamii ya Kitanzania. Baadhi ya watu waliokubaliana na utamaduni wa kikoloni walionekana kama wasaliti wa imani na maadili ya Kitanzania. Vilevile, kulikuwa na wale waliopinga mabadiliko haya ya kikoloni, wakidai kwamba utamaduni na hasa imani za asili, zinahitaji kulindwa na kuheshimiwa. Hivyo, kukandamizwa kwa dini za jadi kulichangia kuzizorotesha, kwani vizazi vipya vilihimizwa kufuata Ukristo au Uislamu. Hii ilisababisha upotevu wa maarifa na desturi za kiutamaduni ambazo kwa muda mrefu zilikuwa muhimu kwa mfumo wa kijamii wa jamii za Kitanzania.

**Zoezi la 2.3**

1. Bainisha athari zingine zilizoletwa na Ukristo nchini Tanzania.
2. Linganisha mfumo wa elimu ya jadi na mfumo wa elimu ya sasa.
3. Eleza mchango wa dini za jadi katika kulinda na kudumisha maadili ya Kitanzania.
4. Fafanua umuhimu wa tiba za asili katika mazingira ya sasa ya Kitanzania.

*Lugha:* Kabla ya ukoloni, jamii za Kitanzania zilizungumza lugha za kiasili kama vile Kimasai, Kisukuma, Kichaga, Kizigua, Kizaramo, Kidigo, Kimwera, Kitumbatu na nyinginezo nyingi. Lugha hizi hazikuwa tu njia za mawasiliano, bali pia zilibeba utamaduni, utambulisho, mila, desturi, miiko na kumbukumbu katika jamii iliyohusika. Hata hivyo, mifumo ya elimu ya kikoloni ilileta mabadiliko makubwa kwenye lugha za asili. Lugha kama Kiingereza kilianza kutumika kama lugha ya kufundishia shuleni, hali iliyosababisha kupungua kwa matumizi ya lugha za asili. Moja ya athari kubwa ilikuwa ni kushinikiza matumizi ya lugha za kikoloni hivyo kusababisha kupungua kwa matumizi ya lugha za asili. Jamii zilianza kuwaona wasomi wanaozungumza Kiingereza kama kipimo cha usomi na ustaarabu. Watu wasiojua kuandika na kuzungumza Kiingereza walionekana kuwa si wasomi na wastaarabu. Usomi na

FOR ONLINE READING ONLY

ustaarabu ulianza kupimwa kwa kujua lugha za kigeni na utamaduni wa kikoloni kama lugha, mavazi, aina ya vyakula na kazi za ofisini na utawala.

Aidha, ukoloni ulisababisha kutengenezwa kwa vitabu na nyaraka nyingi kwa lugha za kikoloni badala ya lugha za asili, hivyo kusababisha upungufu wa vyanzo vya maarifa kwa lugha za asili za Tanzania. Hii ilisababisha watoto kujifunza masomo yao yote kwa lugha za kigeni na hivyo kupoteza uwezo wao wa kujieleza vizuri kwa lugha zao za asili. Kama inavyoaminika na wataalamu wengi wa elimu, hali hii iliwafanya wanafunzi wapoteze uwezo wao wa ubunifu, kuelewa na kujiamini, kwa sababu lugha waliyoitumia haikuwa ya asili yao. Hata hivyo, kwa Tanzania, ukoloni ulitumia lugha ya Kiswahili kwa shughuli za Waafrika kama kutoa maelekezo na kendesha kesi katika mahakama za wenyeji zilizosimamiwa na machifu.

Zaidi ya hayo, mifumo ya elimu ya kikoloni ilisababisha kuibuka kwa msamiati wa kigeni. Kwa mfano, maneno mengi ya Kiingereza na Kijerumani yalipokelewa, kutoholewa na kutumika katika Kiswahili. Mfano wa maneno haya ni "shule" kutoka "*schule*," "nanasi" kutoka "*ananas*," na "hela" kutoka "*heller*" yalitoka katika lugha ya Kijerumani. Pia, maneno kama "polisi" kutoka "*police*," "benki" kutoka "*bank*," "baiskeli" kutoka "*bicycle*," na "hospitali" kutoka "*hospital*" yalitoka katika lugha ya Kiingereza. Vilevile, athari za lugha za kikoloni zimejidhihirisha kupitia maneno, misemo na mabadiliko ya sarufi. Mabadiliko haya yanaonesha jinsi ukoloni ulivyoweza kubadilisha matumizi ya lugha za Kitanzania na kuathiri utamaduni na mawasiliano ya kila siku.

Katika kipindi cha 1890-1961, Kiswahili kiliathiriwa sana na kuingiliana na lugha za kikoloni. Ushawishi wa kikoloni, kama vile Wajerumani, ambao walikuwa wakoloni wa kwanza nchini ulijidhihirisha kupitia matumizi ya lugha ya Kijerumani kwenye baadhi ya masuala ya utawala na kidogo sana kwenye elimu. Baadaye, Waingereza walipochukua mamlaka baada ya Vita Kuu ya Kwanza ya Dunia, Kiingereza kilitumika kama lugha ya kufundishia shuleni na lugha rasmi ya serikali.

**Kazi ya kufanya 2.4**

Andika insha isiyopungua maneno 200 ukionesha:

(a) Umuhimu wa kuhifadhi na kuendeleza lugha za asili kwa jamii za Kitanzania; na

(b) Mikakati ya kuhifadhi na kuendeleza lugha za asili kwa kizazi cha sasa na kijacho.

FOR ONLINE READING ONLY

*Mavazi:* Baada ya ujio wa ukoloni, kulianza kujitokeza mabadiliko ya taratibu katika mitindo ya mavazi. Mavazi ya Kimagharibi kama vile suti, tai, magauni, kaptula, suruali na mengineyo, yalianza kuingizwa na kukubalika, hasa miongoni mwa walioelimika au wale waliokuwa na ushawishi katika utawala wa kikoloni. Hii ilisababisha kudunishwa au kupuuzwa kwa mavazi na maadili ya kijadi ya mavazi. Mabadiliko haya mara nyingi yalisababisha kuachwa kwa mavazi ya kiutamaduni, kwani mitindo ya Kimagharibi ilihusishwa na usasa, maendeleo, ustaarabu, nguvu za utawala na heshima. Pia, maadili na tabia za jamii zilianza kubadilika kutokana na ushawishi wa utamaduni wa kigeni wa mavazi.

Vilevile, katika maeneo ya pwani, hasa miongoni mwa jamii za Waswahili, mavazi yaliathiriwa sana na utamaduni wa Kiarabu kutokana na karne nyingi za biashara na mwingiliano. Kwa kawaida, wanaume wa Kiarabu huvaa "kanzu," vazi refu ambalo mara nyingi huwa na rangi nyeupe, huku wanawake wakivaa "baibui" vazi jeusi linalofunika mwili mzima. Mavazi ya Waswahili kwa kiasi kikubwa yaliakisi utamaduni wa Kiarabu. Vielelezo 2.3 na 2.4 vinaonesha baadhi ya mavazi yaliyoletwa na wageni.



**Kielelezo 2.3:** *Vazi la baibui*



**Kielelezo 2.4:** *Vazi la suti na kanzu*

FOR ONLINE READING ONLY

## Zoezi la 2.4

1. Fafanua athari zilizosababishwa na mwingiliano kati ya wageni katika mitindo ya mavazi ya asili.
2. Eleza faida na changamoto za maendeleo ya kisayansi na kiteknolojia katika kuyadumisha mavazi ya asili.
3. Umejifunza nini kutokana na athari za ukoloni katika mavazi ya Kitanzania?

*Mfumo wa utawala na sheria:* Baada ya ujio wa utawala wa kikoloni, mifumo ya jadi ilibadilishwa na kuwekwa chini ya mamlaka ya kikoloni. Mabadiliko haya ya kiutawala yalileta maadili mapya kama vile utii kwa mamlaka ya kikoloni, muda wa kazi na kufuata sheria za kikoloni, ambazo mara nyingi zilikinzana na kanuni zilizowekwa za jamii za wenyeji. Msisitizo wa mamlaka ya mtu binafsi na udhibiti wa dola ya kikoloni ulivuruga utawala wa kijumuiya na wa maridhiano, ambao ulikuwa msingi wa jamii za Kitanzania.

Kwa mfano, jamii za Kitanzania zilikuwa na sheria zao za kimila ambazo zilikuwa na mizizi katika mila, desturi na imani zao za kimaadili. Sheria hizi zilisimamia nyanja mbalimbali za maisha, zikiwemo ndoa, mali, mirathi, utatuzi wa migogoro na tabia za kijamii. Sheria hizi zilinyumbulika na kuendana na mahitaji na maadili ya jamii, zikiwa na lengo la kurejesha maelewano na kudumisha uhusiano mzuri ndani ya jamii.

Hivyo basi, kuanzishwa kwa mifumo ya kisheria ya kikoloni kulileta mabadiliko makubwa ambayo mara nyingi yalikuwa magumu kutekelezwa na jamii. Sheria hizi zilitekelezwa na mahakama za kikoloni ambazo hazikuzingatia mila, desturi na taratibu za haki za jadi. Matokeo yake, sheria za kimila na desturi za jamii za Kitanzania ziliwekwa pembeni na hivyo kuvuruga mfumo wa maadili ya kijamii na kijadi kwa kuvunja mamlaka za viongozi wa jadi kama vile machifu na wazee wa kimila. Sheria hizi ni pamoja na mikataba rasmi, haki za umiliki wa ardhi na haki ya kuadhibu, ambazo mara nyingi zilikinzana na kanuni na sheria za kimila.

*Mifumo ya familia na jamii:* Miundo ya kitamaduni ya familia katika jamii za Kitanzania ilijumuisha familia pana, zenye uhusiano wa kindugu na majukumu yaliyo wazi kwa kila mwanafamilia. Hata hivyo, kuja kwa ukoloni kuliathiri kwa kiasi kikubwa maadili na miundo ya familia na jamii hizo. Kwa mfano, uchumi wa kikoloni ulianzisha aina mpya za ajira kama vile kazi za ujira kwenye mashamba makubwa na migodi, ambazo mara nyingi zilihitaji wanaume kuhama kutoka maeneo ya vijijini kwenda mijini au maeneo ya kazi za mbali. Uhamaji huu ulivuruga majukumu ya kiutamaduni ya familia na hivyo wanawake walilazimika kubeba majukumu ya ziada katika kaya na jamii.

FOR ONLINE READING ONLY

Aidha, uhamaji wa wanaume kwenda kufanya kazi mbali ulisababisha kuenea kwa tabia mpya za mahusiano kati ya wanaume hao na wanawake wa mijini au mashambani walikokuwa wakifanya kazi. Hali hii ilisababisha baadhi ya wanaume kupoteza uaminifu na hivyo kusababisha kuenea kwa maradhi ya zinaa na kuvunjika kwa ndoa.

Vilevile, ukoloni ulipandikiza maadili mapya ambayo mara nyingi yalikinzana na kanuni za asili za jamii. Kwa mfano, uchumi wa kikoloni ulikuza ubinafsi na ushindani, ambapo watu walihimizwa kutafuta faida za kibinafsi kupitia kazi za ujira, uzalishaji wa mazao ya biashara na biashara kwa ujumla. Mabadiliko haya yalijenga ubinafsi ambao ulidhoofisha uhusiano na ushirikiano wa kindugu na kijamii uliokuwa ukiunganisha jamii za Kitanzania. Pia, wakoloni walileta maadili mapya kuhusu familia, ndoa na uhusiano wa kijamii. Kwa mfano, ndoa za Kikristo na Kiislamu zilianza kuchukua nafasi ya ndoa za kitamaduni na hivyo kubadilisha maadili ya kijamii yanayohusu familia na majukumu ya kijinsia.

FOR ONLINE READING ONLY

### Athari za kiuchumi

Kuja kwa wakoloni kuliathiri taratibu mbalimbali za uzalishaji mali katika jamii. Kabla ya ukoloni, shughuli za kiuchumi kama vile kilimo, biashara, uvuvi na ufugaji zilifanyika kwa mujibu wa mila na desturi za Kitanzania na kulingana na mahitaji ya jamii iliyohusika. Shughuli hizi zilifanywa kwa pamoja chini ya mamlaka za jadi. Hata hivyo, kuingia kwa wakoloni kulibadilisha mfumo mzima wa uzalishaji na umiliki wa mali. Watu walianza kunyang'anywa mali zao kama vile ardhi, ambayo ilichukuliwa na walowezi wa kikoloni pamoja na serikali yao.

Zaidi ya hayo, uchumi wa kikoloni uliweka msisitizo kwenye uzalishaji wa mazao ya biashara kama vile pamba, kahawa, chai na karafuu, ili kuzalisha malighafi kwa ajili ya viwanda huko Ulaya magharibi. Wakoloni pia walileta uchumi unaoendeshwa kwa fedha, umiliki binafsi wa mali, pamoja na teknolojia mpya iliyotumika katika uzalishaji mali. Mabadiliko haya yalisababisha kuibuka kwa matabaka katika jamii, kuongezeka kwa umaskini, migogoro na hatimaye kumomonyoka kwa maadili.

Umoja na mshikamano uliokuwepo kabla ya ukoloni ulitoweka. Hivyo, mfumo mpya ulioletwa na wakoloni ulijenga jamii tegemezi na yenye mashindano badala ya umoja na ushirikiano kama ilivyokuwa hapo awali. Kwa mantiki hii, jamii za Kitanzania zilianza kutoka kwenye misingi yao ya maisha na kuingia kwenye misingi mipya ambayo ilitingisha na kuathiri mifumo ya asili ya maadili.

## Maadili ya Kitanzania yaliyodumishwa wakati wa ukoloni

Maadili ya jamii za Kitanzania yaliendelea kudumishwa hata wakati wa ukoloni.

Ingawa kulikuwa na jitihada kadhaa za kubadilisha maadili hayo kutokana na ushawishi wa wakoloni, bado maadili yaliendelea kuwa nguzo muhimu katika jamii. Katika awamu ya mwisho ya ukoloni, mawazo ya utaifa na harakati za uhuru yaliibuka na kuungwa mkono na baadhi ya wazungu wenye msimamo huria. Hali hii ilichangia kuunda maadili mapya ya kisiasa na kijamii, ambapo watu walihimizwa kujivunia utambulisho wao wa Kitanzania na kupinga utawala wa kikoloni. Hata hivyo, wakati wa ukoloni, baadhi ya maadili ya kiutamaduni ya Kitanzania yaliendelea kuhifadhiwa na jamii za wenyeji. Baadhi ya maadili haya yanaelezwa katika sehemu zinazofuata.

**Umoja na ushirikiano:** Dhana ya maisha ya jumuiya na uwajibikaji wa pamoja ilikuwa tunu kuu katika jamii nyingi za Kitanzania. Kwa mfano, miongoni mwa Wachaga wa Kilimanjaro, kilimo cha jumuiya na kazi za pamoja zilikuwa na umuhimu mkubwa. Vitendo hivi vilichangia kudumisha mshikamano wa kijamii na kuhakikisha kwamba hakuna mwanajamii aliyeachwa nyuma, hata katika mazingira ya shinikizo la utawala wa kikoloni. Shughuli za pamoja kama vile kilimo, ujenzi, au shughuli nyingine za kijamii zilifanywa kwa manufaa ya jamii nzima ili kuimarisha uhusiano wa kijamii.

**Heshima kwa wazee:** Licha ya utawala wa kikoloni, jamii za Kitanzania ziliendelea kuzingatia kanuni za kiutamaduni zilizosisitiza heshima kwa wazee. Kwa mfano, jamii za Wazaramo wa eneo la pwani ziliendelea kushikilia maadili haya wakati wa ukoloni, ambapo wazee walitumika kutoa ushauri na kufanya uamuzi. Aidha, wazee walikuwa walinzi wa maarifa, mila, ujuzi na mapokeo ya kijamii.

Vilevile, jamii ya Wamasai iliendelea kushikilia tamaduni zao za kuonesha heshima kwa wazee na viongozi wa jadi. Heshima hii kwa viongozi ilikuwa muhimu kwani ilidumisha umoja na mshikamano wa kijamii. Hivyo, kudumisha utulivu wa kijamii na mwendelezo wa utamaduni na maadili, licha ya usumbufu uliosababishwa na ukoloni. Kwa ujumla, kuheshimu wazee na watu waliowazidi umri kulikuwa na nafasi kubwa katika jamii nyingi za Kitanzania hata katika kipindi cha ukoloni.

**Mifumo ya haki ya jadi:** Jamii nyingi za Kitanzania ziliendelea kutumia mifumo yao ya haki ya jadi katika kutatua migogoro. Kwa mfano, miongoni mwa jamii za Wasukuma katika Kanda ya Ziwa, kulikuwa na mabaraza ya kimila yaliyowajibika kusuluhisha migogoro ndani ya jamii. Mabaraza haya, yalishirikiana na mfumo wa kisheria wa kikoloni lakini yalisalia kuwa chombo muhimu cha kudumisha sheria na utulivu ndani ya jamii. Jambo hili linadhihirisha uimara wa mifumo ya utawala wa kimila. Mifano hii inaonesha jinsi tunu za Kitanzania zilivyohifadhiwa na kubadilishwa wakati wa ukoloni na hivyo kuonesha uthabiti wa mila na desturi katika kukabiliana na athari za nje.

FOR ONLINE READING ONLY

**Ukarimu:** Jamii za Kitanzania zilijulikana kwa ukarimu wao na thamani hii iliendelezwa hata wakati wa ukoloni. Jamii hizi ziliamini katika umuhimu wa kuwatendea wageni kwa heshima na ukarimu. Pia, jamii hizi ziliendelea kusisitizwa kuonesha uvumilivu na utu katika kuishi na kushirikiana na watu wa tamaduni tofauti, huku wakijifunza na kuchangamana nao. Thamani ya umoja na mshikamano ilisisitizwa katika kukabiliana na changamoto za ukoloni, kihistoria na kiuchumi, ambapo jamii hizi zilipigania uhuru na haki ya kujitawala.

**Utii kwa mamlaka:** Wakati wa utawala wa kikoloni, heshima kwa uongozi wa ndani na miundo ya kimila iliendelea kudumishwa. Heshima hii ilienea pia kwa watawala wa kikoloni, ingawa mara nyingi iliambatana na upinzani. Kwa mfano, chini ya utawala wa kikoloni, jamii nyingi za Kitanzania ziliendelea kuwaheshimu viongozi wao wa kimila kama machifu, wazee na wakuu wa koo. Viongozi hawa walionekana kama mamlaka halali zinazosimamia masilahi ya jamii. Kwa mfano, jamii za Wachaga na Wahehe ziliendelea kuwaheshimu machifu wao, ambao walijulikana kama Mangi na Mtwa mtawalia, kama viongozi wao halali. Licha ya kuwepo kwa watawala wa kikoloni, jamii nyingi za Kitanzania mara nyingi zilishauriana na machifu wao katika kutoa uamuzi na miongozo mbalimbali. Hali ambayo ilidhihirisha heshima kwa mifumo yao ya utawala wa kimila.

**Utamaduni wa masimulizi:** Uwasilishaji wa historia, utamaduni na maadili kupitia masimulizi, hadithi, mashairi, methali na nyimbo ulibaki kuwa njia muhimu ya kuhifadhi historia na utambulisho wa makabila/jamii mbalimbali za Kitanzania. Maadili haya yalikuwa muhimu kwa mifumo ya jamii za Kitanzania. Hii ilisaidia kudumisha utambulisho na mwendelezo hata chini ya utawala wa kikoloni. Simulizi hizi zilikuwa na mchango mkubwa katika kuhifadhi historia, maadili na imani za jamii za Kitanzania na zilizuia rekodi hizi kupotoshwa na wakoloni.

Vilevile, mapokeo ya simulizi yaliwezesha jamii kudumisha utambulisho wao kwa kurithisha hadithi, methali, nyimbo, utani na ngano ambazo zilikuwa na urithi wao wa kitamaduni. Kwa mfano, hadithi kuu za Wasukuma, ambazo zilirithishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine, zilibeba kumbukumbu ya hekima na ujasiri wa mababu zao na zilitumika kama chanzo cha fahari na utambulisho, hata wakati ambapo wakoloni walijaribu kukandamiza tamaduni za wenyeji.

Aidha, utamaduni wa masimulizi ulichangia kueneza hisia za kupinga ukoloni. Kwa mfano, hadithi na nyimbo zilitumika kukosoa mamlaka za kikoloni, kutia moyo ujasiri na kukuza mshikamano miongoni mwa wanyonge. Mathalani, nyimbo na ngoma miongoni mwa jamii za Wangoni waliopo kusini mwa Tanzania zilijumuisha ujumbe wa upinzani dhidi ya majeshi ya kikoloni ya Wajerumani wakati wa Vita

FOR ONLINE READING ONLY

ya Majimaji, iliyopiganwa kuanzia mwaka 1905 hadi 1907. Vilevile, nyimbo hizi zilitumika kuwahamasisha na kuwaunganisha wapiganaji dhidi ya majeshi ya kikoloni ya Wajerumani.

Kadhalika, utamaduni wa masimulizi ulisaidia kueneza elimu kwa vizazi vichanga kuhusu maadili, kanuni za kijamii na stadi maisha. Wakati wa ukoloni, mifumo rasmi ya elimu ilidhibitiwa na wakoloni, hivyo jamii zilihakikisha kwamba watoto wa Kitanzania wanaendelea kujifunza utamaduni na historia yao kupitia kwa wazee. Kwa mfano, miongoni mwa jamii za Wanyamwezi, wazee walisimulia hadithi ili kutoa mafunzo kuhusu ushujaa, hekima na umuhimu wa jumuiya, ambayo yalikuwa muhimu katika kusaidia jamii kukabiliana na changamoto za utawala wa kikoloni.

**Zoezi la 2.5**

1. Kwa nini wakoloni walishindwa kutokomeza maadili ya Kitanzania pamoja na jitihada kubwa walizozifanya?
2. Eleza umuhimu wa masimulizi katika kuyadumisha maadili ya Kitanzania.
3. Bainisha maadili mengine ya jamii za Kitanzania yaliyodumu licha ya ushawishi wa utawala wa kikoloni kuyafuta.
4. Eleza mchango wa serikali ya Tanzania katika kuenzi na kudumisha maadili ya Kitanzania.

**Mavazi:** Jamii za Kitanzania ziliendelea kuenzi mavazi yao ya kiasili hata katika kipindi cha ukoloni. Jamii mbalimbali zilichukua juhudi za kipekee kuendeleza na kusambaza maarifa ya mavazi ya jadi kwa vizazi vilivyofuata, zikitambua umuhimu wa kuheshimu na kudumisha utamaduni wao wa kipekee licha ya shinikizo kubwa la kuvaa mavazi tofauti yaliyoletwa na wageni. Mavazi ya Ulaya Magharibi yalijenga taswira ya ubora wa utamaduni wao, imani mpya, nguvu, ustaarabu na usomi. Mavazi ya asili yalienziwa kupitia matamasha, mikusanyiko na sherehe mbalimbali za kijadi kama vile sherehe za mavuno, jando na unyago, harusi na tohara.

**Kazi ya kufanya 2.5**

Fanya utafiti katika jamii unamoishi na bainisha maadili ya jamii za Kitanzania yaliyokuwepo wakati wa ukoloni ambayo bado yanaenziwa hadi wakati wa sasa.

FOR ONLINE READING ONLY

## Zoezi la marudio

1. Eleza dhana ya "maadili" katika utamaduni wa Mtanzania.
2. Jadili nafasi ya vijana katika kukuza maadili kwa jamii ya Kitanzania.
3. Eleza jinsi sera za kikoloni zilivyochangia katika mabadiliko ya maadili ya jamii za Kitanzania.
4. Eleza athari za dini za kigeni katika mila na desturi za jamii za Kitanzania.
5. Nini athari za mfumo wa elimu ya kikoloni katika maadili ya Kitanzania.
6. Eleza matokeo ya muda mrefu ya ukoloni kwa maadili ya jamii ya Kitanzania.
7. Fafanua mbinu mbalimbali zilizotumiwa na jamii za Kitanzania kupinga mifumo iliyokuwa inaathiri maadili yao wakati wa ukoloni.

FOR ONLINE READING ONLY

Sura ya Tatu

# Mapambano ya awali dhidi ya uvamizi wa kikoloni

## Utangulizi

Jamii za Kitanzania zilitumia mbinu na njia mbalimbali kuukataa na kuupinga uvamizi wa kikoloni. Katika sura hii, utajifunza kuhusu dhana ya uvamizi wa kikoloni na sababu za kupinga uvamizi wa kikoloni. Pia, utajifunza mbinu na njia zilizotumika katika kuupinga uvamizi wa kikoloni. Umahiri utakaoujenga utakusaidia kuenzi, kuthamini na kuendeleza harakati za ukombozi dhidi ya unyonyaji na ukandamizaji wa aina mbalimbali katika jamii.

**Fikiri**

Mapambano ya jamii za Kitanzania dhidi ya uvamizi wa kikoloni.

### Dhana ya uvamizi wa kikoloni

Uvamizi wa kikoloni ni kitendo cha nchi moja kuingia katika nchi nyingine kwa lengo la kuanzisha utawala wake kisiasa, kiuchumi na kijamii. Mara nyingi, uvamizi huu hutekelezwa kwa kutumia nguvu za kijeshi. Uanzishwaji wa utawala wa kikoloni hutegemea kushindwa kwa nchi inayovamiwa kujilinda au kuzuia uvamizi huo. Uvamizi wa kikoloni nchini Tanzania (Tanganyika na Zanzibar) ulipingwa vikali kwa sababu jamii za Kitanzania zilifahamu kwamba kuruhusu wakoloni kuvamia kungesababisha kupoteza uhuru wao.

Kwa sababu za kizalendo na kupenda jamii zao, viongozi wengi wa jamii za Kitanzania waliongoza mapambano dhidi ya uvamizi huo tangu miaka ya 1880 na mapambano hayo yaliendelea hata baada ya ukoloni kuanzishwa nchini Tanganyika. Wananchi walipinga na kuonesha wazi hisia zao za kutokubali dhuluma na unyanyasaji kutoka kwa wakoloni, hali iliyojitokeza karibu katika kila sehemu ya Tanzania. Mapambano ya awali dhidi ya wakoloni yalihusisha jamii moja moja, jambo ambalo linamaanisha kuwa, hatua za mwanzo za kuupinga uvamizi wa kikoloni hazikuhusisha nguvu za pamoja za jamii mbalimbali za Kitanzania au taifa moja la Tanzania.

FOR ONLINE READING ONLY

Mapambano haya yalilenga kuzuia kuingizwa kwa maadili ya kikoloni katika jamii za Kitanzania. Jamii hizi zilikuwa na maadili, mila na desturi zilizowiana na mazingira yao, pamoja na lugha, ngoma na imani za kidini (dini za jadi). Kila jamii ilikuwa na imani katika Mungu, ambaye alitambulika kwa majina mbalimbali ya kijadi kama vile *Mlungu, Mnungu* (kwa Wazigua), *Kyala* (kwa Wanyakyusa), *Ruwa* (kwa Wachaga) na *Ngai* (kwa Wamasai).

Hata hivyo, baada ya kuingia kwa wakoloni na kuanzisha utawala wao, utamaduni na maadili ya jamii za Kitanzania yalidhoofishwa na kutajwa kuwa ya kishenzi. Wakoloni walileta utamaduni kutoka katika mataifa yao uliosisitiza maadili ya kibepari, ikiwa ni pamoja na ubaguzi wa rangi, uporaji, ukatili, unyonyaji, unyanyasaji, matabaka na ubinafsi. Pia, walileta maadili ya dini za kigeni (Ukristo na Uislamu) ambayo mara nyingi yalipingana na maadili ya dini za jadi.

**Kazi ya kufanya 3.1**

Soma matini kutoka vyanzo mbalimbali na ubainishe tofauti ya uvamizi uliokuwepo kati ya Afrika Mashariki ya Kijerumani (Tanganyika) na Zanzibar.

**Kazi ya kufanya 3.2**

Kwa kutumia taarifa kutoka vyanzo mbalimbali fanya uchunguzi kuhusu Karl Peters alivyoingia mikataba ya kilaghai. Andika insha yenye maneno mia tatu (300) ukiwashauri viongozi wa kizazi cha sasa kipi cha kujifunza kutokana na mikataba ya Karl Peters.

**Zoezi la 3.1**

1. Eleza dhana ya mtawala na mtawaliwa.
2. Tofautisha utawala wa Waarabu Zanzibar na ule wa Wajerumani katika Afrika Mashariki ya Kijerumani.
3. Fafanua mbinu zilizotumiwa na wakoloni kuanzisha utawala wa kikoloni Tanganyika.
4. Eleza namna maadili ya kibepari yanavyoendelea kuathiri maadili ya jamii za Kitanzania wakati wa sasa.

FOR ONLINE READING ONLY

## Sababu za kuupinga uvamizi wa kikoloni na maadili yake

Utawala wa kikoloni nchini Tanzania ulisababisha kupotea kwa uhuru, kudunishwa na kuharibiwa kwa maadili ya jamii. Wakoloni walidhihaki mila na desturi ambazo zilikuwa msingi wa maadili ya jamii. Hali hii iliwachochea wananchi, chini ya uongozi wa viongozi wao hodari na shupavu wa jadi, kuupinga utawala wa kigeni ili kulinda uhuru, utamaduni na maadili yao.

Aidha, wananchi walinyonywa kwa kulazimishwa kufanya kazi za vibarua na kulipwa ujira mdogo katika mashamba ya mkonge, pamba, chai, tumbaku na pareto. Wakulima, wakiwa chini ya usimamizi mkali wa majumbe na wanyapara, walidhalilishwa kwa kuchapwa viboko. Pia, wananchi walilazimishwa kulima mazao ya biashara kama pamba, kahawa na chai kwa faida ya wakoloni na mabepari wa Ulaya Magharibi, ambapo mazao hayo yaliuzwa kwa bei ndogo.

Zaidi ya hayo, mfumo mpya wa kodi ulioanzishwa na wakoloni uliwalazimisha wananchi kulipa kodi ya kichwa na kodi nyingine kwa pesa tasilimu. Jambo hili liliwakera sana kwa kuwa hawakuwa na pesa, hivyo walilazimika kuuza mifugo yao, kufanya kazi za vibarua kwa wakoloni na walowezi au kulima mazao ya biashara ili kupata pesa za kulipa kodi.

Wakoloni walitumia adhabu za kikatili kama kuwanyonga viongozi wa jamii za Kitanzania waliopinga utawala na maadili yao. Wananchi pia waliteswa na kudhalilishwa hadharani kwa kuchapwa viboko walipo shindwa kulipa kodi au walipotenda makosa mengine dhidi ya utawala wa kikoloni, jambo lililoshusha heshima, ushujaa na utu wao ambao ulikuwa umejengwa kwa muda mrefu na jamii zao za asili.

Aidha, ardhi yenye rutuba iliporwa na wakoloni kwa ajili ya kilimo cha mazao ya biashara, hali iliyowafanya wananchi washindwe kukidhi mahitaji yao ya chakula kutokana na kuwa na mashamba madogo yasiyo na rutuba ya kutosha. Hatimaye, wananchi walinyang'anywa udhibiti wa maeneo yao ya biashara kwa mfano, Wahehe walipambana na Wajerumani walipojaribu kuimarisha na kupanua mipaka yao ya biashara, jambo lililosababisha chuki na mapambano.

FOR ONLINE READING ONLY

**Kazi ya kufanya 3.3**

Fanya utafiti mdogo, kisha andika taarifa kuhusu jinsi uvamizi wa kikoloni ulivyosababisha mmomonyoko wa maadili katika jamii za Kitanzania.

## Zoezi la 3.2

1. Je, ni sababu gani ziliwafanya jamii za Kitanzania kupinga utawala wa kikoloni?
2. Eleza mbinu ambazo jamii za sasa za Kitanzania zinaweza kutumia kulinda rasilimali, utamaduni na maadili ya jamii zao.
3. Jadili namna maadili ya Watanzania yaliyokiukwa kutokana na uvamizi wa kikoloni.
4. Fafanua athari za kiuchumi kwa jamii za Kitanzania zilizosababishwa na utawala wa kikoloni.

## Upinzani dhidi ya uvamizi wa kikokoni katika jamii za Kitanzania

Karibu jamii zote za Kitanzania ziliupinga uvamizi wa kikoloni kwa sababu hakuna jamii iliyopenda kuupoteza uhuru na utamaduni wake kwa wageni. Jinsi jamii hizi zilivyoupinga uvamizi huo, au njia gani walizozitumia zilitegemea uwezo wa kivita, kiuchumi, mazingira na uongozi bora na imara. Kwa hiyo, kuna jamii zilizoupinga ukoloni kwa kupigana vita, zingine kwa kujisalimisha na nyingine kwa kuungana na wavamizi.

### Njia ya kupambana kwa vita

Njia ya vita ilikuwa maarufu zaidi kati ya jamii za Kitanzania, kwani jamii nyingi hazikuwa tayari kuupoteza uhuru wao na hivyo ziliupinga waziwazi uvamizi huo kwa kutumia vita. Jamii hizi nyingi zilikuwa na uongozi shupavu, zilimiliki silaha, zilikuwa na uwezo wa kiuchumi na nyingi pia zilikuwa chini ya dola zenye nguvu. Mapambano dhidi ya uvamizi yalihusisha jamii moja moja au jamii nyingi kwa pamoja. Kwa mfano, mapambano ya mwanzo dhidi ya uvamizi wa kikoloni na maadili yake yalihusisha jamii moja moja na siyo makabila mengi au nchi nzima.

*Mapambano ya Wanyamwezi:* Harakati za kuupinga uvamizi wa kikoloni magharibi mwa Afrika Mashariki ya Kijerumani, ziliongozwa na Mtemi wa Wanyamwezi aliyejulikana kama Isike au Mwana Kiyungi kuanzia mwaka 1886 hadi 1891. Mtemi Isike alipinga vikali uvamizi wa Wajerumani katika himaya yake baada ya maeneo yake ya kiutawala kuporwa. Pia, alitetea masilahi ya biashara iliyokuwa ikifanyika miongoni mwa jamii ya Wanyamwezi huko Tabora. Mtemi Isike alikusanya ushuru kutoka kwa wafanyabiashara wa Kiarabu waliokuwa wakipita katika himaya yake kuelekea Ujiji mpaka Katanga (sasa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo), Burundi na wengine kaskazini kuelekea kanda ya Ziwa Viktoria hadi ufalme wa Buganda na Bunyoro.

FOR ONLINE READING ONLY

Ili kulinda uhuru na maadili ya jamii ya Wanyamwezi, Mtemi Isike aliwaongoza kwa ushupavu askari wake kupambana na majeshi ya Wajerumani. Zaidi ya askari 1000 wa jeshi la Wajerumani walipambana vikali na askari wa Isike. Hata hivyo, ngome ya Mtemi Isike ilivunjwa na majeshi ya kivamizi ya Wajerumani. Isike alipoelemewa, aliona ni bora ajiue kuliko kukamatwa na Wajerumani, hivyo alijilipua kwa baruti pamoja na familia yake mnamo mwaka 1893. Hii inaonesha kuwa Mtemi Isike alikuwa mzalendo wa kweli aliyekuwa tayari kufa kwa ajili ya nchi yake na hakuwa tayari kunyanyaswa na wavamizi wa kikoloni.

*Mapambano ya jamii za watu wa pwani:* Mapambano ya awali dhidi ya uvamizi wa Kijerumani katika ukanda wa pwani ya Afrika Mashariki ya Kijerumani (sasa Tanzania) yaliongozwa na wafanyabiashara mashuhuri Abushiri bin Salim al-Harthi wa Pangani na Bwana Heri bin Juma wa Uzigua. Viongozi hawa waliongoza mapambano dhidi ya sera za unyonyaji za Wajerumani, ambazo zilivuruga na kutishia masilahi ya biashara katika ukanda wa pwani na pia kupora uhuru wao.

Mwaka 1889, Abushiri bin Salim aliwaongoza wananchi wa pwani katika maeneo ya Pangani kupigana na Wajerumani na kufanikiwa kuwaondoa katika baadhi ya maeneo ya pwani. Kutokana na upinzani mkali alioutoa kwa majeshi ya Kijerumani, Wajerumani waliomba msaada kutoka kwa majeshi ya Uingereza. Muungano huu ulisababisha Abushiri kukimbia kwa sababu za kiusalama. Kwa kutumia njia ya kugawa umoja miongoni mwa jamii za Kitanzania, Wajerumani walifanikiwa kumkamata Abushiri bin Salim al-Harthi baada ya kusalitiwa na Chifu Magaya wa Usagara. Mwaka 1889, Abushiri bin Salim al-Harthi aliuawa kikatili kwa kunyongwa hadharani na Wajerumani huko Bagamoyo. Kielelezo 3.1 kinaonesha Abushiri bin Salim.



**Kielelezo 3.1**: *Abushiri bin Salim*

Bwana Heri bin Juma aliwaongoza Wazigua wa maeneo ya Saadani dhidi ya uvamizi wa Wajerumani. Ingawa baadaye alishindwa, aliendesha mapambano makali ambayo yalionesha jinsi wananchi walivyokuwa hawako tayari kunyanyaswa na kunyonywa na Wajerumani. Wakati huo huo, mapambano dhidi ya Wajerumani katika maeneo ya Kilwa Kivinje yaliongozwa na Hassan bin Omari Makunganya mwaka 1894. Kama ilivyokuwa kwa mashujaa wengine, Makunganya alipambana vikali sana katika maeneo yake. Hata hivyo, baadaye alikamatwa na kunyongwa na Wajerumani huko Kivinje kwenye mwembe ambao mpaka sasa unajulikana kama "Mwembe Kunyonga."

FOR ONLINE READING ONLY

**Kazi ya kufanya 3.4**

Mapambano ya kupinga uvamizi wa kikoloni hayakuwa lelemama. Machifu na Watemi waliyapoteza maisha yao wakitetea maadili na ardhi yao isivamiwe na wageni. Soma matini kutoka vyanzo mbalimbali na uandike taarifa kuhusu viongozi walionyongwa kwa kuupinga uvamizi wa kikoloni.

*Mapambano ya Wahehe*: Jamii ya Wahehe chini ya uongozi wa Mtwa Mkwawa (kama inavyoonekana kwenye Kielelezo 3.2), ilipinga vikali uvamizi wa Wajerumani kati ya mwaka 1891 na 1898 kwa njia ya vita. Kabla ya uvamizi huo, Wahehe walikuwa wamejiimarisha kibiashara kwa kudhibiti maeneo mengi. Sababu kubwa ya mapambano ya Wahehe dhidi ya Wajerumani ilikuwa kuyalinda maadili, uhuru na masilahi yao, hasa ya kiuchumi. Kwa mfano, katika jitihada za kujiimarisha kiuchumi, Wahehe walipanua maeneo yao hasa sehemu za Mpwapwa na Usagara ili kuongeza kipato kupitia ushuru waliotoza kwa misafara ya wafanyabiashara waliopita katika eneo lao kutoka Bagamoyo kwenda bara huko Tabora, Ujiji, kanda ya Ziwa na Katanga.

Kwa upande wao, Wajerumani walikuwa wanapanua himaya yao kuelekea bara na walikasirishwa na kitendo cha Wahehe kuendelea kujiimarisha kwa kuongeza maeneo kama Usagara, Mpwapwa na Ugogo. Kuimarika kwa himaya ya Wahehe kulisababisha Wajerumani kukosa mapato ya ushuru na malighafi kutoka bara. Aidha, Wahehe walikuwa wanaendeleza nguvu zao kutoka Kalenga, ambayo ilikuwa ngome ya Mtwa Mkwawa hadi maeneo mengine.

Wahehe walipendelea kumaliza mzozo wao na Wajerumani kwa njia ya mazungumzo ya amani, hivyo Mkwawa alituma askari wawili kupeleka ujumbe kwa kiongozi wa Wajerumani huko pwani. Hata hivyo, Wajerumani walihisi askari hao walikuwa wapelelezi na hivyo waliwaua. Kitendo hiki cha kikatili kilimkasirisha sana Mtwa Mkwawa na ndipo alipoamua kuanzisha mapambano rasmi dhidi ya Wajerumani.

Mapambano ya kwanza ya kijeshi kati ya Wahehe na Wajerumani yalifanyika mwaka 1891 katika eneo la Lugalo. Wanajeshi wa Kijerumani chini ya uongozi wa kamanda Emil von Zelewisky (aliyejulikana kwa jina la Nyundo), walitumwa kuangamiza Wahehe. Katika mapigano hayo, wapiganaji wa Kihehe waliwashinda Wajerumani na askari 300 wa Kijerumani pamoja na kiongozi wao waliuawa. Kaburi la kiongozi huyo wa Kijerumani bado lipo katika eneo la Lugalo, mkoani Iringa, hadi leo. Kielelezo 3.3 kinaonesha mnara wa kumbukumbu walipouwawa askari wa Kijerumani wakiongozwa na Emil Zelewisky huko Lugalo Iringa mwaka 1891.

FOR ONLINE READING ONLY



**Kielelezo 3.2**: *Mtwa Mkwawa*



**Kielelezo 3.3**: *Mnara wa kumbukumbu walipouwawa askari wa Kijerumani*

Licha ya kushindwa mwaka 1891, Wajerumani waliendelea kujiimarisha kivita kwa kuanzisha vikosi vya kijeshi katika maeneo ya Kilosa na Kisaki. Baada ya kujiimarisha, Wajerumani walituma wajumbe kwa Mtwa Mkwawa wakimtaka aitambue serikali ya Wajerumani, alipe gharama za vita, aache kuvamia misafara ya kibiashara katika maeneo jirani na utawala wake, asalimishe silaha zilizotekwa na aruhusu wafanyabiashara na wamisionari kutumia eneo lililokuwa chini ya utawala wake. Mkwawa alikataa mapendekezo yote hayo, akipinga ukatili, unyonyaji na unyanyasaji uliokuwa unafanywa na Wajerumani.

Mwaka 1894, Wajerumani chini ya Kamanda Tom Prince walivamia ngome ya Wahehe huko Kalenga. Mkwawa alikimbilia mafichoni na kuendelea na vita vya msituni. Mwaka 1898, Mtwa Mkwawa aliamua kujiua badala ya kukamatwa na Wajerumani. Kifo cha namna hii kilikuwa ushujaa wa aina yake, kwani Mkwawa aliona ni fedheha kwa shujaa kukamatwa, kunyanyaswa na kuuawa kikatili kwa kunyongwa na wavamizi.

*Mapambano ya Wayao*: Mapambano ya kupinga uvamizi wa Wajerumani upande wa kabila la Wayao yaliongozwa na kiongozi wao jasiri na shupavu, Mwene Machemba. Mwene Machemba alishinda karibu mapigano yote aliyoyaongoza dhidi ya Wajerumani. Ushindi huu ulitokana na ukweli kwamba Mwene Machemba alikuwa kiongozi hodari, shupavu na mwenye kupenda kutetea maadili na uhuru wa watu wake. Kwa mfano, katika barua aliyowaandikia Wajerumani, Mwene Machemba

FOR ONLINE READING ONLY

alisema: *"Nimesikiliza maneno yenu, lakini sijaona sababu ya kuwatii. Niko tayari kufa…, sisemi mnitii mimi kwa kuwa nyie ni watu huru kama mimi."* Maneno haya yanaonesha jinsi alivyosimamia utu na uhuru wa watu wake kwa ujasiri mkubwa.



**Kielelezo 3.4**: *Mwene Machemba*

Hata hivyo, Mwene Machemba alikimbilia Msumbiji baada ya kupambana vikali na majeshi ya Wajerumani, ambapo Wayao walizidiwa nguvu na kushindwa vita. Kielelezo 3.4 kinaonesha picha ya Mwene Machemba.

*Mapambano ya Wachaga*: Mapambano dhidi ya uvamizi wa Wajerumani katika jamii ya Wachaga yaliongozwa na viongozi wa Kibosho na Moshi. Kwa upande wa Kibosho, wakiwa chini ya uongozi wa Mangi Sina, walipinga kitendo cha Wajerumani kuingilia mgogoro uliokuwepo miongoni mwa watawala wa Kibosho, Moshi na Marangu. Kitendo hicho kilimuudhi Mangi Sina, kwani kilionekana kuwa na nia ya kuwagawa. Kwa hasira, Mangi Sina aliichana bendera ya Wajerumani, kitendo ambacho kilikuwa ishara ya kuupinga ukatili na unyanyasaji uliokuwa unafanywa na Wajerumani Uchagani. Kitendo hicho kiliwakasirisha Wajerumani, ambao walituma majeshi ya kukodi ya Wanubi kutoka Sudani ili kupambana naye. Hata hivyo, baada ya kuzidiwa nguvu na majeshi ya Wajerumani, Mangi Sina alilazimika kutoroka.



**Kielelezo 3.5:** *Mangi Meli*

Vilevile, Mangi Meli aliongoza mapambano dhidi ya Wajerumani huko Moshi, akipinga ukatili na mfumo wa unyanyasaji na unyonyaji wa wakoloni. Katika mapambano hayo, kamanda wa jeshi la Wajerumani, Von Bulow, aliuawa. Kwa kulipiza kisasi, Wajerumani walimshambulia Mangi Meli, wakamkamata na baadaye wakamnyonga kwa ukatili kijijini kwake. Kielelezo 3.5 kinaonesha picha ya Mangi Meli.

*Vita vya Liti Kidanka dhidi ya Wajerumani* (*1908-1910*): Wajerumani walifika Singida mnamo mwaka 1901. Wajerumani walikabiliana na upinzani mkali kutoka kwa Wanyaturu, walioongozwa na mwanamke shupavu, Liti Kidanka, kupinga uvamizi huo. Liti Kidanka hakutaka Wajerumani watawale eneo ambalo sasa ni Mji wa Singida. Hivyo, aliongoza mapambano makali dhidi ya askari wa Kijerumani walioongozwa na Kapteni Eberhard von Sick.

FOR ONLINE READING ONLY

Liti na askari wake walipambana na Wajerumani mara mbili na kufanikiwa kuwakimbiza nje ya mji wa Singida kwa kutumia mbinu ya kipekee ya silaha ya nyuki wakali. Wakati vita vilipokuwa vikipamba moto, nyuki hao walifunguliwa na kuwashambulia Wajerumani pekee na askari wao. Mapambano kati ya Liti na Wajerumani yalidumu kwa miaka mitatu, kuanzia mwaka 1908 hadi 1910.



**Kielelezo 3.6:** *Liti Kidanka*

Hata hivyo, katika jaribio la tatu na la mwisho, Liti hakufanikiwa kuwashinda Wajerumani kutokana na kusalitiwa na mmoja wa washirika wake. Hivyo, Wajerumani walimkamata yeye na mume wake, Nyalandu Mtinangi na kuwaua. Kichwa cha shujaa huyu kilikatwa na kupelekwa Ujerumani. Kielelezo 3.6 kinaonesha picha ya Liti Kidanka.

Hii ni mifano michache ya mapambano ya kuupinga uvamizi wa kikoloni kwa njia ya vita yaliyofanywa na makabila moja moja. Zaidi ya hayo, jamii za Kitanzania zilitumia njia ya vita kupinga mfumo wa ukoloni na hasa uchumi wa kikoloni kwa kushirikisha makabila mengi. Hata hivyo, ni muhimu kufahamu kuwa makabila haya yalipigana kila moja kivyake. Mfano mzuri wa aina hii ya mapambano ya kushirikisha makabila mengi ni Vita ya Maji Maji.

*Mapambano ya jamii za Kusini mwa Afrika Mashariki ya Kijerumani*: Mapambano ya jamii za kusini, yajulikanayo kama Vita vya Maji Maji, yalianza mwaka 1905 na kumalizika mwaka 1907. Kiongozi wa mapambano haya alikuwa Kinjekitile Ngwale wa kabila la Wamatumbi, ambaye aliwaongoza Wamatumbi kupinga ukatili, unyonyaji na ukandamizaji wa Wajerumani. Kinjekitile alikuwa kama roho ya mapambano hayo na aliwaahidi kuwalinda wafuasi wake dhidi ya Wajerumani.

Alidai kuwa ameoteshwa dawa ambayo ingewaepusha na risasi za wavamizi. Dawa hiyo ilikuwa ni maji yaliyochanganywa na mtama, yaliyodaiwa kuwa na uwezo wa kuzigeuza risasi kuwa maji. Wanajamii waliamini ahadi zake na, hata vita vilipoanza, wakoloni waliporusha risasi, wao walitamka "maji." Hata hivyo, kadri walivyosema "maji," ndivyo walivyopoteza maisha. Vita hivi vilienea katika maeneo ya kusini na mashariki mwa Afrika Mashariki ya Kijerumani, kama vile Rufiji, Mohoro, Somanga, Kibata, Nandete, Mikindani, Liwale, Lindi, Songea, Njombe na Mahenge. Kinjekitile alitumia mbinu hii ili kuwaunganisha na kujenga mshikamano miongoni mwa wananchi ili wapambane na mkoloni bila hofu. Angalia Kielelezo 3.7 kinachoonesha baadhi ya jamii zilizopinga utawala wa Wajerumani.

FOR ONLINE READING ONLY




**Kielelezo 3.7:** *Jamii zilizopinga utawala wa Wajerumani*

**Kazi ya kufanya 3.5**

Kwa kutumia vyanzo mbalimbali vya taarifa ikiwemo mitandao andika nukuu ya *Mwene* Machemba kwenye barua aliyowaandikia Wajerumani, kisha eleza jinsi alivyopinga uvamizi kwa nguvu zake zote.

### Kwa njia ya kuungana

Kuna jamii za Kitanzania zilijua nguvu ya kijeshi ya Wajerumani na hawakuwa tayari kupambana na kuupinga uvamizi wao moja kwa moja. Lakini waliungana ili kuweza kuwashinda maadui wao. Hii ilitokana na imani kwamba, baada ya kuwashinda maadui wao wa muda mrefu wangebaki kuwa na nguvu zaidi na kujiimarisha. Pia, kuungana huku walikusudia kupata misaada ya silaha na vifaa vingine kutoka kwa Wajerumani. Silaha na vifaa hivyo vingewafanya kuwa imara zaidi hata kuwashinda

FOR ONLINE READING ONLY

wavamizi kama Wajerumani baadae. Lakini baadae mpango wao ulishindwa na wao kujikuta wakitawaliwa kirahisi zaidi. Mfano wa jamii hizi za Kitanzania ni kama vile Wachaga. Ambao chini ya Mangi Mandara waliungana na Wajerumani ili kumshinda Mangi Sina; Mangi Marealle aliungana na Wajerumani ili kumshinda Mangi Meli; Wasangu na Wabena chini ya Mtwa Merere na Mbeyela mtawalia waliungana na Wajerumani dhidi ya Wahehe chini ya Mtwa Mkwawa na jamii zingine nyingi. Ukweli ni kwamba jamii hizi zote zilishindwa kupata walichokitarajia na mwisho kutawaliwa kirahisi sana na Wajerumani. Hivyo, usaliti wao dhidi ya watawala wa jamii za Kitanzania kwa kuungana na wakoloni Wakijerumani ulikuwa ni fedheha kwao kwani haukuwa na manufaa yoyote.

**Kwa njia ya kusalimu amri**

Kuna baadhi ya jamii za Kitanzania ambazo hazikupenda kutawaliwa na wakoloni lakini zilijiona hazina uwezo wa kuweza kukabiliana na Wajerumani kivita. Nyingi ya jamii hizi ni zile zilizokuwa zimeathirika na baa la njaa au magonjwa, ukosefu wa dola zenye nguvu mazingira magumu ya kivita na sifa nyingine kama hizo. Kwa mfano, jamii ya Kimasai hapa nchini ilisalimu amri kwa Wajerumani kufuatia kupatwa na majanga ya magonjwa ya Wanyama miaka ya 1870s na 1880s na mazingira yake kutokuwa mazuri kwa vita.

**Zoezi la 3.3**

1. Fafanua namna jamii za Watanzania na viongozi wao walivyoupinga utawala wa Wajerumani.
2. Eleza mbinu zinazoweza kutumiwa na jamii za sasa za Kitanzania kulinda rasilimali, utamaduni na maadili ya jamii zao.
3. Eleza kwa nini vita ya Maji Maji hujulikana kama vita kubwa Tanzania.

## Changamoto zilizokabili mapambano dhidi ya uvamizi wa kikoloni

Wananchi walijaribu kupambana na kupinga ukoloni, lakini wakoloni waliwazidi nguvu na kuwashinda. Zipo sababu nyingi zilizowafanya wananchi kushindwa katika mapambano hayo. Miongoni mwa sababu hizo ni kama zinavyoelezwa katika sehemu zinazofuata.

**Ukosefu wa umoja miongoni mwa jamii za Kitanzania**

Kama ilivyoonekana, mapambano dhidi ya ukoloni yalifanywa kati ya wakoloni na jamii moja moja za Kitanzania. Hii inamaanisha kuwa, katika kipindi cha ukoloni, jamii za Kitanzania zilishindwa kwa sababu zilikosa umoja na hazikushirikiana kupambana na wakoloni. Kwa mfano, hata katika vita ya Maji Maji, makabila hayakuungana yote kwa pamoja kila kabila lilipigana kivyake katika eneo lake.

FOR ONLINE READING ONLY

**Matumizi ya silaha duni dhidi ya silaha bora za Wajerumani**

Katika sehemu kubwa ya Tanzania, wananchi walioshiriki katika mapambano hawakufanikiwa kuangusha utawala wa kikoloni kwa sababu Wajerumani walitumia silaha bora zaidi kuliko zile zilizotumiwa na wananchi. Kwa mfano, Wajerumani walitumia mizinga na bunduki, wakati wananchi walitumia pinde, mishale, ngao, mawe, marungu na majambia.

**Usaliti**

Baadhi ya viongozi wa jadi waligeuka kuwa vibaraka wa serikali ya kikoloni. Katika maeneo mengi, baadhi ya jamii za Kitanzania ziliungana na Wajerumani kupigana na jamii zingine za Kitanzania. Hii ilisababisha jamii nyingi kushindwa vita, kwani jamii jirani zilizoungana na Wajerumani ziliwasaidia kufichua udhaifu na nguvu za jamii hizo na hivyo kurahisisha ushindi kwa Wajerumani. Kwa mfano, Wasangu na Wabena waliungana na Wajerumani kutoa siri na kupigana na Wahehe. Vivyo hivyo, katika jamii za Wachaga, Mangi Mandara/Rindi aliungana na Wajerumani kumshinda Mangi Sina.

**Maandalizi duni**

Wananchi hawakuwa na maandalizi mazuri ya vita ikilinganishwa na wavamizi wa kikoloni. Wavamizi walikuwa na muda mzuri wa kujiandaa kwa vita, wakati jamii nyingi za Kitanzania zilijikuta katika vita ghafla, mara baada ya kuona wavamizi tayari wamevamia. Jamii za Kitanzania zilikuwa hazijamjua vyema adui yao, hali iliyochangia kushindwa kwao. Maandalizi mazuri ya Wajerumani yaliwafanya washinde vita kwa urahisi.

**Teknolojia duni ya mawasiliano**

Wajerumani walikuwa na teknolojia nzuri ya mawasiliano na usafiri, ambayo ilirahisisha mawasiliano kati ya maeneo mbalimbali. Kwa mfano, waliweza kutumia telegramu kutuma taarifa za vita kuhusu vifaa na wanajeshi kwa haraka. Hii ilikuwa ngumu kwa jamii za Kitanzania, ambazo zilitegemea njia za jadi za mawasiliano zilizochukua muda mrefu kufikisha ujumbe kwa walengwa. Pia, Wajerumani walitumia magari na vyombo vingine vya usafiri vilivyowarahisishia harakati zao, huku wapiganaji wa Kitanzania wakitumia muda mrefu kutembea kwa miguu.

**Uchumi dhaifu**

Jamii nyingi za Kitanzania zilikuwa na uchumi dhaifu ambao usingeweza kuhimili vita kwa muda mrefu. Uchumi wao ulitegemea kilimo na biashara ndogo ndogo zilizofanywa na wanajamii, ambao wakati wa vita walihitajika kuenda vitani badala ya kuendeleza shughuli zao za kiuchumi. Hii ilimaanisha kuwa kipato chao kidogo kingeweza kusaidia mapigano kwa muda mfupi tu. Wakati huo huo, Wajerumani walikuwa na uchumi imara uliowawezesha kuhimili vita kwa muda mrefu, kwani nchi ya Ujerumani ilikuwa na uwezo wa kuwasaidia kifedha.

FOR ONLINE READING ONLY

**Kazi ya kufanya 3.6**

Fanya utafiti kupitia vyanzo mbalimbali vya taarifa ili kubaini sababu nyingine zilizosababisha Watanzania kushindwa katika vita dhidi ya uvamizi wa kikoloni.

**Zoezi la 3.4**

1. Linganisha vita ya Maji Maji na vita vya jamii nyingine za Kitanzania zilizopinga uvamizi wa Wajerumani.
2. Fafanua maadili ambayo viongozi wa sasa wanaweza kujifunza kutoka kwa viongozi wa jamii za Kitanzania waliopinga uvamizi wa kikoloni.
3. Eleza athari za uvamizi wa kikoloni katika jamii za Kitanzania.

## Matokeo ya kupinga uvamizi wa kikoloni

Ni muhimu kukumbuka kuwa jamii za Kitanzania zilipambana vikali kuupinga ukoloni. Kutokana na matumizi ya silaha duni za jadi, wakoloni walifanikiwa kuzishinda na kuendelea kuzitawala. Katika kipindi chote cha vita, wananchi walijitoa kwa hali na mali, wakiongozwa na viongozi wa jadi waliotetea uhuru, haki, masilahi na utu wao. Matokeo ya mapambano hayo yalikuwa kama ifuatavyo:

**Shughuli za uzalishaji mali zilisimama:** Kipindi chote cha vita, badala ya kuzalisha, muda mwingi ulitumika katika kujipanga kivita na kupigana. Hali hii ilisababisha upungufu wa chakula na kuleta njaa kubwa, kama ilivyotokea wakati wa Vita vya Maji Maji, ambapo njaa hiyo iliitwa "Fungafunga." Njaa hii iliwafanya watu kuishiwa nguvu na kufa; wengine walilazimika kula wadudu, mizizi ya miti na matunda ya msituni, ambayo mengine yalikuwa na sumu.

**Kutumikishwa kwa nguvu kazi ya vijana:** Wanaume, hasa vijana wenye nguvu, walisafirishwa mbali na makazi yao na kutumikishwa katika mashamba ya walowezi. Pia, kulizuka maradhi ya mlipuko kama vile mafua makali, kichocho na kuhara. Maradhi haya yalisambaa kwa haraka kwa sababu wananchi wengi walikimbia makazi yao na kushindwa kupata maji salama na chakula.

**Vifo kutokana na wanyama pori:** Athari nyingine ya vita ilikuwa vifo vilivyosababishwa na wanyama pori. Wakati wa vita, wapiganaji walitumia muda mwingi msituni. Wanawake na watoto pia walikimbilia maeneo ya msituni na mapangoni kujificha na wengi wao walijeruhiwa au kuuawa na wanyama wakali wa msituni.

FOR ONLINE READING ONLY

**Hofu miongoni mwa Watanzania:** Vita vilisababisha kujengeka kwa hofu miongoni mwa Watanzania. Kutokana na kushindwa kwa mapambano, watu wengi walipata hofu ya kupigana tena na Wazungu.

**Mateso na vifo vingi:** Vita vya kupinga uvamizi wa wakoloni vilisababisha maelfu ya vifo katika mapambano, kukamatwa kwa mateka, kunyongwa na vifo vilivyotokana na njaa wakati na baada ya vita. Vilevile, vita viliathiri uzalishaji wa mazao ya biashara kama vile pamba, mkonge na mpira na pia iligharimu serikali ya kikoloni kiasi kikubwa cha fedha kugharamia vita. Kwa sababu hiyo, Wajerumani walilazimika kufanya mabadiliko katika sera zao za utawala na uchumi ili kupunguza migogoro na wananchi.

**Mwamko mpya wa harakati za uhuru:** Ingawa jamii za Kitanzania zilishindwa katika mapambano ya awali dhidi ya uvamizi wa kikoloni, mapambano hayo yaliacha alama muhimu katika historia. Jamii hizi zilionesha ujasiri na dhamira ya kweli ya kupinga ukandamizaji wa kigeni. Hali hii ilichochea mwamko mpya wa wapigania uhuru wa baadaye, ambao walijifunza mengi kutoka kwa harakati hizo za kitaifa za kudai uhuru.

**Kumbukumbu muhimu katika historia ya Tanzania:** Hapana shaka kwamba vita vya kupinga ukoloni ni kumbukumbu muhimu katika historia ya Tanzania inayostahili kuheshimiwa na yeyote anayethamini utu, uhuru, haki, heshima na usawa. Vita hivyo ni kielelezo halisi cha Watanzania kukataa utawala wa kikoloni. Wajerumani walijifunza kwamba mababu na mabibi zetu walikuwa tayari kuutetea na kuulinda uhuru na rasilimali zao. Miaka mingi imepita tangu vita hivyo kutokea na kila Mtanzania anapaswa kujiuliza ni mafundisho yapi anaweza kujifunza kutokana na matukio hayo. Je, bado tunao ule moyo wa ushujaa, uzalendo, heshima na usawa kama ilivyokuwa enzi za mababu na mabibi zetu?

## Zoezi la marudio

1. Tofautisha kati ya maadili ya kikoloni na maadili ya jamii za Kitanzania wakati ukoloni unaingia.
2. Eleza sababu za kushindwa kwa mapambano ya awali ya jamii za Kitanzania dhidi ya uvamivi wa kikoloni.
3. Eleza jinsi viongozi wa sasa wanapaswa kutetea masilahi ya wananchi kwa ujasiri na uzalendo.
4. Bainisha vitendo vya kijasiri vilivyooneshwa na viongozi wa jamii za Kitanzania waliongoza mapambano ya awali dhidi ya uvamizi wa kikoloni.
5. Je, unafikiri ni namna gani mbinu ya jadi ya kivita iliyotumiwa na Kinjeketile ilisaidia katika kupinga uvamizi wa Wajerumani?
6. Ni funzo gani viongozi wa sasa wanaweza kujifunza kutoka kwa jamii za Kitanzania zilizopinga uvamizi wa Wajerumani?

FOR ONLINE READING ONLY

# Sura ya Nne

# Harakati za kudai uhuru wa Tanganyika na Zanzibar

## Utangulizi

*Harakati za kudai uhuru wa Tanganyika na Zanzibar ziliendana na juhudi mbalimbali za kisiasa na kijamii zilizolenga kukomesha utawala wa kikoloni. Katika sura hii, utajifunza kuhusu dhana ya uhuru na harakati za kudai uhuru, pamoja na misingi na mbinu zilizotumika katika kupigania uhuru wa Tanganyika na Zanzibar. Pia, utajifunza mchango wa harakati hizo katika kuupinga utawala wa kikoloni, kuyatunza maadili ya Kitanzania na kuujenga uzalendo. Umahiri utakaoupata utakuwezesha kuthamini juhudi za wapigania uhuru wa Tanganyika na Zanzibar na pia kuuheshimu na kuuenzi uhuru wetu.*

**Fikiri**

*Harakati za kudai uhuru wa Tanganyika na Zanzibar.*

### Dhana ya uhuru na harakati za kudai uhuru

Neno "uhuru" linaweza kufafanuliwa kwa namna mbalimbali. Uhuru ni hali ya mtu au nchi kuamua na kufanya mambo yake bila kuingiliwa na mtu au taifa lolote, iwe kiuchumi, kisiasa, kijamii au kiutamaduni. Katika muktadha huu, uhuru ni hali ya nchi kujikomboa kutoka kwenye ukoloni wa mataifa ya kibepari. Harakati za kudai uhuru wa Tanganyika na Zanzibar ni mchakato au juhudi za watu wa nchi hizo kutafuta uhuru kutoka kwa serikali za kikoloni. Pia, ni hatua zilizochukuliwa na wananchi wa Tanganyika na Zanzibar hadi kufanikisha kupata uhuru wao.

Tanganyika ilitawaliwa na wakoloni wa Kijerumani kuanzia mwaka 1885 hadi 1918. Baada ya Vita ya Kwanza vya Dunia, Tanganyika ilitawaliwa na Waingereza hadi ilipopata uhuru wake tarehe 9 Desemba, 1961. Zanzibar ilikuwa chini ya utawala wa Kisultani kutoka Oman kuanzia mwaka 1840 hadi 1890, kisha ikatawaliwa na Waingereza kuanzia mwaka 1890 hadi 1963. Baada ya harakati za kutafuta uhuru,Waingereza walikabidhi uhuru wa Zanzibar kwa vyama vya ZNP na ZPPP

FOR ONLINE READING ONLY

chini ya Sultani Jamshid bin Abdullah Al Said tarehe 10 Desemba, 1963. Waziri Mkuu wa Serikali ya Sultani aliitwa Mohamed Shamte kutoka ZPPP. Hata hivyo, harakati za ukombozi wa Waafrika walio wengi zilifanikiwa kupitia Mapinduzi Matukufu ya tarehe 12 Januari, 1964. Hivyo, ilikuwa ni jukumu muhimu kwa wananchi wa Tanganyika na Zanzibar kuanzisha harakati za kuudai uhuru na kujikomboa kutoka katika ukoloni wa Kisultani na Kiingereza.

## Misingi ya kudai uhuru wa Tanganyika na Zanzibar

Harakati za kudai uhuru wa Tanganyika na Zanzibar zilianza mara tu baada ya kuanzishwa kwa serikali za kikoloni. Watanzania wengi hawakupendezwa na tawala za kikoloni na hivyo wakaanzisha mapambano na harakati za kupinga tawala hizo. Zipo sababu kadhaa zilizowafanya Watanzania kuanzisha harakati za kudai uhuru wao. Hii ni pamoja na kuupinga unyonyaji wa mali na rasilimali za wananchi, sera za kibaguzi na za kinyonyaji za wakoloni, ukandamizaji wa Waafrika, kuzilinda mila na desturi dhidi ya tamaduni za kigeni na kutaka kuishi kwa amani katika taifa huru linaloongozwa na viongozi wa Kitanzania. Sababu hizi zinafafanuliwa zaidi katika sehemu zifuatazo:

**Unyonyaji wa mali na rasilimali:** Mfumo wa kikoloni ulikuwa wa kinyanyasaji na kinyonyaji. Watanzania walinyonywa katika nchi yao. Mathalani, walifanya kazi maeneo mbalimbali kama vile mashambani, migodini na sehemu nyingine za nchi bila kupata ujira unaostahili. Pia, mfumo wa kikoloni uliwalazimisha wananchi kulima mazao yaliyoletwa na wakoloni kwa ajili ya viwanda vyao vilivyopo Ulaya. Sera za kikoloni zilizokuwa za kinyonyaji zilisababisha Watanzania kuachana na malengo ya kufanya kazi kwa ajili ya kuzalisha mazao yaliyoletwa na wakoloni. Hali hii ilijenga msingi mmojawapo katika harakati za kudai uhuru wa Tanganyika na Zanzibar.

**Sera za kibaguzi:** Katika kipindi cha ukoloni, sera mbalimbali za kibaguzi zilianzishwa kupitia huduma za jamii na ajira. Kwa mfano, wananchi walibaguliwa katika kupata huduma za kijamii kama vile; afya, elimu na makazi. Wazungu, Waarabu na Waasia walipewa huduma bora wakati Waafrika wakipewa huduma duni au kutokupewa kabisa. Vilevile, kulikuwa na ubaguzi katika kupata ajira zenye hadhi. Kwa ujumla, Waafrika walipewa kazi za usaidizi na zile za ngazi ya chini sana zilizosababisha kulipwa ujira mdogo usioendana na uzito wa kazi walizokuwa wakifanya. Hali hii ilisababisha baadhi ya wananchi kususia bidhaa za kikoloni kama njia ya kupinga sera za kibaguzi za wakoloni.

**Ukandamizwaji wa Waafrika:** Wakoloni walipofika walianza kupora ardhi nzuri ya uzalishaji mali kutoka kwa wenyeji. Hivyo, ili watu waweze kuishi, iliwalazimu kufanya kazi katika mashamba ya wakoloni kwa ujira mdogo na wakati mwingine bila malipo. Pia, serikali za kikoloni ziliwatoza kodi wananchi kwa nguvu na kuwafanyisha kazi katika mashamba yao kwa ujira mdogo. Vilevile, katika maeneo mengine,

FOR ONLINE READING ONLY

Watanzania walilazimishwa kujenga miundombinu mbalimbali. Kwa mfano, watu walijenga reli ya kati na Tanga, 1893-1911, kwa lazima na kuchapwa viboko pale walipogoma kufanya kazi. Watu walilazimika kufanya kazi hata pale walipokuwa wamechoka. Hali hii iliwakasirisha sana Watanzania.

**Kudhihakiwa kwa mila na desturi za Watanzania:** Wakoloni kupitia Wamisionari walipiga marufuku mila na desturi za Kiafrika. Kwa mfano, majina ya Kiafrika yalionekana ni ya "kishenzi" na vilevile dini za jadi zilionekana ni za "kishenzi". Baadhi ya vyakula, nguo, lugha na sanaa vilipigwa marufuku. Badala yake walitilia mkazo matumizi ya utamaduni wa kigeni. Dini za Ukristo na Uislamu zikawa ni alama ya ustaarabu kwa Waafrika waliozifuata imani hizi. Hali hii iliwakasirisha wanajamii na hivyo hawakuwa tayari kuona mila na desturi zao zikidharaulika. Kwa mfano, moja ya sababu za kuibuka kwa vita vya Maji Maji katika eneo la Songea ni kudhihakiwa na kuchomwa moto kwa eneo la ibada za jadi za jamii ya Wangoni huko Maposeni karibu na Peramiho. Kitendo hicho kilisababisha kuuawa kwa padri mwenye asili ya Ujerumani aliyeitwa Franciscus Leuthner pamoja na kuvunjwa kwa kanisa katika eneo la Peramiho tarehe 10 Septemba mwaka 1905.

**Kuongozwa na wakoloni:** Wakoloni walitaka kutawala Tanganyika na Zanzibar kwa muda mrefu. Hivyo, mifumo ya kiutawala haikutoa nafasi kwa Waafrika kuendelea na utamaduni wao wa kuongozwa na viongozi wao wa jadi. Utawala wa kikoloni ulidhihirisha kupotea kwa uhuru wa Watanzania kwani hawakuwa huru. Hata pale viongozi wao wa jadi walipokuwa wakitawala kupitia mfumo wa uwakala. Hata hivyo, uamuzi wote ulitolewa na wakoloni kupitia gavana au wasaidizi wake kama wakuu wa mikoa (*provincial commissioners*) au wakuu wa wilaya (*district commissioners*). Mambo haya yaliwaudhi sana wananchi na kuamua kutafuta uhuru wao uliopotea. Mbaya zaidi hata pale wakoloni walipotakiwa kuwaandaa Watanganyika na Wazanzibari kujitawala, wao waliendelea kuwatawala kwa manufaa yao. Kwa mfano, Umoja wa Mataifa uliwapa Waingereza jukumu la kuisimamia na kuiandaa Tanganyika kujitawala baada ya Vita Kuu ya Kwanza ya Dunia, badala yake hawakuwa na mpango wa kuondoka na kutoa uhuru kwa Watanganyika. Hivyo, waliendelea kujiimarisha kisiasa, kiuchumi na kiutamaduni ili kuendelea kuitawala Tanganyika kwa manufaa ya taifa lao la Uingereza. Hivyo, hali hii iliwakasirisha Watanganyika na kuamua kuanzisha harakati za kudai uhuru.

FOR ONLINE READING ONLY

**Kazi ya kufanya 4.1**

Soma matini kutoka vyanzo mbalimbali ikiwemo mitandao ili kubainisha misingi mingine ya kudai uhuru wa Tanganyika na Zanzibar.

## Zoezi la 4.1

1. Kwa kutumia mifano, eleza maana ya harakati za kupigania uhuru.
2. Kwa nini wananchi wa Tanganyika na Zanzibar walianzisha harakati za kudai uhuru?
3. Eleza kwa nini wakoloni walitumia sera za unyonyaji na ubaguzi wakati wanatawala Tanganyika.
4. Tofautisha maadili ya kikoloni na yale ya jamii za Kitanzania wakati ukoloni unaingia Tanganyika.
5. Je, ni athari gani zilizotokea kutokana na kudharauliwa kwa mila na desturi za jamii za Kitanzania?

### Mbinu zilizotumika kudai uhuru wa Tanganyika na Zanzibar

Kuna vipindi viwili muhimu vya harakati za wananchi katika kudai uhuru wa Tanganyika na Zanzibar. Kipindi cha kwanza kilikuwa kati ya mwaka 1900 hadi 1944. Katika kipindi hicho, harakati ziliendeshwa na vikundi na vyama vya kijamii na kidini (hasa kwa upande wa Tanganyika) katika maeneo machache tu. Kipindi cha pili cha harakati hizi kilikuwa kati ya mwaka 1945 na 1964, ambapo harakati za kudai uhuru zilikuwa na nguvu zaidi zikiendeshwa na vyama vya siasa. Katika kipindi hiki, harakati hizo zilisambaa nchi nzima kutokana na mabadiliko yaliyotokana na mchango wa Vita Kuu ya Pili ya Dunia (1939 – 1945).

Harakati za kudai uhuru wa Tanganyika na Zanzibar zilitumia mbinu mbalimbali, ikiwa ni pamoja na kuanzisha jumuiya, vyama na taasisi za kijamii za Waafrika. Malengo ya kuanzishwa kwa jumuiya, vyama na taasisi hizo yalikuwa ni kutetea na kudai haki za wafanyakazi, wakulima na wafanyabiashara. Kadiri muda ulivyoendelea, jumuiya, vyama na taasisi hizo zilijihusisha na siasa na kuchangia sana katika harakati za kudai uhuru wa Tanganyika na Zanzibar.

### Vyama vya ushirika na wakulima

Chama cha ushirika ni muungano wa watu waliokubaliana kuendesha shughuli zao za kiuchumi kwa pamoja ili kuinua hali zao za maisha. Shughuli hizi ni kama vile kutafuta mahitaji yao ya chakula, elimu, uuzaji wa mazao yao na shughuli nyingine za uchumi zinazoweza kuendeshwa kwa pamoja. Hata hivyo, jambo la muhimu ni kuhakikisha kuwa watu hao wana mahitaji yanayofanana ya kupata huduma ya shughuli yoyote ya kiuchumi iliyowafanya waanzishe chama.

Vyama vya wakulima vilianzishwa na wakulima wenyewe katika maeneo ambapo mazao ya biashara yalilimwa. Vyama hivi vilijulikana kama vyama vya ushirika katika sehemu mbalimbali za Tanganyika na Zanzibar. Baadhi ya malengo ya kuanzishwa kwa vyama hivi yalikuwa ni pamoja na kudai bei nzuri ya mazao yao, kupata

FOR ONLINE READING ONLY

masoko ya uhakika, kudai kupewa pembejeo na zana za kilimo, kupinga unyonyaji, kunyang'anywa ardhi na kutozwa kodi kubwa ya mazao yao. Mfano wa vyama hivi vya wakulima ni: *Bukoba Buhaya Union* (1924), *Kilimanjaro Native Planters Association* (1925), *Meru Citizens' Union* (1930), *Sukuma Union* (1930), Chama cha Waluguru cha *African Cotton Planters Association* (1934), *Nyakyusa Union* (1937), *Buhaya Farmers' Association* (1937) na *Pare Union* (1949).

Kwa upande wa Zanzibar, kulikuwa na jumuiya mbalimbali zilizoundwa na makundi ya wakulima kwa malengo kama hayo ya wenzao kutoka Tanganyika. Kwa mfano, Chama cha Wananchi wa Zanzibar cha Raia wa Sultani kilichojulikana kwa Kiarabu kama *Hizbu l'Watan l'Riaia Sultan Zanzibar*, kwa kifupi HIZBU, kiliundwa na wakulima wa Kiembe Samaki baada ya Vita ya Ng'ombe (*Cattle Riot*) mwaka 1951. Hata hivyo chama, pamoja na kuanzishwa na wakulima wa Kiembe Samaki, hakikuanzishwa kama chama cha ushirika bali kama umoja wa wakulima.

Mbinu hii ya kuanzisha vyama vya ushirika haikuchangia tu kudai haki za wakulima, bali pia ilichangia kwa kiasi kikubwa kuanzishwa kwa Sheria ya Ushirika nchini Tanganyika mnamo mwaka 1932. Vyama hivi vilitoa watu mbalimbali ambao baadaye walikuja kuwa viongozi wa kisiasa, kama Paul Bomani na Clement George Kahama. Vilevile, vyama hivi vilipinga uamuzi wa serikali ya kikoloni ambao ulikuwa unawakandamiza Watanganyika na Wazanzibari. Kwa mfano, vyama vya wakulima wa Tanganyika vilipoungana na kukataa mapendekezo ya walowezi wa Kenya ya kuanzisha shirikisho la Afrika Mashariki, ambalo lingewawezesha uhuru wa kutumia ardhi na masoko katika nchi yoyote ya shirikisho hilo.

Vyama hivi vilichangia kwa kutoa fedha kwa TANU, kuunganisha na kuhamasisha watu katika harakati za kupigania uhuru wa Tanganyika. Pia, vyama vya ushirika vilitoa elimu ya demokrasia kwa wanachama wao na kuwakumbusha umuhimu wa kujikomboa kutoka mikononi mwa utawala wa kikoloni. Hivyo, pamoja na kudai haki za wakulima, vilitumika kama mbinu ya kificho kudai haki za kisiasa, hasa wakati wa harakati za kudai uhuru. Kielelezo 4.1 kinaonyesha picha ya George Kahama na Paul Bomani, ambao walikuwa miongoni mwa viongozi wa vyama vya ushirika Tanganyika.





**Kielelezo 4.1:** *Clement George Kahama (kushoto) na Paul Bomani (kulia)*

FOR ONLINE READING ONLY

**Vyama vya wafanyakazi**

Waafrika waliokuwa wameajiriwa katika viwanda, mashamba, bandari na sehemu nyingine walianzisha vyama vyao vya wafanyakazi kwa lengo la kulinda na kutetea masilahi yao ya kikazi. Malengo hayo yalijumuisha kudai kulipwa mishahara kwa wakati, ujira unaostahili na mazingira bora ya kazi. Madai mengine yalikuwa ni kupinga ubaguzi na unyanyasaji kazini, kupunguza masaa au muda wa kazi na kupinga kodi za kinyonyaji.

Mfano wa vyama hivyo ni *Tanganyika Territory Civil Servants' Association* (TTCSA), kilichoanzishwa na Martin Kayamba mwaka 1922 huko Tanga, ambacho mwaka 1924 kilifungua tawi lake mjini Dar es Salaam. Pia, ndani ya kipindi hicho cha mwaka 1922 wafanyakazi wa serikali wa Dar es Salaam walianzisha *Tanganyika African Government Servants Association* (TAGSA). Vyama vingine vilivyoundwa ni pamoja na *Association of Cooks and Washmen* (1939), *Dock Workers' Union* (1937), *Railway African Civil Service Union* (1920) na *Tanganyika Federation of Labour* (1955) chini ya uongozi wa Rashid Mfaume Kawawa. Kielelezo 4.2 kinaonesha picha ya Rashid Mfaume Kawawa.



**Kielelezo 4.2:** *Rashid Mfaume Kawawa*

Kwa upande wa Zanzibar, mnamo mwaka 1939, *Sheikh* Abeid Amani Karume aliunda Jumuiya ya Mabaharia kwa ajili ya kupigania haki za wafanyakazi katika vyombo vya baharini. Ambapo mwaka 1941, Jumuiya ya Mabaharia, Jumuiya ya Wachukuzi na Umoja wa Watumishi wa Nyumba za Wazungu walikutana kujadili mikakati ya ukombozi dhidi ya unyonyaji kazini. Baadaye, mwaka 1948, Chama cha Masonara, Chama cha Wafanyakazi wa Hospitali na Chama cha Mafundi wa Majahazi pia vilikutana kwa lengo la kujadili namna ya kutetea masilahi yao katika sehemu za kazi.

Aidha, Baraza la Umoja wa Vijana wa Kiafrika (*Youth African Council Union*) liliundwa mwaka 1949. Baraza hili lilianzishwa kwa madhumuni ya kupigania haki ya kupata kazi na mishahara inayolingana na elimu na ujuzi wa mtu. Hata hivyo, mnamo mwaka 1956, Muungano wa Vyama vya Wafanyakazi wa Zanzibar na Pemba (*Federation of Zanzibar and Pemba Trade Unions* - ZPFL) ulianzishwa.

Pamoja na juhudi zao za kutetea masilahi ya wafanyakazi, waliendelea kujadili masuala ya kisiasa na hatimaye walijihusisha na harakati za kudai uhuru.

FOR ONLINE READING ONLY

**Kazi ya kufanya 4.2**

Chagua chama kimojawapo cha ushirika au wafanyakazi kilichoshiriki harakati za kudai uhuru wa Tanganyika na Zanzibar, kisha soma matini mbalimbali kupitia mtandao kuhusu chama hicho na andika maelezo yenye kurasa 2 kuhusu historia na mchango wake katika harakati za kudai uhuru

## Vyama vya wafanyabiashara

Vyama vya wafanyabiashara wa Kiafrika vilianzishwa nchini Tanganyika ili kuyalinda na kuyatetea masilahi ya wafanyabiashara wa Kiafrika dhidi ya wafanyabiashara wa kigeni. Baadhi ya madai yao yalijumuisha kupinga ubaguzi na unyanyasaji katika masoko, kupinga kodi kubwa iliyokuwa ikitozwa na kuboresha mazingira ya kufanyia biashara. Mfano wa vyama hivi ni *African Commercial Association* kilichoanzishwa mwaka 1934 chini ya Erica Fiah. Hata hivyo, Fiah alikibadilisha chama hiki na kukifanya *Tanganyika African Welfare and Commercial Association* mwaka 1936, kisha kuanzishwa tena kama *African Retail Traders' Association* mwaka 1937.

Kwa upande wa Zanzibar, kulikuwa na jumuiya mbalimbali za Wahindi, Waarabu na Waafrika zilizoundwa ili kutetea masilahi yao ya kifedha na kibiashara. Mfano wa jumuiya hizo ni Jumuiya ya Wahindi iliyoundwa mwaka 1910, ambayo ilianzishwa ili kupambana na Waarabu waliokuwa wanadaiwa fedha nyingi na Wahindi baada ya kufilisika kutokana na kufutwa kwa biashara ya utumwa Zanzibar. Pamoja na madai haya, kulikuwa na harakati za chini kwa chini kuhusu masuala ya kisiasa.

Vyama vya kijamii viliendelea kukua mwaka hadi mwaka nchini Tanganyika na Zanzibar na vilianzishwa vyama vyenye lengo la kuwaunganisha watu wa maeneo na sekta mbalimbali. Mfano wa vyama hivi ni *Tanganyika African Association* (TAA), kilichoanzishwa mjini Dar es Salaam mwaka 1929. Chama cha TAA kiliundwa na watumishi wa serikali na baadaye kikazaa chama cha siasa kiitwacho TANU. Rais wake wa kwanza alikuwa Cecil Matola na katibu wake alikuwa Abdulwahid Kleist Sykes. Kufikia mwaka 1948, TAA kilikuwa na matawi makuu Dar es Salaam na Dodoma. Zanzibar kulikuwa na *African Association* na *Shirazi Association*. Jumuiya hizi mbili zilizoundwa Zanzibar zilikuja kuungana na kuunda chama cha

FOR ONLINE READING ONLY

ukombozi cha *Afro-Shirazi Party* (ASP) ambacho pia ndicho kilichoungana na TANU kuunda Chama Cha Mapinduzi mwaka 1977.

Pamoja na kutetea haki na masilahi ya wafanyabiashara, vyama hivi vilikuja kushiriki katika harakati za kudai uhuru, ikiwa ni pamoja na baadhi yao kubadilika na kuwa vyama vya kisiasa. Kielelezo 4.3 kinaonesha picha ya Abdulwahid Kleist Sykes.



**Kielelezo 4.3**: *Abdulwahid Kleist Sykes*

FOR ONLINE READING ONLY

### Vikundi na vyama vya kidini

Dini za Kikristo na Kiislamu zilitumika kama vyombo vya kuwaunganisha watu na kuendeleza harakati za kudai uhuru wa Tanganyika na Zanzibari. Vyama na vikundi vya kidini vya Waafrika vilianzishwa kwa lengo la kupigania haki, usawa na uhuru wa kuabudu, pamoja na kudumisha utamaduni wa Watanganyika na Wazanzibari. Miongoni mwa vikundi na vyama vya kidini vilivyoanzishwa nchini Tanganyika ni *Al-Jamiatul Islamiyya fi Tanganyika* (1933), *The Watch Tower Church, The African National Church* na *The Church of God*.

*Al-Jamiatul Islamiyya fi Tanganyika* ilitoa viongozi shupavu kama Ally Sykes, Bibi Titi Mohamed, Tewa Said Tewa na wazalendo wengine ambao baadaye walishirikiana na Mwalimu Julius Kambarage Nyerere katika harakati za kudai uhuru wa Tanganyika. Kwa upande wa Zanzibar, kulikuwa na Jumuiya iliyoitwa *Jamiyatu Shubbaniul Muslimin*, iliyoanzishwa tarehe 25 Novemba 1935 huko Gulioni, Unguja na *Sheikh* Salim Bin Abdullah Al Wadan (1901 - 1941), kwa lengo la kupinga mila na desturi za Kizungu.

### Vilabu vya mpira wa miguu

Vilabu vya mpira wa miguu vya Waafrika vilianzishwa na kusaidia kuimarisha umoja na mshikamano miongoni mwa Waafrika sambamba na kueneza fikra za ukombozi dhidi ya madhila ya ukoloni. Vilabu hivyo viliweza kuonesha ushindani mkubwa dhidi ya vilabu vilivyosimamiwa na wakoloni na hivyo kuamsha ari kwa Waafrika ya kupambania haki zao za kijamii, kiuchumi na kisiasa. Mwaka 1931 ilianzishwa klabu ya mpira wa miguu Zanzibar kwa jina la *The African Sports Club* ambayo kiongozi wake alikuwa *Sheikh* Abeid Amani Karume. Aidha, Klabu hii ilikuwa msingi wa kuanzishwa kwa Jumuiya ya Waafrika (*African Association*) mwaka 1933 ambayo iliwaunganisha Waafrika wa Unguja na Pemba kudai haki zao mbalimbali.

Kwa upande wa Tanganyika, mnamo mwaka 1935 ilianzishwa Klabu ya Waafrika yenye jina la *Young African Sports Club* ambayo pamoja na kushiriki mashindano ya mpira wa miguu ilikuwa na lengo la kuwaunganisha Waafrika kujadili masilahi yao, matatizo yao na kuimarisha ushirikiano katika utatuzi wa changamoto mbalimbali. Aidha, vilabu hivi vilichangia kwa kiasi kikubwa kuhamasisha wananchi kujiunga na Jumuiya za Waafrika kama vile; *African Association*, *Shirazi Association* na TAA na baada ya jumuiya hizo kuwa vyama vya kupigania uhuru. Pia, vilabu hivi vilitoa mchango mkubwa wa kuchangisha fedha kwa wanachama wao pamoja na kuwahamasisha kujiunga na vyama vya TANU na ASP.

**Kazi ya kufanya 4.3**

Soma matini kutoka vyanzo mbalimbali ikiwemo mitandao, kisha fafanua jinsi vikundi na vyama vya kidini vilivyochangia katika harakati za kudai uhuru wa Tanganyika na Zanzibar.

**Vyombo vya habari**

Kuanzishwa kwa vyombo vya habari katika Tanganyika na Zanzibar kuliongeza na kuimarisha harakati za Waafrika katika kupigania uhuru wao. Kabla ya kuanzishwa kwa vyombo hivi vya Waafrika, kulikuwepo vyombo vya habari vilivyokuwa vimeanzishwa na serikali ya kikoloni. Hata hivyo, vyombo hivyo vya kikoloni havikutoa habari kuhusu harakati za kudai uhuru wa Tanganyika na Zanzibar, bali vilijikita zaidi katika kuwasifia wakoloni na kuelezea matukio ya huko Ulaya.

Kutokana na changamoto hii, Waafrika wakaona kuwa kuna umuhimu wa kuunda na kuanzisha vyombo vya habari vyao wenyewe. Mfano wa vyombo hivyo ni gazeti la Kwetu, lililoanzishwa na jumuiya ya *African Association* (AA) mwaka 1937 na Sauti ya TANU, ambalo lilihaririwa na Mwalimu Julius Kambarage Nyerere mwaka 1957. Kazi hii ya uhariri ilimletea matatizo Mwalimu Julius Kambarage Nyerere baada ya kuchapisha taarifa ambayo haikuupendeza utawala wa Waingereza. Hivyo, mnamo tarehe 9 Julai 1958, Julius Kambarage Nyerere alishtakiwa katika Mahakama ya Dar es Salaam kwa makosa ya uchochezi dhidi ya serikali ya kikoloni. Tarehe 12 Agosti 1958, Mwalimu Nyerere alihukumiwa kulipa faini ya shilingi elfu tatu, sawa na paundi 150 za Uingereza, au kwenda jela miezi sita kama angeshindwa kulipa. Wanachama na wapenzi wa TANU walichanga fedha na kumsaidia kulipa faini hiyo ili kumnusuru Mwalimu Nyerere asitumikie kifungo cha jela.

FOR ONLINE READING ONLY

Kwa upande wa Zanzibar, kulikuwepo na vyombo vya habari kama magazeti na majarida mbalimbali, kwa mfano, gazeti la Sauti ya Zanzibar (1949), gazeti la Samachar lililoandikwa na Bwana Mtoro bin Abu Rehan, jarida la *African Events* na *Alfalaq* (1929) lililoandikwa na Ahmed Yahya Aldarda. Magazeti mengine ni Afrika Kwetu, Muongozo, Jasho Letu, Mkombozi, Mwiba, Sauti ya Afro-Shirazi, Sauti ya Jogoo na Umma.

Vyombo vya habari vya Waafrika vililenga kuamsha ari ya uzalendo kwa Watanganyika na Wazanzibari ili kuwaunganisha katika kudai uhuru wao. Vilikuwa na jukumu la kutoa elimu ya uzalendo na kuwaelimisha wananchi kuhusu sera na itikadi za vyama kama TANU na ASP. Aidha, vilitumika kuhamasisha na kupaza sauti dhidi ya maovu yaliyokuwa yakifanywa na serikali za kikoloni. Kielelezo 4.4 kinaonesha mojawapo ya ukurasa wa mbele wa gazeti la Sauti ya TANU.


THE TANGANYIKA AFRICAN NATIONAL UNIT

SAUTI YA TANU

No.3 16th March, 1957

During the past few weeks, the government and the press have been very busy criticising TANU and its activities. While we welcome fair and constructive criticism, we cannot accept deliberate or well-calculated ant-TANU activities.

Recent events lead us to believe that it is the intention of certain elements in the territory, not only to discourage African political aspirations but wipe out TANU completely.



Our Korogwe branch has been rendered out of nation and our President muzzled. One wonders what the future has for us in store. But let me say this, that ant-TANU activities or unhealthy press will not stop us from demanding our rights or achieving our objects. Besides, this will not solve' our political problems here, it will only set the clock back. What we need and deserve is a Government that has the imagination to pursue a policy that will load our country to nationhood without bitterness.

**Kielelezo 4.4:** *Gazeti la Sauti ya TANU*

**Vikundi na vyama vya sanaa**

Wakati wa utawala wa kikoloni, hakukuwa na nafasi ya kutosha kwa Watanganyika na Wazanzibari kusimama na kujieleza kwa uhuru kuhusu haki zao na harakati za ukombozi. Badala yake, mambo mengi ya harakati za Watanganyika na Wazanzibari kudai uhuru yalifanyika kwa siri kuhofia adhabu kutoka kwa wakoloni. Viongozi na wanachama wa TANU na ASP waliamua kutumia sanaa na michezo kama mbinu mbadala.



**Kielelezo 4.5**: *Bibi Titi Mohamed akiwa jukwaani*

Sanaa ilitumika katika kukuza na kuendeleza harakati za kudai uhuru wa Tanganyika na Zanzibar. Watanganyika walianzisha vikundi na vyama vya sanaa

FOR ONLINE READING ONLY

na michezo kama vile kikundi cha taarabu cha Jipisheni. Kikundi hicho baadaye kilipewa jina la *Egyptian Music Club*. Kikundi kingine cha taarabu kilikuwa ni *Al-Watan*. Pamoja na taarabu kulikuwa vikundi vya lelemama ambavyo vilikuwa na udugu na vikundi vya taarabu vya *Al-Watan* au *Egyptian*. Vikundi vyote hivi vilitoa mchango mkubwa sana katika kuhamasisha watu kuiunga mkono TANU. Waliounganisha na kuviongoza vyama hivi vya wanawake na harakati za kudai uhuru walikuwa Bibi Titi Mohamed na Bibi Hawa binti Maftah. Kielelezo 4.5 kinaonesha picha ya Bibi Titi Mohamed akiwa jukwaani.

Kulikuwa pia na vyama vya wanawake kama *Nujum ul Azhar* na *Egyptian Club* vilivyokuwepo mjini Tabora. Vyama hivi viliongozwa na wanawake kama Nyange binti Chande na Zarura binti Abdulrahman na vilichangia sana kuipa TANU nguvu katika Jimbo la Magharibi. Muziki na ujumbe uliokuwa katika nyimbo zilizotungwa maalumu kwa ajili ya kuamsha ari ya wanachama wa TANU vilikuwa na athari kubwa, hasa wakati ambapo serikali ya kikoloni ilimpiga marufuku Mwalimu Nyerere kufanya mikutano ya hadhara.

Ili kukwepa marufuku hiyo, TANU iliandaa hafla za taarabu na Mwalimu Nyerere alikuwa akikaribishwa kama mgeni rasmi. Mwalimu Nyerere alisimama kufungua hafla hizo na, kwa kufanya hivyo, alisema maneno machache kuhusu harakati za kudai uhuru. Kwa njia hii, ari ya kudai uhuru iliendelea kuwaka na Mwalimu Nyerere aliweza kuwasiliana na wananchi. Vilevile, kupitia taarabu, TANU ilikusanya fedha kwa ajili ya kuendeleza harakati za ukombozi.

## Zoezi la 4.2

1. Je, ni kwa namna gani mbinu ya kuanzisha vyama vya kiraia ilisaidia harakati za kupigania uhuru wa Tanganyika na Zanzibar?
2. Jadili nafasi ya vyombo vya habari katika harakati za kisiasa wakati wa sasa.
3. Fafanua nafasi ya vijana katika kudumisha uhuru wa Tanganyika na Zanzibar.
4. Eleza mchango wa vikundi na vyama vya kijamii na kidini katika kukukuza demokrasia wakati wa sasa.
5. Pendekeza mikakati ya kudumisha uhuru wa Tanganyika na Zanzibar.

FOR ONLINE READING ONLY

**Vyama vya siasa**

Umoja wa Waafrika ulioitwa *African Association* (AA) uliundwa mwaka 1929 na mnamo mwaka 1948 ulipewa jina jipya la *Tanganyika African Association* (TAA). Mwaka 1954, chama hiki kilibadilishwa jina tena na kuwa chama rasmi cha siasa kwa jina la TANU.

Chama cha TANU kilikuwa na malengo mengi na baadhi ya malengo hayo yalikuwa ni pamoja na kuwaunganisha wananchi wa Tanganyika na kuwaongoza katika mapambano ya kupigania uhuru wa nchi yao, kutoa tafsiri mpya ya ukombozi, kuweka juhudi na fikra mpya za mapambano kwa misingi ya kifalsafa, pamoja na kudai haki ya kuwa na wawakilishi wa kidemokrasia katika vyombo vya kutunga sheria.

Mbali na chama cha TANU, kulikuwa na vyama vingine vya kisiasa wakati wa harakati za kupigania uhuru. Mfano wa vyama hivyo ni *United Tanganyika Party* (UTP) kilichoanzishwa mwaka 1956, ambacho kiliungwa mkono na Wazungu, Waasia na baadhi ya Waafrika, hasa machifu. Vyama vingine ni *African National Congress* (ANC), kilichojitenga kutoka TANU mwaka 1958 na kuongozwa na Zuberi Mtemvu. ANC ilipingana na TANU katika harakati za kudai uhuru wa Tanganyika, hasa katika suala la kupiga kura tatu ambalo mwalimu Nyerere na wanachama wengine wenye msimamo wa kati walilikubali, huku Zuberi Mtemvu na wanachama wengine wenye msimamo mkali walilikataa na kuamua kujitenga. Pia, chama cha *All Muslim National Union of Tanganyika* (AMNUT) kilikuwa chama cha nne kuanzishwa Tanganyika. Kama ilivyokuwa TANU, AMNUT pia kilidai uhuru lakini walitaka mabadiliko ya katiba na uhuru viletwe polepole na si haraka kama TANU ilivyotaka. Mpaka wakati wa uhuru, Tanganyika ilikuwa na vyama hivi vinne.

Kwa upande wa Zanzibar, vyama vilivyojitokeza kudai uhuru ni pamoja na *Zanzibar Nationalist Party* (ZNP) kilichoanzishwa mwaka 1955, *Afro-Shirazi Party* (ASP) kilichoanzishwa mwaka 1957 na *Zanzibar and Pemba People's Party* (ZPPP) lililoundwa mwaka 1959. Vyama vyote hivi vilikuwa na lengo kuu la kudai uhuru wa Wazanzibari, ingawa viliungwa mkono na wanachama wa rangi tofauti.

Chama cha ASP kiliundwa baada ya kuunganishwa kwa vyama viwili vilivyokuwepo hapo awali, yaani *African Association* na *Shirazi Association*. Baada ya kuundwa kwa chama cha ASP, *Sheikh* Abeid Amani Karume alichaguliwa kuwa Rais wa ASP, Mtoro Rehani Kingo alichaguliwa kuwa Makamu wa Rais na Thabiti Kombo Jecha alichaguliwa kuwa Katibu Mkuu. Kielelezo 4.6 kinaonesha picha ya Thabit Kombo Jecha.



**Kielelezo 4.6**: *Thabit Kombo Jecha*

FOR ONLINE READING ONLY

Chama cha ASP kilikuwa na malengo mengi, yakiwemo kupigania uhuru wa Zanzibar, kuunda serikali ya kidemokrasia katika visiwa vya Unguja na Pemba, kuondoa ubaguzi wa aina yoyote katika visiwa hivyo, kudumisha uhuru wa Zanzibar na watu wake, pamoja na kuwaandaa wananchi wawe tayari kupigania uhuru wao.

Vyama vya siasa, hasa TANU kwa Tanganyika na ASP kwa Zanzibar, vilikuwa na mchango muhimu katika kukuza harakati za kupigania uhuru wa nchi hizo. Kwa namna moja ama nyingine, vyama hivi viliunganisha wananchi na kuwaongoza katika mapambano ya kuudai uhuru. Vilihamasisha wananchi kujiunga navyo na kushiriki katika harakati za kuudai uhuru wa nchi zao. Viongozi wa TANU na ASP walitangaza falsafa na sera za vyama hivyo kwa wanachama na wananchi wote kwa ujumla. Pia, vyama hivi viliandaa mikutano ya kisiasa na kuhamasisha wanachama pamoja na wananchi kuhudhuria mikutano hiyo.

Aidha, vyama vya siasa vilianzisha matawi katika maeneo mbalimbali ya nchi ili kuvutia wanachama wengi zaidi. Vyama hivi vilitoa elimu na mafunzo ya kiuongozi na kisiasa kwa viongozi wa matawi na ngazi ya kitaifa. Katika chaguzi mbalimbali zilizofanyika kabla ya uhuru, vyama vya siasa vilishiriki na baadhi ya vyama vilifanikiwa kupata wawakilishi katika Baraza la Kutunga Sheria. Ni muhimu pia kufahamu kuwa, vyama kadhaa, hasa TANU na ASP, vilianzisha vyombo vya habari ili kuendeleza harakati za kudai uhuru. Kwa mfano, TANU kilianzisha gazeti lililoitwa 'Sauti ya TANU' na ASP kilianzisha 'Sauti ya ASP.' Hivyo basi, ni dhahiri kuwa vyama vya siasa vilichochea kukua kwa harakati za kudai uhuru wa Tanganyika na Zanzibar. Hata hivyo, vyama hivyo vilikabiliana na changamoto nyingi, ikiwemo upinzani mkali kutoka kwa serikali ya kikoloni. Kielelezo 4.7 kinaonyesha picha ya Mwalimu Nyerere akiwa na mawakili wake wakielekea mahakamani kujibu kesi ya uchochezi.



**Kielelezo 4.7:** *Mwalimu Nyerere akiwa na mawakili wakielekea mahakamani*

FOR ONLINE READING ONLY

**Kazi ya kufanya 4.4**

Tafuta taarifa kutoka vyanzo mbalimbali ikiwemo mtandao na bainisha mbinu nyingine zilizotumika katika harakati za kuudai uhuru wa Tanganyika na Zanzibar.

**Zoezi la 4.3**

1. Unafikiri ni kwa nini serikali za kikoloni ziliwazuia Waafrika kuanzisha vyama vya kisiasa?
2. Je, unafikiri ni kwa nini vyama vya kiraia vilivyoanzishwa wakati wa harakati za kudai uhuru vilibadilika na kuanza kujihusisha na siasa?
3. Eleza mchango wa vyama vya siasa katika harakati za kudai uhuru wa Tanganyika na Zanzibar.
4. Fafanua mafanikio na changamoto zinazokabili vyama vya siasa kwa sasa.
5. Eleza wajibu wa vyama vya siasa katika kuikuza demokrasia nchini.

## Mchango wa harakati za kupinga uvamizi na ukoloni

Mchango wa harakati za kupinga uvamizi na ukoloni ulikuwa ni pamoja na kutunza maadili na kujenga uzalendo.

### Kutunza maadili

Ujenzi wa maadili ni mchakato wa kihistoria kwa kuwa unatokana na hisia ambazo watu au jamii wamezikuza kwa miaka mingi kama sehemu ya harakati zao za kuleta maendeleo na uhuru katika jamii au nchi yao. Maadili ni muhimu kutunzwa kwa kuwa yanaleta fahari, umoja, ujasiri na mienendo inayokubalika katika jamii. Hivyo, harakati za kupinga ukoloni nazo zilichangia katika utunzaji wa utambulisho wa Mtanzania, ambao ni pamoja na umoja, utu, mshikamano na lugha ya Kiswahili.

*Umoja*

Harakati za kupinga uvamizi na mifumo ya kikoloni zilichangia pia katika kudumisha maadili ya umoja miongoni mwa jamii za Kitanzania. Kabla ya ukoloni, jamii za Kitanzania zilikuwa zimegawanyika katika makabila mbalimbali. Kila kabila lilikuwa na utaratibu wake wa maisha, ikiwa ni pamoja na mila na desturi zake. Pia, inapaswa kukumbukwa kuwa wakoloni walikuwa na nguvu kubwa za kijeshi na walimiliki silaha bora zaidi ikilinganishwa na silaha za jadi zilizotumiwa na jamii za Kitanzania wakati huo. Hivyo, viongozi wa jamii mbalimbali za Kitanzania walihimiza umoja miongoni mwa wanajamii ili kuwa na nguvu ya kukabiliana na uvamizi na utawala wa kikoloni. Waliamini kuwa "umoja ni nguvu, utengano ni udhaifu."

Aidha, kuelekea kipindi cha kupata uhuru, kwa mfano, viongozi kama Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, *Sheikh* Abeid Karume na wengineo waliunganisha makabila na jamii mbalimbali. Hali hii, ilisaidia kuendeleza mapambano ya ukombozi kwa pamoja kama jamii moja ya Watanganyika na jamii ya Wazanzibari katika kudumisha

FOR ONLINE READING ONLY

maadili ya umoja yaliyodumu kwa muda mrefu. Maadili haya ya umoja yalikuwa muhimu katika kujenga mshikamano miongoni mwa jamii za Kitanzania. Pia, ilisaidia kudumisha nguvu ya kitaifa, kupinga ukoloni na kudai uhuru wa Tanganyika na Zanzibar. Kwa hivyo, harakati za kupinga uvamizi na utawala wa kikoloni na juhudi za kudai uhuru, zilichangia katika kudumisha maadili ya umoja na nguvu ya kitaifa katika kudai uhuru wa nchi zao.

*Utu*

Uvamizi na utawala wa kikoloni ulikuwa ni wa kimabavu na uliweka mifumo ya kuwanyanyasa, kuwanyonya na kuwakandamiza Watanzania. Hali hii ilitweza utu wao. Pia, Watanzania walidhalilishwa kwa adhabu kali za viboko hadharani pale waliposhindwa kulipa kodi au kufanya makosa mengine. Adhabu hizi zilitolewa kwa kuwavua nguo na kuwachapa mijeledi hadharani, kitendo kilichowachukiza sana wananchi kwa kuwa kilitweza na kudhalilisha utu wao.

Kwa sababu hii, wananchi walipinga na kupambana ili kuonesha hisia zao za kuchoshwa na dhuluma na manyanyaso ya wakoloni. Harakati mbalimbali dhidi ya uvamizi na matendo maovu ya wakoloni zilitokea karibu kila sehemu ya Tanganyika. Ukoloni na mifumo yake iliathiri sana utu wa Waafrika na hivyo kuamsha ari ya kupata uhuru ili kutunza maadili ya utu yaliyokuwa yamejengwa na jamii za asili za Tanganyika na Zanzibar. Kwa hivyo, harakati za kupinga ukoloni pia zilichangia katika utunzaji na udumishaji wa maadili ya utu, kwani Watanzania hawakuwa tayari kuona utu wao au maadili yao yakipotea.

*Mshikamano*

Harakati za kupinga ukoloni na kupigania uhuru wa Tanganyika na Zanzibar zilichangia pia katika kutunza maadili ya mshikamano miongoni mwa jamii za Kitanzania. Wakati wa kupinga uvamizi, viongozi waliwaunganisha watu katika jamii zao ili kuwa na nguvu za kupambana na uvamizi wa wakoloni. Viongozi wa jamii kama vile *Mtwa* Mkwawa wa kabila la Wahehe, *Mangi* Meli wa Old Moshi, *Mtemi* Isike wa Unyanyembe na viongozi wengine walihamasisha watu wao kushikamana ili kukabiliana na uvamizi wa wakoloni wa Kijerumani. Viongozi hawa walitambua kwamba adui yao alikuwa na nguvu za kijeshi. Hivyo, jamii zao zilihitaji mshikamano ili kuweza kupambana na wakoloni hao. Kuyatunza maadili ya mshikamano kuliwawezesha kutoa upinzani mkali kwa wavamizi, ingawa baadaye hawakufanikiwa kutokana na sababu mbalimbali.

Aidha, wakati wa harakati za kudai uhuru wa Tanganyika na Zanzibar, viongozi walihimiza mshikamano wa Watanzania wote ili kuwezesha Tanganyika na Zanzibar kupata uhuru. Katika kuimarisha mshikamano dhidi ya utawala wa Waingereza, wananchi walijiunga katika makundi mbalimbali ya kimasilahi, ambapo wakulima wa mazao makuu ya biashara waliunda vyama vya ushirika kupigania bei nzuri ya

FOR ONLINE READING ONLY

mazao na unafuu wa pembejeo za kilimo. Vyama mashuhuri vilikuwa ni pamoja na Kilimanjaro *Native Cooperative Union* (KNCU), Victoria *Federation of Cooperative Union* (VFCU), *Bukoba Bahaya Union* na Umoja wa Meru. Vyama hivi na vingine vilijenga mshikamano miongoni mwa wananchi na wakati wa harakati za kupigania uhuru, vilitoa mchango mkubwa wa kisiasa na hatimaye kuwa sehemu ya chama cha ukombozi cha *Tanganyika African National Union* (TANU). Hivyo, harakati za kupinga uvamizi wa wakoloni na kupigania uhuru zilichangia katika utunzaji wa maadili ya mshikamano ambayo yanaenziwa na taifa letu hadi sasa.

*Kiswahili*

Harakati za kupinga ukoloni na kupigania uhuru wa Tanganyika na Zanzibar zilitumia lugha ya Kiswahili kwa namna mbalimbali. Mathalani, Kiswahili kilitumika kusaidia kuleta umoja na mshikamano miongoni mwa wanachama wa TANU na ASP pamoja na wananchi wote. Lugha ya Kiswahili pia ilitumika kuwaunganisha wananchi wa Tanganyika na Zanzibar ili kupigania uhuru wa nchi zao. Wananchi wa nchi hizo, licha ya kwamba walitoka katika makabila na jamii tofauti, lugha ya Kiswahili iliwaunganisha na kuwafanya kuwa kitu kimoja katika kupigania nchi zao. Aidha, lugha ya Kiswahili ilisaidia kupeleka ujumbe kwa Watanganyika na Wazanzibari kwani ilitumika na wengi. Mbinu na mikakati iliyotolewa kuhusu uzalendo na ari ya kujitolea kupambana na ukoloni iliwasilishwa kwa kutumia lugha ya Kiswahili. Vilevile, katika harakati za kupambana na ukoloni, nyimbo, hasa taarabu, zilitumia lugha ya Kiswahili kupeleka ujumbe. Vyombo vya habari, kama vile magazeti ya Afrika Kwetu, Mkombozi, Mwiba, Sauti ya Afro-Shirazi, Ukombozi na Sauti ya Jogoo, vilitumia Kiswahili kuelimisha na kutoa habari kwa wananchi kuhusu harakati za kupigania uhuru.

Aidha, sera na itikadi za TANU na ASP zilielezwa kwa lugha rahisi ya Kiswahili, hivyo kurahisisha ufikishaji wa ujumbe kwa wananchi. Viongozi waliamua kutumia lugha ya Kiswahili ili kueneza na kufikisha kwa urahisi sera za vyama vyao kwa wananchi. Wananchi walihamasishwa kutumia Kiswahili katika mawasiliano, jambo lililosaidia kuondoa hali ya ukabila na ubaguzi wakati wa kupigania uhuru. Kiswahili kilikuwa nguzo muhimu katika kufikisha taarifa na habari juu ya harakati za kupigania uhuru na kilisaidia kuwaunganisha wananchi hadi kufikia hatua ya kupatikana kwa uhuru wa Tanganyika na Zanzibar.

**Kujenga uzalendo**

Harakati za kupinga ukoloni zilihusisha kupinga sera na hata kuhusisha kupigana vita dhidi ya wakoloni. Katika harakati za kupinga ukoloni, Watanzania walionesha na kujenga uzalendo kwa jamii zao pale waliposimama kidete kuupinga uvamizi na utawala wa kikoloni kwa sera zao za unyonyaji na ukandamizaji. Pia, Watanzania walipinga kuingia kwa utawala wa kikoloni kwa kupambana kivita dhidi ya wavamizi

FOR ONLINE READING ONLY

wa Kijerumani na baadaye wa Kiingereza. Baadhi ya Watanzania waliochangia katika ujenzi wa uzalendo kwa jamii zao ni pamoja na Abushiri bin Salim al-Harthi wa Pangani, *Mangi* Meli wa *Old* Moshi, *Mtemi* Isike wa Unyanyembe, *Mtwa* Mkwawa wa Iringa, *Mwene* Machemba wa Wayao, *Nkosi* Songea, Mbano wa Wangoni na Liti Kidanka wa Singida.

Hivyo, harakati za wazalendo hawa kupinga uvamizi wa kikoloni, ulichangia katika ujenzi wa maadili ya uzalendo kwani wananchi walijitoa kushiriki katika vita na ulinzi wa jamii zao. Wanajamii walichangia ujenzi wa uzalendo pale walipopinga waziwazi sera za wakoloni na walipojitoa kushiriki katika vita dhidi ya wavamizi. Harakati za kupinga utawala na mifumo ya kikoloni zilipanda mbegu ya uzalendo kwa jamii za Kitanzania, kupenda jamii zao na hata kujitoa maisha yao kupambana dhidi ya uvamizi wa kikoloni. Hali hii ilichangia katika ujenzi wa kizalendo ndani ya jamii zao na baadaye kwa nchi nzima ya Tanzania.

Vilevile, harakati za kudai uhuru wa Tanganyika na Zanzibar nazo zilichangia katika ujenzi wa uzalendo miongoni mwa Watanzania. Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na *Sheikh* Abeid Amani Karume pia walitoa mchango mkubwa nyakati zote za harakati za kudai uhuru. Walijitolea sehemu kubwa ya maisha yao kupigania uhuru wa Tanganyika na Zanzibar. Mwalimu Nyerere kwa upande wa Tanganyika alitoa mchango mkubwa katika kubadili TAA na kuanzishwa kwa TANU tarehe 7 Julai 1954, kwani chama cha TAA kilikuwa na mwelekeo wa kijamii zaidi kuliko siasa. Pia, Mwalimu Nyerere akiwa mwenyekiti wa TANU na *Sheikh* Karume akiwa mwenyekiti wa ASP walifanikiwa kuwaunganisha viongozi na wananchi hadi kupatikana kwa uhuru wa Tanganyika na Zanzibar mtawalia. Kielelezo 4.8 kinaonesha picha ya viongozi wakuu wa TANU na ASP, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na *Sheikh* Abeid Amani Karume.



**Kielelezo 4.8:** *Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na Sheikh Abeid Amani Karume*

Aidha, viongozi wa vyama vya TANU na ASP pamoja na viongozi wengine katika ngazi mbalimbali walikuwa wazalendo, kwani walitoa mchango muhimu katika kuanzisha na kuendeleza harakati za kudai uhuru. Uzalendo wao ulidhihirika kupitia

FOR ONLINE READING ONLY

ushiriki wao katika kuanzisha na kusimamia vyama vya siasa. Kupitia vyama hivyo, viongozi hawa walihamasisha uzalendo kwa kuwaongoza wanachama na hata wananchi kudai uhuru na haki zao. Mbali na Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na *Sheikh* Abeid Amani Karume, kulikuwa na wazalendo wengine ambao nafasi yao kubwa ilikuwa kufadhili harakati za uhuru kwa hali na mali. Miongoni mwao walikuwemo John Rupia, Dossa Aziz, Abdulwahid Sykes na wengine. Uzalendo huu ulienea nchi nzima, ambapo watu walijitolea mali zao kusaidia harakati za uhuru. Kwa mfano, Aikael Mbowe (Kilimanjaro), Hamisi Heri na Sadiki Patwa (Tanga), pamoja na Suleiman Masudi Mnonji (Lindi).

Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, pamoja na viongozi wengine, waliongoza chama cha TANU kwa uzalendo hadi kufanikiwa kuikomboa Tanganyika kutoka kwa utawala wa kikoloni. Mwalimu Julius Kambarage Nyerere alitembelea sehemu mbalimbali za Tanganyika katika juhudi za kuimarisha chama cha TANU. Kazi kubwa ilikuwa kuwaandaa wananchi kwa ajili ya madaraka na uhuru. Pia, TANUkwa kushirikiana na vyama vya wakulima na wafanyakazi, waliwaelimisha wananchi kuhusu umuhimu wa kujiunga na TANU ili kufanikisha kumng'oa mkoloni.

Hata hivyo, mwaka 1955, Julius K. Nyerere alitumwa na chama chake kwenda *New York,* makao makuu ya Umoja wa Mataifa, ili Umoja huo uwashawishi Waingereza kuipa Tanganyika uhuru wake. Mwaka 1957, Mwalimu Julius K. Nyerere aliteuliwa kujiunga na Baraza la Kutunga Sheria - *Legislative Council* (LEGCO).

Haikuwa rahisi kwa TANU kusonga mbele bila vikwazo. Waingereza waliwakataza watumishi wa serikali kujiunga na vyama vya siasa. Pia, mikutano ya hadhara ilipigwa marufuku na matawi ya TANU yalifungwa katika baadhi ya maeneo kwa lengo la kuidhoofisha TANU. Hata hivyo, chama hiki kiliendelea kusonga mbele na kushinda kwenye uchaguzi wa mwaka 1958/1959. Katika uchaguzi wa mwaka 1960, TANU ilishinda na kupata wajumbe wengi katika Baraza la Kutunga Sheria. Ushindi huo uliwaharakisha Watanganyika kupata uhuru wao mapema. Uhuru ulipatikana tarehe 9 Desemba 1961. Kielelezo 4.9 kinaonesha picha ya wananchi wakisherehekea uhuru wa Tanganyika.




**Kielelezo 4.9:** *Wananchi wakisherehekea uhuru wa Tanganyika mwaka 1961*

FOR ONLINE READING ONLY

## Kazi ya kufanya 4.5

Tafuta taarifa kutoka vyanzo mbalimbali ikiwemo mitandao, kisha bainisha jinsi maadili mengine ya Kitanzania yaliyotunzwa wakati wa harakati za kudai uhuru wa Tanganyika na Zanzibar.

## Zoezi la 4.4

1. Eleza jinsi maadili ya kikoloni yalivyoathiri maadili ya jamii za Kitanzania wakati wa ukoloni.
2. Kwa kurejea muktadha wa kipindi cha kupigania uhuru wa Tanganyika na Zanzibar. Fafanua misingi ya usemi kuwa, "umoja ni nguvu, utengano ni udhaifu".
3. Pendekeza mikakati ya kudumisha maadili yaliyotunzwa wakati wa harakati za kudai uhuru wa Tanganyika na Zanzibar.
4. Eleza mikakati ya kujenga uzalendo kwa vijana katika mazingira ya sasa.

FOR ONLINE READING ONLY

## Zoezi la marudio

1. Je, unafikiri ni kwa nini harakati za kudai uhuru wa Tanganyika na Zanzibar zilifanikiwa kuwaunganisha wananchi?
2. Kwa nini vyama vya TANU na ASP vilipata uungwaji mkono mkubwa ukivilinganisha na vyama vingine vya siasa wakati wa kupigania uhuru?
3. Eleza mchango wa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na *Sheikh* Abeid Amani Karume katika kupatikana kwa uhuru wa Tanganyika na Zanzibar.
4. Eleza kwa nini uhuru wa Tanganyika na Zanzibar unapaswa kulindwa.
5. Fafanua maadili yaliyodumishwa wakati wa harakati za kudai uhuru wa Tanganyika na Zanzibar.
6. Kwa kutumia mifano, eleza maana ya uzalendo.
7. Jadili mchango wa viongozi wa kisiasa wa sasa katika kutunza maadili na kujenga uzalendo.

# Sura ya Tano

# Ujenzi wa taifa baada ya ukoloni

## Utangulizi

Mara tu baada ya kupata uhuru, kilianza kipindi cha mpito kutoka katika harakati za kudai uhuru hadi kuanzishwa kwa harakati mpya za ujenzi wa taifa huru. Katika sura hii, utajifunza dhana ya ujenzi wa taifa, mifumo ya kiuchumi, kisiasa, kijamii na kimaadili iliyojengwa kuanzia mwaka 1961 hadi 1966. Pia, utajifunza mikakati na changamoto zilizokuwapo katika harakati za ujenzi wa taifa. Umahiri utakaoujenga utakuwezesha kulinda na kuthamini juhudi za ujenzi wa taifa zilizoanzishwa na waasisi wa taifa letu.

**Fikiri**

Hali ya taifa letu mara baada ya uhuru.

### Dhana ya ujenzi wa taifa

*Ujenzi wa taifa ni mchakato unaohusisha juhudi za pamoja za kuunda taifa jipya lenye utambulisho wake kupitia mifumo ya kisiasa, kiuchumi, kijamii na kiutamaduni, unaozingatia haki, usawa na demokrasia. Katika taifa la Tanzania, mfumo huu* ulijengwa juu ya misingi ya kiitikadi, fikra, falsafa na maadili ya jamii za Kitanzania. *Harakati za ujenzi wa taifa zilikuwa muhimu kwa sababu ukoloni uliacha jamii iliyogawanyika, yenye ukosefu wa miundombinu muhimu, rasilimali watu na pia tofauti za kiuchumi na kijamii miongoni mwa wananchi. Harakati za ujenzi wa taifa baada ya ukoloni zililenga kujenga umoja wa kitaifa, uchumi imara, demokrasia, maadili na ustawi wa wananchi wote. Aidha, harakati hizi zililenga kuondoa mabaki na kasumba za mifumo ya utawala wa kikoloni iliyokuwa imeigawa jamii katika misingi ya rangi, kikabila, kidini na kikanda.*

### Mifumo iliyojengwa kati ya mwaka 1961 hadi 1966

*Uhuru wa Tanganyika wa Desemba 9, 1961, pamoja na Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar ya Januari 12, 1964, yaliashiria mwanzo wa ujenzi wa mifumo mipya ya*

FOR ONLINE READING ONLY

kisiasa, kijamii, kiutamaduni na kiuchumi kwa Taifa huru la Tanzania. Mifumo hiyo ilijengwa chini ya uongozi wa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere kwa upande wa Tanganyika na *Sheikh* Abeid Amani Karume kwa upande wa Zanzibar. Katika kipindi hiki, vyama vya TANU na ASP vililenga kujenga taifa lenye kuzingatia maadili ya usawa, utu, heshima kwa kila mtu, haki na wajibu. Aidha, umoja, uzalendo, kujitolea na kupenda kazi vilikuwa miongoni mwa maadili yaliyojengwa, yakiongozwa na kauli mbiu iliyotangaza vita dhidi ya maadui watatu: umaskini, ujinga na maradhi. Kila mwananchi alisisitizwa kuzingatia maadili ya Kitanzania na kujiepusha na unyonyaji, rushwa, ukabila na uzembe. Mifumo ya kisiasa, kiuchumi na kijamii iliyojengwa katika kipindi hiki imefafanuliwa vema katika sehemu zinazofuata.

**Kazi ya kufanya 5.1**

Pitia mtandao au vifaa vingine vya TEHAMA, sikiliza hotuba za waasisi wa taifa ambao ni Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na *Sheikh* Abeid Amani Karume kuhusu umuhimu wa maadili katika ujenzi wa taifa huru. Baada ya kusikiliza hotuba fanya yafuatayo:

(a) Bainisha mambo yaliyokugusa katika hotuba hizo.

(b) Kama ungekuwepo kipindi hicho ungependa kuwauliza mambo gani waasisi wa taifa letu?

(c) Eleza namna maadili yaliyozungumzwa katika hotuba hizo bado ni muhimu katika Tanzania ya sasa.

**Kisiasa**

*Tanganyika kuwa Jamhuri:* Tanganyika ilikuwa Jamhuri mwaka 1962. Jamhuri ni serikali ya watu yenye mamlaka kamili, inayoongozwa na Rais. Msukumo wa Tanganyika kuwa Jamhuri ulitokana na sababu mbalimbali. Kwanza, ilihitajika kuwa na uhuru kamili wa serikali, badala ya kuwa na uhuru wa bendera chini ya uongozi wa Malkia wa Uingereza. Kabla ya Tanganyika kuwa Jamhuri, serikali ilikuwa inaongozwa na Mwalimu Julius Kambarage Nyerere kama Waziri Mkuu, aliyekuwa chini ya mamlaka ya Malkia wa Uingereza, huku Gavana wa kikoloni akiendelea kuwa kiongozi mkuu wa nchi, akimwakilisha Malkia Elizabeth II wa Uingereza. Gavana huyo aliendelea kutekeleza baadhi ya majukumu ya kiserikali, hivyo kumfanya Waziri Mkuu kukosa mamlaka kamili.

Pia, Tanganyika ilitaka kutambulika katika jumuiya za kimataifa kama nchi yenye uhuru kamili na kuwa Jamhuri ilikuwa njia ya kufanikisha hilo, kwani iliwapa fursa ya kushiriki katika mikutano na jumuiya hizo za kimataifa. Vilevile, wananchi walitaka

FOR ONLINE READING ONLY

Serikali ya Jamhuri ili kuwa na uwezo wa kuingia mikataba ya kimataifa kama nchi huru na yenye mamlaka yake kamili. Sababu nyingine ya kuunda Jamhuri ilikuwa ni kuwaondoa Wazungu katika nafasi za juu za uongozi na kuruhusu Watanganyika kushika madaraka ya uongozi wa taifa lao. Baada ya Tanganyika kupata uhuru, Waingereza walikuwa bado wameshikilia baadhi ya nafasi za uongozi na waliendelea kutoa miongozo katika utawala wa nchi, hali iliyowafanya Watanganyika wajihisi kuwa bado wapo chini ya utawala wa kikoloni. Wananchi wa Tanganyika walitaka kufanya uamuzi bila kuingiliwa na wakoloni, kwani viongozi wa serikali hawakuwa na uhuru wa kufanya uamuzi wa kiutawala kabla ya kuwa Jamhuri.

Aidha, nchi kuwa Jamhuri kulilenga kuwapa uhuru wananchi na viongozi kujitawala na kuharakisha maendeleo ya taifa. Jamhuri ilileta umoja na mshikamano, ikitokomeza misingi ya ukabila na udini ambayo ilitumiwa na wakoloni kuwatenganisha Watanganyika, hivyo kuwapa nafasi ya kujiletea maendeleo kwa kasi zaidi. Baada ya Tanganyika kuwa Jamhuri, Mwalimu Nyerere aliunda baraza la kwanza la mawaziri, kama baadhi yao wanavyoonekana katika Kielelezo 5.1.

**Kazi ya kufanya 5.2**

Tafuta taarifa kutoka vyanzo mbalimbali ikiwamo mtandao ili kubainisha majina ya mawaziri wa Baraza la Mawaziri la kwanza la Tanganyika mwaka 1961.



**Kielelezo 5.1:** *Baraza la Kwanza la Mawaziri la Tanganyika mwaka 1961*

FOR ONLINE READING ONLY

*Kuanzishwa kwa sera ya Afrikanaizesheni:* Hii ni sera iliyowapa madaraka Watanganyika na Wazanzibari wazawa. Sera hii ililenga kutoa nafasi za uongozi na ajira kwa wazawa ambazo awali zilikuwa zikishikiliwa na Wazungu na Waasia wakati wa utawala wa kikoloni. Watanganyika na Wazanzibari wenye ujuzi walihamasishwa kufanya kazi serikalini na katika mashirika ya umma.

*Kuanzishwa kwa mifumo ya ulinzi na usalama:* Ulinzi na usalama wa nchi ulikuwa ni suala lingine ambalo serikali iliweka mkazo katika kujenga taifa. Jitihada mbalimbali zilianzishwa ili kuhakikisha nchi inakuwa salama. Mfumo wa ulinzi na usalama wa taifa ulifayika kuanzia ngazi ya chini kupitia mfumo wa ubalozi wa nyumba kumi. Huu ulikuwa ni mfumo wa kiulinzi uliowezesha kujua ni nani anaingia na kufanya nini ndani ya nchi. Kwa kutumia mfumo huu, ilikuwa rahisi kuwabaini wageni na wahalifu hivyo, kuimarisha ulinzi na usalama katika makazi ya wananchi wote. Mfumo huu ulilenga kubaini shughuli, makazi na tabia za wananchi wote pamoja na wageni wao. Pia, kwa wale waliokuwa wakisafiri walipaswa kuripoti kwa balozi ili wajulikane walikotoka na wanakoelekea. Kila balozi alikuwa na jukumu la kusimamia eneo lake na kutatua changamoto husika au kuziwasilisha kwa mamlaka zinazohusika za serikali. Mfumo huu ulisaidia katika kulinda usalama, kujenga mshikamano, kusimamia mila na desturi za Kitanzania na kutatua changamoto mbalimbali za kijamii katika ngazi ya nyumba kumi.

Ili kuimarisha ulinzi na usalama, Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) liliundwa mwaka 1964. Tanzania ilirithi jeshi la kikoloni lililojulikana kama *King's African Rifles* (KAR), ambapo nafasi nyingi za juu zilikuwa zikishikiliwa na wageni, yaani Wazungu na Waasia. Mara baada ya uhuru, jeshi hili lilibadilishwa jina na kuitwa *Tanganyika Rifles* (TR) hadi mwaka 1964 lilipoanzishwa JWTZ. Hii ni kufuatia maasi ya jeshi la TR mwaka 1964 na serikali kuamua kuwafukuza waasi wote kutokana na kukosa utii, uaminifu na uzalendo. Brigedia Mirisho Sam Hagai Sarakikya aliteuliwa kuwa mkuu wa majeshi (Kielelezo 5.2).



**Kielelezo 5.2:** *Brigedia Mirisho Sam Hagai Sarakikya*

Baada ya kuanzishwa kwa JWTZ, serikali ikawa makini kuteua na kuchagua watu waliounda jeshi jipya. Kwa sehemu kubwa, jeshi hili liliundwa na vijana watiifu, waadilifu na wazalendo kutoka Chama cha TANU na ASP. Hivyo, chini ya uongozi wa Brigedia Sarakikya waliunda Jeshi la nchi kavu *(infantry),* jeshi la majini *(navy)* na jeshi la anga *(airforce).* Pia Jeshi jipya lilianzisha shule za wapiganaji na vyuo vya maofisa. Sarakikya aliongoza jeshi kuanzia 1964 hadi 1974.

FOR ONLINE READING ONLY

*Muungano wa Tanganyika na Zanzibar:* Tarehe 26 Aprili, 1964, ni tukio muhimu la kihistoria na kisiasa katika kipindi hicho. Muungano huu ulitokana na uhusiano wa kihistoria uliokuwepo kati ya jamii za Tanganyika na Zanzibar, uhusiano ambao ulitokana kwa kiasi kikubwa na udugu, historia na biashara uliojengwa karne nyingi kabla ya ukoloni. Aidha, Muungano huu ulikuwa nguzo muhimu katika kulinda uhuru na Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar. Muungano huu uliunda utaifa mpya wa Utanzania.

*Uanzishwaji wa mfumo wa chama kimoja cha kisiasa mwaka 1965:* Tanzania iliamua kufuta mfumo wa vyama vingi na kuanzisha mfumo wa chama kimoja. Vyama vilivyoruhusiwa kufanya siasa vilikuwa ni TANU kwa Tanganyika na ASP kwa upande wa Zanzibar. Sababu ya kuanzisha mfumo wa chama kimoja ilikuwa ni kuleta maendeleo na kuudumisha umoja na mshikamano. Uanzishwaji wa mfumo huu ulienda sambamba na uanzishwaji wa siasa ya ujamaa na kujitegemea mwaka 1967.

FOR ONLINE READING ONLY

**Zoezi la 5.1**

1. Pendekeza mikakati ya kuboresha mfumo wa ubalozi wa nyumba kumi katika kuimarisha ulinzi na usalama kwenye mazingira unayoishi.
2. Kwa nini sera ya Afrikanaizesheni ilikuwa muhimu mara baada ya uhuru wa Tanganyika na Mapinduzi ya Zanzibar?
3. Eleza umuhimu wa kuwa na vijana wenye uzalendo katika taifa.
4. Eleza umuhimu wa Jeshi la Kujenga Taifa katika kujenga maadili ya vijana wa Kitanzania.

**Uchumi na huduma za jamii**

Mara baada ya uhuru, serikali iliweka mkazo katika kujenga mifumo imara ya uchumi na huduma za jamii. Harakati za kujenga mifumo hii ziliongozwa na nadharia ya kupambana na maadui watatu: ujinga, maradhi na umasikini. Kuwapo kwa ujinga, maradhi na umasikini kulisababishwa na mifumo ya kiuchumi na kijamii iliyojengwa wakati wa ukoloni. Hivyo, katika kipindi hiki, kulikuwa na umuhimu wa kujenga na kuimarisha uchumi na huduma za jamii.

*Uchumi*

Mara baada ya uhuru, Tanganyika na Zanzibar zilirithi mfumo wa uchumi wa kikoloni ambao ulinufaisha watu wachache, wengi wao wakiwa wageni. Uchumi huu haukuwa na uwiano wa maendeleo; kulikuwa na maendeleo hafifu katika sekta ya kibiashara, huku sekta ya viwanda ikiwa ndogo na kumilikiwa na wageni. Kulihitajika kujenga

mfumo mpya wa uchumi. Mifumo ya uchumi iliyobuniwa katika kipindi hiki ililenga kujenga jamii ya watu wanaojitegemea. Kwa mfano, Tanganyika ilianzisha Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitatu uliotekelezwa kuanzia mwaka 1961 hadi 1964. Baada ya mpango huo, ulianzishwa Mpango wa Kwanza wa Maendeleo wa Miaka Mitano (1964–1969), ambao ulitakiwa kufuatiwa na Mpango wa Pili wa Miaka Mitano. Mipango hii ililenga, miongoni mwa mambo mengine, kuleta maendeleo ya kiuchumi ya taifa huru.

Kuanzia mwaka 1963 hadi 1965, sera ya maendeleo vijijini ilianzishwa. Hii ilikuwa ni sehemu ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitatu. Sera hii ililenga kuwaweka wananchi katika vijiji ili kuimarisha kilimo kwa kutumia teknolojia ya kisasa. Serikali iliamini kuwa kuwakusanya wananchi vijijini kungewezesha kurahisisha utoaji wa huduma za ugani, elimu na miundombinu muhimu. Hii ilisaidia pia kuhamasisha maendeleo ya kilimo na kuwapa wananchi fursa ya kushiriki kikamilifu katika ujenzi wa taifa. Kilimo kilipewa kipaumbele na kuhimizwa kuwa uti wa mgongo wa taifa, huku wakulima wakihamasishwa kulima mazao ya biashara na chakula. Kupitia uhamasishaji huu, walipatiwa pembejeo na kupewa uhakika wa masoko ya mazao yao kupitia vyama vya ushirika.

Vilevile, viwanda mbalimbali vilijengwa Tanganyika. Kwa mfano, Kiwanda cha Nguo cha Urafiki kilijengwa mwaka 1966 chini ya makubaliano ya urafiki kati ya Tanzania na China. Hiki kilikuwa kiwanda kamilifu chenye mitambo ya kisasa ya utengenezaji wa nguo. Viwanda vingine vingi katika kipindi hiki vilimilikiwa na wageni na vilijikita katika uzalishaji wa bidhaa kama vile vinywaji, uchakataji wa malighafi za kilimo na bidhaa za matumizi kama *Coca-Cola, East African Breweries, Tanganyika Packers, British American Tobacco, Metal Box* na *Bata Shoes*, Ubungo *Fram Impelements* na *National Printing Company.*

Aidha, serikali ilijikita katika kuhakikisha taasisi za fedha zinaendelezwa ili kuwa mihimili muhimu katika ukuaji wa uchumi na maendeleo ya taifa. Serikali ilianzisha Benki Kuu ya Tanzania mwaka 1966 ili kusimamia masuala muhimu ya kifedha nchini. Pia sekta nyingine, kama vile uvuvi, nishati na madini, zilipewa kipaumbele.

**Kazi ya kufanya 5.3**

Tembelea wazee na watu wengine wenye ufahamu kuhusu mifumo ya uchumi iliyojengwa mara baada ya uhuru, kisha fanya mahojiano nao kuhusu mifumo hiyo kwa kuzingatia mambo yafuatayo:

(a) Maisha ya jamii kiuchumi mara baada ya uhuru;

(b) Mifumo ya kiuchumi iliyojengwa na jinsi ilivyoinufaisha jamii; na

(c) Andika ripoti ya uchunguzi wako.

FOR ONLINE READING ONLY

*Huduma za jamii*

Mabadiliko katika utoaji huduma za jamii yalilenga kubadilisha mfumo wa kikoloni na kuunda mfumo unaokidhi mahitaji ya taifa huru. Mfumo mpya wa utoaji huduma za jamii ulilenga kujenga jamii yenye ujuzi, maarifa na afya katika ujenzi wa taifa huru.

Mara baada ya uhuru vipaumbele vya elimu vilibadilika kuendana na matakwa ya nchi. Baada ya uhuru, wataalamu wengi Wazungu waliondoka, hivyo watumishi Waafrika walibaki wachache. Hii ilileta umuhimu wa kuwaandaa wataalamu wazawa. Kwa maana hiyo, serikali ilijikita kutoa elimu kwa wote iliyokuwa na lengo la kufanya kila raia anakuwa na ufanisi katika kazi zake za kila siku na inayoweza msaidia kujiendeleza zaidi kielimu. Hii ilitekelezwa zaidi upande wa elimu ya msingi ambapo shule mpya zilijengwa na kuongeza idadi ya wanafunzi. Pia, Mpango wa Kwanza wa Miaka Mitano ulijikita katika upanuzi wa elimu ya sekondari ili kuandaa wataalamu na viongozi wa baadaye, ingawa changamoto za rasilimali na walimu zilikuwepo. Pamoja na hayo, elimu hii ilitolewa kwa watu wote bila kujali jinsia, ukanda, hadhi au kabila tofauti na elimu ya kikoloni. Serikali ilianzisha na kujenga shule mpya na kuongeza idadi ya wanafunzi waliojiunga na elimu ya sekondari.

Vilevile, serikali ilianzisha vyuo vya ufundi ili kutoa mafunzo ya ufundi na ufundi stadi kwa vijana, jambo ambalo lilikuwa muhimu kwa kuimarisha sekta ya viwanda na kilimo. Kwa mfano, Chuo cha Ufundi Dar es Salaam, ambacho kilipanuliwa mwaka 1962 na kuanza kutoa elimu ya ufundi mwaka 1964. Aidha vyuo vya ualimu vilianzishwa na kupanuliwa. Baadhi ya vyuo hivyo ni Chuo cha Ualimu Morogoro (Kigurunyembe) ambacho hapo mwanzo kilimilikiwa na Wamisionari. Chuo hiki kilijikita katika kuandaa walimu wa kwenda kufundisha shule za msingi ili kuendana na upanuzi wa shule za msingi nchini walipoanzisha Daraja la IIIA mwaka 1961 na Diploma (stashahada) baadae mwaka 1970 baada ya kupandishwa hadhi na kuanza kutoa mafunzo ya Diploma (stashahada) mwaka 1966.

Maendeleo katika sekta ya elimu hayakuishia katika kada za chini na kati tu, bali yalienda hadi katika elimu ya juu. Kwa mfano, mwaka 1961 serikali ilikianzisha Chuo Kikuu Kishiriki cha Dar es Salaam (*University College of Dar es Salaam*) chini ya Chuo Kikuu cha London. Hii ilikuwa hatua muhimu katika kuandaa wasomi na wataalamu mbalimbali wa ngazi ya juu.

Upanuzi wa miundombinu ya afya, ikijumuisha ujenzi wa zahanati na hospitali za umma vijijini na mijini. Upanuzi mkubwa ulikuwa ni ule wa Hospitali ya Muhimbili mnamo mwaka 1961 mara baada ya uhuru. Upanuzi huu ulisababisha kubadili jina toka Hospitali ya *Princess Margareth* na kuwa Hospitali ya Muhimbili. Hii ilikuwa hatua kubwa sana katika sekta ya afya. Pia, serikali ilijenga na kupanua hospitali za kikanda na pia kujenga vituo vya afya na zahanati katika maeneo ya mijini na vijijini. Lengo lilikuwa kufikisha huduma kwa wananchi wengi, hususani wale wa maeneo ya vijijini ambao awali walikuwa hawapati huduma bora za afya. Juhudi hizi zilihusisha kuajiri na kutoa mafunzo kwa wahudumu wa afya.

FOR ONLINE READING ONLY

Aidha, uanzishwaji programu za mafunzo ya wahudumu wa afya na madaktari. Hii ilijumuisha ufadhili wa masomo kwa wanafunzi wa tiba na wahudumu wa afya waliokuwa wakipelekwa nje ya nchi kwa mafunzo ya juu. Vilevile, serikali ilijitahidi kuleta vifaa tiba na dawa kutoka nje ya nchi ili kuongeza ubora wa huduma zilizokuwa zinatolewa. Juhudi zote hizi ziliwezesha kuboresha hali ya afya kwa ujumla, kuweka mfumo wa afya wakushughulikia changamoto mbalimbali za kiafya.

**Zoezi la 5.2**

1. Eleza umuhimu wa elimu katika kujenga taifa lenye umoja, amani na mshikamano mara baada ya uhuru.
2. Chambua mchango wa huduma za jamii katika kukuza uchumi wa nchi mara baada ya uhuru.
3. Linganisha mikakati ya utoaji huduma za jamii mara baada ya uhuru na sasa.

**Utamaduni na maadili**

Utamaduni ni mfumo wa maisha unaojengwa na kurithishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine kupitia malezi, elimu na mawasiliano ndani ya jamii. Unajumuisha imani, maadili, mila na desturi, lugha, sanaa, muziki, mavazi, chakula na tabia ambazo zinaainisha na kuunganisha kundi fulani la watu. Katika kipindi cha uhuru, utamaduni ulikuwa na jukumu muhimu katika kuunda na kujenga taifa. Moja ya hatua kubwa zilizochukuliwa na serikali katika kipindi hicho ilikuwa kuifanya lugha ya Kiswahili kuwa lugha rasmi ya taifa. Wakati huo, Kiswahili hakikutumika tu kama chombo cha mawasiliano, bali pia kama njia ya kuhifadhi na kueneza maarifa, maadili na historia ya jamii.

Pia, serikali ilianzisha vyombo mbalimbali vya kusimamia sanaa na michezo ili kulinda na kukuza utamaduni wetu. Ilianzisha Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA), Baraza la Michezo la Taifa (BMT), Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA), Bodi ya Filamu Tanzania, Makumbusho ya Taifa na vyama mbalimbali vya kusimamia michezo kama mpira wa miguu, pete, kikapu, ndondi na riadha.

Aidha, sanaa na muziki ni sehemu nyingine muhimu ya utamaduni iliyopewa uzito kipindi hiki. Sanaa kama vile uchoraji, uchongaji, ngoma na nyimbo hutumiwa kuelezea hisia, mawazo na historia ya jamii. Muziki ulitumika kuelezea maadili na mapambano yaliyofanywa kulikomboa taifa. Vilevile, sanaa na muziki vilitumika kuamsha hisia za umoja na fahari ya taifa. Wasanii na waandishi wa vitabu walihimizwa kutumia kazi zao kuelimisha umma kuhusu ujenzi wa taifa. Bendi mbalimbali za muziki zilianzishwa na nyingine kuimarishwa. Baadhi ya bendi hizo ni kama NUTA Jazz Band (1964), Dar es Salaam Jazz Band, Kilwa Jazz Band, Morogoro Jazz Band,

FOR ONLINE READING ONLY

Cuban Marimba *Band* na Jamuhuri Jazz *Band*. Bendi hizi zilivutia mashabiki wengi kwa mtindo wa muziki wa rumba na cha-cha-cha. Mlimani *Park Orchestra* (Sikinde) ilianzishwa mwaka 1978, lakini chimbuko lake lilikuwa katika miaka ya 1960 na baadaye ikawa mojawapo ya bendi kubwa sana nchini. Kielelezo 5.3 kinaonesha baadhi ya waimbaji wa bendi ya muziki ya NUTA wakiwa jukwaani.



**Kielelezo 5.3:** *NUTA Jazz Band*

**Kazi ya kufanya 5.4**

Kwa kutumia mtandao au maktaba mtandao, soma matini mbalimbali na chunguza mchango wa lugha ya Kiswahili katika kujenga utambulisho wa taifa mara baada ya uhuru. Baada ya uchunguzi andika ripoti fupi kwa maneno yasiyozidi ukurasa mmoja.

**Zoezi la 5.3**

1. Je, ni kwa namna gani sanaa na muziki vinaweza kuendelea kutumika kama nyenzo za kuyajenga maadili na uzalendo katika Tanzania ya sasa?
2. Eleza nafasi ya sanaa katika kuleta maendeleo ya jamii.
3. Eleza nafasi ya Kiswahili katika kuuendeleza na kuudumisha utamaduni wa Mtanzania kwa kizazi cha sasa.

FOR ONLINE READING ONLY

## Mikakati ya ujenzi wa taifa

Kati ya mwaka 1961 hadi 1966, serikali ya Tanzania iliweka mikakati mbalimbali ya kujenga taifa linalojitegemea. Mojawapo ya mikakati hiyo ilikuwa kuanzisha mfumo wa chama kimoja cha siasa, Chama cha TANU, ambacho kilikuwa chama pekee kilichoruhusiwa kufanya shughuli za kisiasa Tanganyika (Tanzania Bara) na Chama cha ASP kwa upande wa Zanzibar. Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliona mfumo wa chama kimoja kama njia bora ya kuleta mshikamano na umoja wa kitaifa. Mfumo huu ulilenga kuondoa siasa za kibaguzi na kuipunguza migogoro ya kisiasa ambayo ingeweza kutishia umoja wa taifa changa. Aidha, mfumo wa chama kimoja ulikuwa njia ya kuhamasisha jamii kushiriki katika shughuli za maendeleo.

Vyama vya TANU na ASP vilikemea ukiukwaji wa maadili na muundo wa kijamii, kisiasa na kiuchumi ulioathiriwa kutoka mfumo wa kikoloni. Mfumo wa kikoloni ulikuwa na ubaguzi na vitendo vya rushwa. Kutokana na hali hii, TANU ilitengeneza kauli mbiu yake iliyosema, "Rushwa ni adui wa haki, sitatoa wala kupokea rushwa." Tanganyika iliendelea na mapambano dhidi ya vitendo vya rushwa kwa kutumia Sheria ya Kuzuia Rushwa (Sura ya 400) ya Mwaka 1958 (*The Prevention of Corruption Ordinance, PCO, of 1958*), sheria iliyorithiwa kutoka kwa wakoloni.

Pia, mwaka 1962, serikali ilifuta mfumo wa uchifu katika uongozi wa nchi. Kuondolewa kwa mfumo wa machifu, ambao ulikuwa sehemu muhimu ya utawala wa kikoloni, kulikuwa na mkakati wa makusudi wa kulijenga taifa jipya. Machifu walikuwa na nguvu kubwa katika jamii zao na mara nyingi walitumiwa na wakoloni kama vibaraka wao. Lengo la kuondoa mfumo huu lilikuwa kuvunja mamlaka ya kikabila na kuipa serikali kuu mamlaka ya kutawala maeneo yote, hivyo kuondoa hisia za ukabila.

Vilevile, serikali ilianzisha Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) tarehe 10 Julai, 1963. Jeshi hili lilianzishwa kama sehemu ya mikakati ya kukuza uzalendo, maadili na ujenzi wa taifa. Jeshi hili lililenga kutoa mafunzo ya kijeshi pamoja na stadi za kazi kwa vijana wa Kitanzania. Kupitia JKT, vijana walihamasishwa kushiriki katika ujenzi wa miundombinu ya taifa, kama vile barabara, mashamba ya umma na miradi mingine ya maendeleo. Jeshi hili lilitumika kama chombo cha kuimarisha nidhamu, uzalendo, uvumilivu, kujitolea na uwajibikaji wa kijamii miongoni mwa vijana na kuwafanya kuwa sehemu ya nguvu kazi na hazina ya taifa. Hivyo, JKT liliwajengea vijana nidhamu, uzalendo, ukakamavu na kuwafundisha ujuzi hatimaye kuchangia katika ulinzi wa Taifa na maendeleo ya kiuchumi.

Halikadhalika, miaka mitano baada ya uhuru wa Tanganyika, yaani mwaka 1966, vitendo vya rushwa vilionekana kuongezeka na baadhi ya viongozi wa umma walianza kujisahau. Tofauti kubwa kati ya watu wenye nacho na wasio nacho, pamoja na wenye elimu na wasio na elimu, ilionekana kuongezeka. Watu waliosoma walikuwa na fursa

FOR ONLINE READING ONLY

za kupata huduma bora, hasa katika utoaji wa mikopo. Aidha, baadhi ya watu ndani ya chama walionesha nia ya kupata uongozi ili kujinufaisha binafsi na kujilimbikizia mali. Baadhi ya mambo yaliyojitokeza baada ya uhuru ni kama yafuatayo:

(a) Kujengeka kwa matabaka ya kiuchumi, kisiasa na kijamii, kinyume na mfumo wa kijamii uliokuwepo kabla ya uhuru ambapo jamii iliishi kwa umoja, udugu, upendo na kushirikiana; na

(b) Baadhi ya viongozi na watumishi wa umma walianza kukiuka maadili ya utumishi wa umma na kutumia nafasi walizopewa kama vitega uchumi ili kujinufaisha wenyewe.

Kutokana na kuongezeka kwa matabaka, ubadhirifu wa mali na baadhi ya viongozi wa umma kuanza kujilimbikizia mali, Serikali ya Awamu ya Kwanza ilichukua hatua ya kuunda tume. Mwaka 1966, Mwalimu Julius K. Nyerere aliunda Tume ya Rais ya Kudumu ya Uchunguzi (*The Presidential Permanent Commission of Enquiry*) ili kuchunguza mwenendo wa viongozi na watumishi wa umma waliokuwa wakikiuka maadili, kujilimbikizia mali na kutumia madaraka vibaya kinyume na miiko ya chama cha TANU, ambacho mara kwa mara kilikemea vitendo vya rushwa. Tume ya Rais ya Kudumu ya Uchunguzi ya mwaka 1966 ilichangia Kamati Kuu ya TANU kutangaza Azimio la Arusha mwaka 1967, lililoweka miiko mbalimbali yenye misingi ya utu na usawa katika jamii, mambo ambayo yalisaidia katika mapambano dhidi ya rushwa.

Kwa upande wa Zanzibar, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iliweka sera ya umiliki wa ardhi chini ya tangazo la tarehe 8 Machi 1964. Kupitia tangazo hilo, Serikali ya *Sheikh* Abeid Amani Karume ilitaifisha mali zisizohamishika kama ardhi, mashamba na majengo na kuweka mpango wa ugawaji ardhi kwa utaratibu wa hekari tatu kwa kila familia. Sheria hiyo ilitoa fursa kwa ardhi iliyotaifishwa kugawanywa kwa familia na watu masikini wasio na ardhi. Kabla ya mapinduzi, asilimia kubwa ya ardhi, yakiwemo mashamba ya mikarafuu na minazi, ilikuwa ikimilikiwa na watu wachache hasa Waarabu.

Ugawaji wa ardhi ulifanyika kupitia amri ya utaifishaji wa mali zisizohamishika, "*The Confiscation of Immovable Property Decree 1964*," na amri ya ugawaji wa ardhi, "*The Land Distribution Decree 1966*." Ugawaji huo ulianza huko Dole tarehe 11 Novemba 1965, ambapo wananchi waligawiwa hekari tatu kila familia. Hadi kufikia mwaka 1973, zaidi ya hekari 24,000 zilikuwa zimetolewa kwa Wazanzibari.

FOR ONLINE READING ONLY

**Kazi ya kufanya 5.5**

Tafuta taarifa kutoka vyanzo mbalimbali ikiwemo mtandao na andika maelezo zaidi kuhusu uanzishwaji wa mfumo wa chama kimoja cha siasa na mchango wake katika ujenzi wa taifa.

**Zoezi la 5.4**

1. Eleza mchango wa mfumo wa chama kimoja katika ujenzi wa taifa katika kipindi cha 1961 hadi 1966.
2. Ni kwa namna gani tatizo la ardhi Zanzibar lilitatuliwa mara baada ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar?
3. Fafanua mchango wa Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) katika kukuza maadili na uzalendo kwa vijana mara baada ya uhuru.
4. Toa sababu tano zilizosababisha serikali kuvunja mamlaka za jadi mwaka 1962.

## Changamoto za ujenzi wa taifa

Kipindi cha mwaka 1961 hadi 1966 Taifa lilipitia changamoto mbalimbali za kiuchumi. kijamii na kisiasa. Kwa mfano, sekta ya kilimo ilipitia changamoto mbalimbali ikiwemo matumizi ya zana duni. Pia, kulikuwa na ukosefu wa wataalamu wa kilimo na uhaba wa masoko ya uhakika ya bidhaa. Hata hivyo, viwanda vilikuwa havijaimarika kutokana na upungufu wa wataalamu wa kuviendesha na pia kulikuwa na uhaba wa vipuri. Matatizo ya kifedha na mitaji yaliathiri juhudi za awali za kuleta maendeleo nchini. Aidha, kukosekana kwa uhusiano wa moja kwa moja kati ya kilimo na viwanda kuliathiri maendeleo ya sekta zote mbili. Hata hivyo, pamoja na changamoto hizi zote, pato la taifa liliendelea kukua na kuimarika na hili liliendelea kuipa Tanzania heshima kimataifa. Kwa ujumla, kulikuwa na changamoto kadhaa zilizoathiri ujenzi wa taifa mara baada ya uhuru.

**Uasi wa jeshi mwaka 1964:** Uasi wa Januari 20-27, 1964, pale Colito (sasa Lugalo), ambapo kikundi kidogo cha wanajeshi wa Tanganyika Rifles (TR) kiliasi na kutaka kuipindua serikali. Jaribio hilo lilizimwa na waliohusika walipewa adhabu kali, kama kufukuzwa jeshini, kufungwa na kuwekwa kizuizini kwa muda mrefu. Uasi huu ulisababisha kuundwa kwa Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ).

FOR ONLINE READING ONLY

**Kuibuka kwa tabaka la mabepari uchwara:** Kama ilivyokuwa katika nchi nyingine nyingi za Afrika, tabaka jipya la mabepari uchwara waliokuwa wamechukua madaraka serikalini walianza kutumia nyadhifa zao kujinufaisha. Wananchi walianza kushuhudia viongozi wakiishi maisha ya anasa huku raia wa kawaida wakibaki masikini. Hali hii ilikuwa tishio kwa umoja, maadili, amani na mshikamano uliokuwa unasisitizwa na kujengwa mara baada ya uhuru.

**Hali mbaya ya uchumi:** Katika kipindi hiki, hali mbaya ya uchumi ilitokea na kuathiri sana upatikanaji wa huduma za kijamii kama elimu, afya na nyinginezo zinazotolewa na serikali. Tatizo hili lilisababisha pia ukosefu wa wataalamu, teknolojia duni, kuongezeka kwa maradhi, ujinga na umaskini, pamoja na kuwapo kwa miundombinu mibovu. Uchumi ulitegemea kwa kiasi kikubwa uzalishaji wa malighafi badala ya bidhaa za viwandani. Hata hivyo, serikali ilianza kuchukua hatua za mageuzi ili kurekebisha changamoto hizi.

Serikali pia ilikabiliwa na changamoto za kifedha na kiutawala katika kutoa huduma za afya kwa umma. Juhudi za kuanzisha zahanati na hospitali mpya zilikwamishwa na upungufu wa vifaa na wahudumu wa afya wenye sifa. Hali hii ilisababisha huduma za afya kutokidhi mahitaji katika baadhi ya maeneo. Pia, utegemezi wa misaada kutoka mataifa mengine ulifanya utoaji wa huduma za afya na miradi mingine kudorora.

Uwapo wa vita baridi miongoni mwa mataifa makubwa duniani pia kuliathiri sera za mambo ya nje za Tanzania. Hii ni kwa sababu nchi ilikuwa mwanachama wa Harakati za Kutofungamana na Upande Wowote (*Non-Alignment Movement, NAM*). Hali hii ilileta migogoro na mataifa makubwa yaliyokuwa yakihasimiana. Vilevile, utegemezi wa misaada kutoka nje ulipunguza uhuru wa taifa wa kupanga na kuamua mambo yake. Kwa mfano, mwaka 1965, Tanzania ilikumbwa na mgogoro wa kidiplomasia na Uingereza, hali iliyosababisha Uingereza kusitisha misaada. Hii iliathiri utekelezaji wa miradi mingi ya kimkakati nchini. Pamoja na changamoto hizi, mikakati ya awali ya ujenzi wa taifa iliweka msingi muhimu kwa juhudi za baadaye za maendeleo.

**Kazi ya kufanya 5.6**

Tafuta taarifa kutoka vyanzo mbalimbali ikiwemo mtandao na bainisha changamoto nyingine za ujenzi wa taifa na jinsi zilivyotatuliwa.

FOR ONLINE READING ONLY

## Zoezi la marudio

1. Eleza jinsi tabaka jipya la mabepari uchwara lilivyoathiri umoja na maadili ya kitaifa baada ya uhuru.
2. Fafanua mikakati iliyochukuliwa na serikali baada ya uasi wa jeshi wa Januari 1964 ili kuimarisha usalama wa taifa.
3. Fafanua umuhimu wa sera na mifumo ya kisiasa iliyoanzishwa mara baada uhuru katika maendeleo ya kiuchumi na kisiasa kwa Tanzania ya sasa.
4. Eleza faida za Tanganyika kuwa Jamhuri.
5. Ni kwa jinsi gani ngoma na nyimbo za jadi zinaweza kutumika katika kujenga maadili na umoja wa kitaifa wakati wa sasa?
6. Ni maadili gani yalijengwa na kukuzwa wakati wa ujenzi wa taifa, 1961 hadi 1966?
7. Ni njia gani bora zinazoweza kutumika kujenga na kuimarisha umoja wa kitaifa wakati wa sasa?
8. Pendekeza mikakati ya kuendelea na ujenzi wa taifa la Tanzania wakati wa sasa.

FOR ONLINE READING ONLY

# Sura ya Sita

# Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar

## Utangulizi

*Katika harakati za kudai uhuru, njia mbalimbali zilitumika. Njia hizo zilijumuisha matumizi ya mtutu wa bunduki, mapinduzi na njia ya amani au katiba. Zanzibar ilitumia njia ya mapinduzi katika harakati za kudai uhuru wa kweli. Katika sura hii, utajifunza kuhusu dhana ya mapinduzi, chimbuko la Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar, sababu zake na mchango wake katika kujenga umoja, mshikamano na maadili ya taifa. Umahiri utakaoujenga utakuwezesha kuyatetea, kuyalinda na kuyaenzi Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar.*

**Fikiri**

*Historia ya Mapinduzi ya Zanzibar.*

FOR ONLINE READING ONLY

### Dhana ya mapinduzi

Neno 'mapinduzi' linaweza kuwa na maana nyingi kulingana na mazingira tofauti. Hata hivyo, katika muktadha huu, mapinduzi yanarejelea harakati za kubadili utawala wa kisiasa ndani ya muda mfupi, kwa kutumia nguvu za kijeshi au nguvu za umma. Kuna aina mbili za mapinduzi, ambazo ni mapinduzi ya kisiasa na mapinduzi ya kijeshi.

Mapinduzi ya kisiasa ni yale yanayofanywa kupitia nguvu za umma. Katika mapinduzi haya, wananchi walio wengi na wanyonge huwaondoa watawala wachache kwa kuzitumia nguvu za umma, mara nyingi bila kumwaga damu kwa kiasi kikubwa. Ili kufanikisha jambo hili, wananchi wanaweza kuandamana au kuzitumia mbinu nyingine za kijamii.

Aina ya pili ni mapinduzi ya kijeshi. Mapinduzi haya hufanywa na jeshi kwa lengo la kuondoa utawala uliopo madarakani kwa kutumia mapigano au mbinu za kijeshi. Mfano wa mapinduzi ya aina hii ni yale yaliyotokea Misri yakiongozwa na Kanali Gamal Abdel Nasser dhidi ya Mfalme Farouk I mwaka 1952, mapinduzi ya Mengistu Haile Mariam wa Ethiopia dhidi ya Haile Selassie mwaka 1974, mapinduzi ya Jenerali Iddi Amin Dada wa Uganda dhidi ya Rais Milton Obote mwaka 1971 na mapinduzi ya Libya chini ya Kanali Muammar Gaddafi dhidi ya Mfalme Idris mwaka 1969.

**Zoezi la 6.1**

1. Eleza sababu zilizosababisha Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar.
2. Fafanua namna uzalendo na ujasiri ulivyochangia kufanyika kwa Mapinduzi ya Zanzibar.
3. Jadili umuhimu wa kuyalinda Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar.

**Kazi ya kufanya 6.1**

Umeteuliwa kushiriki katika mdahalo wenye mada isemayo "*Mapinduzi ilikuwa ndio njia pekee ya Wazanzibari kujikwamua kutoka katika ukoloni*." Soma vitabu na matini mbalimbali kisha andaa dondoo utakazotumia wakati wa mdahalo.

## Chimbuko la Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar

Zanzibar ilikuwa chini ya utawala wa kisultani hadi mwaka 1890. Kama ilivyotajwa awali, Sultani Seyyid Saidi alikuwa sultani wa kwanza kuongoza dola mbili, yaani Oman na Zanzibar, akiifanya Zanzibar kuwa makao makuu ya himaya hizo. Sultani Seyyid Said alihamia Zanzibar mwaka 1840 akitokea Muscat, Oman. Mnamo mwaka 1890, Zanzibar iliwekwa chini ya utawala wa Waingereza na ikatambulika kama Mahamia ya Uingereza au "*British Protectorate*." Katika hali hiyo, utawala wa sultani ulitumiwa na Waingereza katika kuitawala Zanzibar. Hali hii ilisababisha mgawanyiko mkubwa kati ya Waarabu wachache, ambao walikuwa na nguvu kubwa za kisiasa na kiuchumi na Waafrika walio wengi ambao hawakuwa na nguvu zozote zaidi ya umasikini na kutumikishwa na Waarabu pamoja na wageni wengine wakiwemo Waingereza na Waasia.

FOR ONLINE READING ONLY

Mapinduzi ya Zanzibar yalitokana na sababu nyingi za kijamii, kiuchumi na kisiasa. Kwa mfano, Waarabu, ambao walikuwa wachache, walipewa upendeleo na walitawala kisiasa na kiuchumi. Hali hii haikuwaridhisha Waafrika waliokuwa wengi. Waarabu walihodhi madaraka, ardhi na utajiri mwingine wa Zanzibar, huku Waafrika wakiwa wafanyakazi wa watawala.

Aidha, jamii ya Zanzibar iliathiriwa kwa kiasi kikubwa na mchanganyiko mkubwa wa watu wenye tamaduni tofauti. Kulikuwa na watu wenye tamaduni za Waarabu, Waafrika na Wahindi. Hivyo, jamii iligawanyika katika makundi ya watu kulingana na rangi na asili ya jamii iliyohusika. Kwa mfano, jumuiya za Waarabu, hususani Waarabu wa Oman, walikuwa na nguvu kubwa za kisiasa na kiuchumi na walikuwa na hadhi ya juu zaidi. Wahindi walikuwa na nguvu za kiuchumi kwa kushikilia biashara nyingi, hivyo walikuwa ni kundi lenye hadhi ya kati. Wakati huo huo, Waafrika waliokuwa wengi na walikuwa na hadhi ya chini kabisa katika jamii, wakiwa hawana nguvu za utawala wala uchumi. Utaratibu huu uliathiri kanuni za kimaadili na kijamii za wakati huo, kwani heshima, utu na tabia ziliamuliwa kutokana na asili (rangi), hadhi na nafasi ya mtu katika jamii.

Kutokana na kukosa haki zao za msingi, vyama vya siasa vya ASP, ZNP na ZPPP viliongeza shinikizo kwa serikali ya kikoloni kuwapatia uhuru Wazanzibari. Vuguvugu hili halikuwa rahisi na lilichukua sura na mitazamo tofauti. Hata hivyo, baada ya malumbano makali na chaguzi nyingi kufanyika, Uingereza iliutoa uhuru kwa Zanzibar tarehe 10 Desemba 1963. Uhuru huu ulikuwa wa serikali ya mseto wa vyama vya ZNP na ZPPP. Katika kipindi hiki, Waziri Mkuu alikuwa Mohammed Shamte, huku Sultani Jamshid bin Abdullah Al Said akibaki kwenye nafasi yake kama kiongozi wa nchi. Uhuru huu haukuungwa mkono na wengi, hasa Waafrika, ambao waliona kuwa Waingereza wamekabidhi serikali kwa Waarabu badala ya wananchi wote.

Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar yalikuwa ni kilele cha harakati za mapambano ya ukombozi wa Wazanzibari. Mapambano haya yalikuwa ni matokeo ya uchaguzi na uhuru uliotolewa tarehe 10 Desemba 1963 chini ya serikali ya Waziri Mkuu Mohammed Shamte na Sultani Jamshid bin Abdullah Al Said, uhuru ambao ulijulikana kama "uhuru wa wachache." Hivyo, kufikia tarehe 12 Januari 1964,

FOR ONLINE READING ONLY

yalifanyika mapinduzi rasmi Zanzibar chini ya uongozi wa mwanamapinduzi *Sheikh* Abeid Amani Karume, ambaye aliiongoza Zanzibar kuanzia mwaka 1964 hadi alipouawa tarehe 7 April1972. Kielelezo 6.1 kinaonesha aliyekuwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, *Sheikh* Abeid Amani Karume.



**Kielelezo 6.1:** *Sheikh Abeid Amani Karume*

**Zoezi la 6.2**

1. Fafanua sababu za kihistoria zilizosababisha Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar mwaka 1964.
2. Eleza mchango wa *Sheikh* Abeid Aman Karume kwenye Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar.
3. Eleza mchango wa vijana katika kufanikisha Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar.

## Sababu za Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar

Kama ilivyoelezwa hapo awali, Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar yalikuwa matokeo ya upendeleo uliokuwepo tangu enzi za ukoloni, upendeleo ambao ulisababisha ubaguzi mkubwa katika sekta mbalimbali na kuwafanya Waafrika kuwa duni na wanyonge. Ubaguzi huu ulikuwa pigo kubwa kwa Waafrika kisiasa, kiuchumi na kijamii. Hali hii iliwapa Waafrika msukumo na hamasa ya kupigania haki na usawa katika nyanja za siasa, uchumi na utamaduni.

Wakati wa harakati za ukombozi wa Zanzibar, mfumo wa kimaadili ulikuwa umeathiriwa sana na mazingira ya kiuchumi, kijamii na kisiasa. Tabaka la Waafrika lilikuwa limebaguliwa na wakoloni kwa muda mrefu katika nyanja zote. Hivyo, Kamati ya vijana jasiri na shupavu iliundwa mapema hata kabla ya uhuru wa bandia wa tarehe 10 Desemba 1963. Lengo la kamati hiyo lilikuwa ni kuratibu kwa usiri wa hali ya juu suala zima la mapinduzi. Vijana hawa walifanya maandalizi yote na mnamo tarehe

FOR ONLINE READING ONLY

12 Januari 1964, Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar yalifanyika. Sultani Jamshid bin Abdullah Al Said aling'olewa madarakani pamoja na serikali yake chini ya Waziri Mkuu Mohamed Shamte wa ZPPP. Hatimaye tarehe 12 Januari 1964, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya ASP ikatangazwa. Kielelezo 6.2 kinaonesha baadhi ya viongozi walioshiriki katika Mapinduzi ya Zanzibar ya mwaka 1964.



**Kielelezo 6.2:** *Baadhi ya viongozi walioshiriki Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar mwaka 1964*

Kulikuwa na sababu kadhaa zilizosababisha Mapinduzi ya Zanzibar. Sababu hizi zilichochewa na madai ya muda mrefu dhidi ya utawala wa sultani, ambaye alionekana kuwa mwakilishi wa Waingereza. Baadhi ya sababu hizo ni kama zifuatazo:

**Sababu za kisiasa:** Kabla ya ujio wa Waarabu, Zanzibar ilikuwa imegawanyika katika maeneo mbalimbali ya kiutawala na kila eneo lilikuwa na kiongozi wake. Baadaye, watawala wa kienyeji kama vile Mwinyi Mkuu kwa upande wa Unguja na Makamandume kwa Pemba, waliunganisha mamlaka ndogondogo na kuunda himaya kubwa zaidi. Viongozi hawa walizisimamia sheria na taratibu za kijamii na waliheshimiwa sana. Walikuwa na jukumu la kuamua migogoro, kuongoza sherehe za kijamii na kusimamia maadili katika jamii walizoziongoza. Hata hivyo, hali ilibadilika baada ya kuja kwa utawala wa wageni, hasa kuanzia kipindi cha Usultani wa Waarabu. Watawala wa kienyeji waliondolewa na katika utawala huu, kuanzia wakati wa usultani hadi ukoloni wa Waingereza, masilahi ya wenyeji hayakuzingatiwa wala hayakupewa kipaumbele. Kwa mfano, wenyeji hawakushirikishwa kwenye vyombo vya kutoa uamuzi na kuwa viongozi serikalini.

Hata hivyo, kulikuwa na mabadiliko kidogo baada ya kuundwa kwa Baraza la Kutunga Sheria mwaka 1925. Wakati huu Waafrika wachache walipata nafasi, ingawa idadi kubwa ya wajumbe ilikuwa ni Waarabu na Wahindi. Wazanzibari hawakupata uhuru wa kujitawala na kufanya uamuzi wao wenyewe. Wajumbe hawa wachache hawakuweza kutetea masilahi ya Waafrika walio wengi Zanzibar. Hata uhuru uliopatikana baada ya uchaguzi wa mwaka 1963 ulikuwa ni mwendelezo wa mizizi ya ukoloni ya kutowatendea haki na heshima Wazanzibari.

Vilevile, chaguzi zote tatu zilitawaliwa na mizengwe iliyosababisha kukataliwa kwa matokeo. Chaguzi zilifuatiwa na fujo na ulaghai na ushindi wa ASP haukutambuliwa.

FOR ONLINE READING ONLY

Mathalani, uchaguzi wa Julai 1963 uliwapa ushindi muungano wa ZNP na ZPPP ambao walipata viti 18 dhidi ya viti 13 vya ASP. Mohamed Shamte wa ZPPP akawa Waziri Mkuu wa kwanza wa Zanzibar, jambo ambalo lilionekana kuwa ni la upendeleo na kuuendeleza ubaguzi. Wazanzibari walichoka kutawaliwa na wageni kwa muda mrefu na walihitaji kujitawala wenyewe. Hivyo basi, Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar yalikuwa ni hatua muhimu ya kujikomboa na kuupata uhuru ili kujenga maendeleo, kulinda utamaduni na maadili ya watu wa Zanzibar.

**Sababu za kijamii:** Kabla ya kuja kwa utawala wa Waarabu, utamaduni wa jadi wa jamii za Kizanzibari ulikuwa na tabia na sifa maalumu zinazotokana na mazingira, mila na desturi za jamii hizo. Wazanzibari walifundishwa kuheshimu watu wa rika zote, wakiwemo wazazi, wazee na viongozi wa mila. Aidha, watoto walilelewa kwa kushiriki katika kazi za kijamii kama kilimo na uvuvi. Pia, kulikuwa na mgawanyo wa majukumu katika familia na jamii. Kwa mfano, wanawake walijihusisha na shughuli za ususi wa vikapu na mikeka kwa kutumia majani mbalimbali kama ya ukindu, minazi na miti ya porini. Wanaume walijihusisha na uvuvi, uwindaji, kilimo, pamoja na ufundi wa kutengeneza zana za kilimo na uvuvi. Pia wanaume walijenga nyumba za jadi kwa kutumia udongo, makuti, mawe na miti hasa mikoko.

Vilevile, jamii iliishi kwa kuzingatia misingi ya umoja, haki na amani. Matukio kama vile harusi, tohara na mazishi yalitumika kuwaunganisha watu pamoja. Vyombo vya muziki kama ngoma, njuga, filimbi na marimba vilikuwa maarufu katika kuenzi maadili na utamaduni wa Wazanzibari. Muziki na ngoma za jadi zilitumika katika sherehe na matukio haya muhimu ya kijamii kama vile unyago kwa wasichana na jando kwa wavulana. Hivyo, maadili haya na utamaduni wa jadi vilijenga msingi wa jamii ya Wazanzibari kabla ya kuja kwa wageni ambao walileta athari za kiutamaduni, kisiasa, kiuchumi na kijamii.

Kuja kwa ukoloni kulileta ubaguzi katika jamii. Watu walianza kuheshimiwa kutokana na vyeo na asili yao (rangi). Maadili ya kuheshimu watu wa rika na tabaka zote hayakuzingatiwa. Vilevile, huduma za jamii kama vile maji, umeme na makazi zilitolewa kwa ubaguzi. Wazanzibari walibaguliwa katika nyanja za elimu, afya, makazi na umiliki wa rasilimali kama vile ardhi. Kwa mfano, mwaka 1955, asilimia 14 ya bajeti ya Serikali katika elimu ilielekezwa kwenye shule za Wahindi, wakati kipindi hicho Wahindi walikuwa 6% tu ya watu wote wa Zanzibar. Huduma muhimu za kijamii, kama vile maji safi, umeme na makazi, ziliimarishwa katika Mji Mkongwe ambako tabaka la Waarabu, Wahindi, pamoja na familia za wakoloni au Wazungu ziliishi. Huduma hizi hazikupatikana maeneo mengine kama Ng'ambo ambako Waafrika wengi waliishi.

FOR ONLINE READING ONLY

Hata hivyo, Waafrika ndio walioathirika zaidi katika mfumo wa kibaguzi wa kikoloni. Pamoja na wingi wao kufikia 85% ya watu wote wakati wa Mapinduzi, walipata huduma kidogo sana (chini ya 12%) ukilinganisha na wengine kama Waarabu na Wahindi. Wahindi na Waarabu ndio waliopata nafasi kubwa zaidi katika kupata huduma za kijamii, hasa maji, afya na elimu. Hivyo, ubaguzi katika nyanja mbalimbali ulileta chuki na kusababisha kuzuka kwa Mapinduzi ya Zanzibar mnamo Januari 1964.

**Sababu za kiuchumi:** Kabla ya ujio wa Waarabu, kilimo na uvuvi vilikuwa shughuli kuu za kiuchumi kwa Wazanzibari. Wazanzibari walilima mazao ya chakula kama vile mihogo, ndizi, nazi na mtama kwa ajili ya chakula na biashara. Pia, jamii hizi zilijihusisha na shughuli za ufugaji na utengenezaji wa zana za kazi. Vilevile, mazingira ya visiwa yaliruhusu uvuvi, ambao ulikuwa sehemu muhimu ya maisha ya Wazanzibari. Jamii hizi zilitumia mitumbwi ya kienyeji, madema na nyavu za mikono katika shughuli za uvuvi, hususani uvuvi wa samaki.

Hata hivyo, taratibu hizi zilibadilika mara baada ya kuja kwa wageni, yaani Waarabu na baadaye Wazungu wakati wa ukoloni. Wageni, hususani Waarabu walinyakua rasilimali kama vile ardhi nzuri kwa kilimo cha minazi na mikarafuu kwa manufaa yao binafsi na ya ukoloni. Wazanzibari wengi walinyang'anywa ardhi yao yenye rutuba na kubaki vibarua katika mashamba ya karafuu na minazi, pamoja na kufanya kazi za ndani. Wahindi walitawala biashara zote za jumla na rejareja madukani wakiwa pamoja na baadhi ya Waarabu. Hivyo, Mapinduzi ya mwaka 1964 yalikuwa ni ya lazima ili kupinga na kuondoa utawala dhalimu wa kikoloni, kulinda rasilimali za Wazanzibari na kujenga jamii inayozingatia misingi ya utu, usawa, haki na uwajibikaji kiuchumi.

Chama cha ASP kilifanya mikutano ya hadhara na kutumia vyombo vya habari kufichua maovu na unyanyasaji uliofanywa na wakoloni. Kwa mfano, mwezi Desemba 1959, katika viwanja vya Raha Leo, *Sheikh* Abeid Amani Karume alitangaza kwenye mkutano wa hadhara kwamba ASP ilitaka Zanzibar ipate uhuru na kuwa jamhuri. Serikali ya kikoloni haikukubaliana na kauli hiyo. Kwa kuwa milango yote ya kidemokrasia kwa Waafrika ilikuwa imefungwa, ASP iliona kuwa njia pekee ya kuleta uhuru wa kweli Zanzibar ni mapinduzi. Ndipo ilipofika tarehe 12 Januari 1964, ASP iliongoza Mapinduzi hayo na kuwakomboa Wazanzibari.

FOR ONLINE READING ONLY

**Zoezi la 6.3**

1. Eleza nafasi ya ASP katika kufanikisha Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar.
2. Eleza ni kwa namna gani huduma za kijamii kama vile elimu, afya na makazi zilitolewa kulingana na matabaka ya rangi Zanzibar.
3. Ni kwa namna gani ubaguzi wa rangi ulichochea Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar?

**Kazi ya kufanya 6.2**

Soma matini mbalimbali kupitia mtandao yanayohusu Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar, kisha andika maelezo kwa ufupi kuhusu:

(a) Namna Mapinduzi yalivyofanyika;

(b) Viongozi walioongoza Mapinduzi; na

(c) Ulichojifunza kutokana na Mapinduzi hayo.

## Mchango wa Mapinduzi wa Matukufu ya Zanzibar

Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar ya mwaka 1964 yalileta mabadiliko makubwa katika historia ya Zanzibar na yalikuwa na athari kubwa katika ukanda wa Afrika Mashariki na maeneo mengine. Mapinduzi hayo yalisababisha kuondolewa kwa utawala wa kisultani na kuanzishwa kwa serikali iliyoongozwa na wazalendo wa Chama cha *Afro-Shirazi* (ASP). Chama cha ASP kiliongoza kwa misingi ya utu, haki na ustawi wa watu wote bila kuzingatia tofauti za asili, hadhi au kabila. Mchango wa Mapinduzi hayo unajidhihirisha katika nyanja mbalimbali kama vile kujenga umoja, kuimarisha mshikamano na kuendeleza maadili katika jamii za Kizanzibari na Tanzania kwa ujumla.

### Kujenga umoja

Mapinduzi yalisaidia kuvunja migawanyiko na chuki zilizojengwa kutokana na hali ya ubaguzi katika jamii wakati wa ukoloni. Kwa kuwapindua watawala waliokuwa wakionekana kama wawakilishi wa wakoloni walioondoka, Mapinduzi yalileta umoja

FOR ONLINE READING ONLY

wa kitaifa. Mapinduzi ndiyo yalifungua njia ya utambulisho wa taifa linaloongozwa kwa misingi ya uhuru, haki na demokrasia. Ili kufanikisha azma hii, mnamo tarehe 21 Januari 1964, aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Watu wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, *Sheikh* Abeid Amani Karume, alitangaza wajumbe 29 wa Baraza la Kwanza la Mapinduzi Zanzibar. Baraza hili lilikuwa na jukumu la kuunda upya taifa lenye umoja, haki na kuondoa ubaguzi uliokuwa umeota mizizi kwa miaka mingi visiwani Zanzibar. Kielelezo 6.3 kinaonesha wajumbe wa Baraza la Kwanza la Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.




**Kielelezo 6.3:** *Baraza la Kwanza la Serikali ya Mapinduzi Zanzibar mwaka 1964*

FOR ONLINE READING ONLY

Vilevile, Mapinduzi ya Zanzibar yalichochea muungano kati ya Zanzibar na Tanganyika na hatimaye kuundwa kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwaka 1964. Muungano huu uliwaleta pamoja watu kutoka asili na kanda mbalimbali. Hivyo, kuimarisha hisia ya utambulisho wa kitaifa na umoja. Sababu za kihistoria na kiuhusiano zilizosababisha kuungana kwa nchi hizi baada ya Mapinduzi zilifanya muungano huu ufanikiwe na kuendelea kudumu hadi leo. Pia, nia ya viongozi wa pande zote mbili, yaani Mwalimu Julius Kambarage Nyerere wa Tanganyika na *Sheikh* Abeid Amani Karume wa Zanzibar, ya kudumisha umoja na mshikamano wa kitaifa, hivyo ilichangia sana katika kufanikisha muungano huu.

**Kujenga mshikamano**

Mapinduzi ya Zanzibar yalichangia kwa kiasi kikubwa kuleta mshikamano wa kitaifa miongoni mwa wananchi. Hii ilifanikishwa kupitia kuundwa kwa serikali inayowakilisha makundi yote ya kijamii na kuondoa mgawanyiko wa kikabila na kidini. Maadili ya mshikamano, upendo na umoja yalikuzwa na hivyo yameendelea kuwa nguzo muhimu katika ujenzi wa taifa.

Aidha, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ilipitisha kanuni za ujamaa na udugu ambazo zilisisitiza usawa, umiliki wa pamoja wa rasilimali na mshikamano. Huduma za jamii kama vile elimu, afya na makazi zilitolewa kwa usawa kwa wote bila kujali rangi, kabila, au dini ya mtu. Misingi hii iliendana na ile ya serikali ya Tanganyika na itikadi ya pamoja ilisaidia kuwaunganisha watu wa Zanzibar na Tanganyika chini ya dira ya pamoja ya kitaifa.

Vilevile, Mapinduzi ya Zanzibar yalichochea hisia ya fahari ya kitaifa, uzalendo na kujitolea kwa manufaa ya wote, ambayo yameendelea kujenga mfumo wa maadili wa taifa hadi sasa. Mshikamano huu ulikuwa muhimu katika kuhamasisha wananchi kuunga mkono serikali mpya na sera zake. Serikali ya ASP ilifanya kazi ya kukuza mshikamano wa kijamii kwa kuzuia sera zote za kibaguzi na kuweka misingi thabiti ya usawa, utu, heshima na kuboresha hali ya maisha ya watu katika nyanja zote.

**Kazi ya kufanya 6.3**

Soma matini mbalimbali yanayohusu mapinduzi ya kisiasa katika nchi mbalimbali duniani, kisha eleza ni kwa namna gani mapinduzi yanavyoweza kujenga umoja na mshikamano kwa taifa linalohusika.

FOR ONLINE READING ONLY

**Ujenzi wa maadili**

Mapinduzi ya Zanzibar yalileta ukomo wa matabaka yaliyokuwapo kati ya Waarabu, Wahindi na Waafrika. Kwa kuondoa mfumo wa ubaguzi na ukandamizaji, Mapinduzi haya yaliweka misingi wa usawa wa kijamii, ambapo watu wote walihesabiwa kuwa na thamani sawa bila kujali asili yao. Hii ilijenga mazingira ya usawa, upendo, amani, heshima na mshikamano miongoni mwa watu wote. Serikali mpya ilisisitiza umuhimu wa demokrasia, haki za binadamu, utu, usawa na ustawi wa watu. Hii ilichangia katika kuhifadhi maadili ya jamii kama vile ushirikiano, usawa, kuheshimiana na kusaidiana ambayo ni sehemu muhimu ya utamaduni na utambulisho wa Mzanzibari.

Sambamba na hayo, Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar yalichangia kukuza na kuendeleza lugha ya Kiswahili. Baada ya Mapinduzi, serikali mpya ilitilia mkazo umuhimu wa Kiswahili kama nyenzo muhimu ya kujenga umoja na utambulisho wa kitaifa. Kiswahili kikawa lugha rasmi ya serikali na wananchi wote wa Zanzibar. Ili kuhakikisha lugha hii inakua na kustawi, vilianzishwa vyombo mbalimbali vya habari kama vile magazeti ya Kiswahili, redio na baadaye vipindi vya televisheni. Pia, taasisi na wasomi walihimizwa kusoma na kuandika makala mbalimbali kwa kutumia lugha hii. Jambo hilo lilisababisha kuandikwa kwa kamusi na vitabu vya sarufi. Vitabu hivi vilikuwa nyenzo za elimu kwa lengo la kukuza Kiswahili katika maeneo mengine ya Afrika Mashariki na bara zima la Afrika.

Serikali ilihamasisha matamasha mbalimbali ya kitamaduni ili kuimarisha umoja na mshikamano wa Wazanzibari. Kwa mfano, kuna matamasha kama Sauti za Busara, Sherehe za Mwaka Kogwa, Tamasha la Nchi za Jahazi Zanzibar (ZIFF), Tamasha la Vyakula vya Asili Makunduchi na mashindano ya mpira wa miguu ya Kombe la Mapinduzi. Haya matamasha yamesaidia na yanaendelea kusaidia, katika kuelimisha kizazi kipya kuhusu maadili, urithi wa kitamaduni na umuhimu wa kuuhifadhi.

**Zoezi la 6.4**

1. Bainisha jitihada zingine zilizochukuliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kuujenga umoja, usawa na mshikamano kwa jamii za Wazanzibari.
2. Eleza ni kwa namna gani lugha ya Kiswahili imefanikiwa kuwaunganisha Wazanzibari baada ya Mapinduzi.
3. Fafanua namna Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar yanavyoenziwa katika jamii ya sasa ya Watanzania.

FOR ONLINE READING ONLY

### Kazi ya kufanya 6.4

Kwa kutumia vifaa vya TEHAMA, sikiliza hotuba kuhusu Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar mwaka 1964, kisha jibu maswali yafuatayo:

1. Umejifunza nini kutokana na hotuba uliyosikiliza?
2. Je, viongozi wa sasa wanaweza kujifunza nini kutoka kwa Mapinduzi ya mwaka 1964 katika kuzilinda na kuzitetea haki za raia?

## Zoezi la marudio

1. Kwa kutumia mifano, jadili sababu za kufanyika kwa Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar.
2. Ni kwa nini uhuru wa Desemba 10 mwaka 1963 wa Zanzibar uliitwa uhuru wa bandia?
3. Jadili athari za Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar katika muundo wa kijamii na kisiasa wa Zanzibar.
4. Fafanua maadili yaliyojengwa kutokana na Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar.
5. Ni kwa namna gani Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar yamechochea Muungano wa Tanganyika na Zanzibar?
6. Eleza mchango wa vyama vya michezo katika Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar.
7. Pendekeza njia mbalimbali zinazoweza kutumiwa katika kulinda Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar.

FOR ONLINE READING ONLY

# Faharasa

| | |
|---|---|
| **Afrikanaizesheni** | Utaratibu wa kuwaingiza na kuwapa Waafrika wenye sifa madaraka ya kiuchumi, kijamii na kisiasa baada ya nchi za Kiafrika kupata uhuru kutoka kwa wakoloni |
| **Bepari** | Mtu ambaye ni mfanyabiashara na tajiri mkubwa anayemiliki njia kuu za uzalishajimali kama vile viwanda na masoko |
| **Falsafa** | Stadi ya maarifa, imani, maisha, chanzo chake na sababu za kuwapo kwake |
| **Itikadi** | Imani au msimamo wa mtu au watu kuhusu jambo fulani mfano dini, chama, mawazo |
| **Kasumba** | Fikra za mtu zinazojengeka kutokana na kuathiriwa kielimu, kiutamaduni au kiutawala na jamii fulani iliyomzunguka |
| **Kibaraka** | Mtu mwenye uwezo wa chini kifedha na anayetumiwa na watu wengine kwa masilahi ya watu hao pasi na kujali madhara wanayopata watu wengine |
| **Propaganda** | Taarifa zisizo na ukweli ambazo hutumika katika uhamasishaji wa watu ili wafuate mtazamo tofauti na ule waliokuwa nao |
| **Manamba** | Mfanyakazi aliyetoka mbali kwa ajili ya kufanya kazi katika mashamba makubwa yaliyokuwa yanamilikiwa na watu wengine hasa walowezi |
| **Telegramu** | Taarifa ya maandishi inayotumwa kwa njia ya simu |
| **Walowezi** | Watu wanaotoka nchi moja na kuhamia nchi au eneo lingine kwa nia ya kudhibiti, kuendeleza, au kutumia rasilimali za eneo hilo. |
| **Wazawa** | Watu ambao wamezaliwa na kukulia katika eneo au nchi fulani na ni wenyeji wa eneo hilo. Kwa mfano, "wazawa wa Tanzania" |

FOR ONLINE READING ONLY

# Bibliografia


Abdallah H. B. (2012). *Dola Kongwe ya Zanzibar Kutoka Oman Hadi Kongo*. Kauthar Printers.

Afro-Shirazi Party. (1977). *A Short History of Zanzibar*. Printing Press Corporation.

Ayany, S.G. (1970). *A History of Zanzibar in A History in Constitutional Development 1934-1964.* East African Literature Bureau.

Boahen, A. A. (1987). *African perspectives on colonialism.* Johns Hopkins University Press.

Davidson, B. (1967). *The growth of African Civilization: East and Central Africa to the late nineteenth century*. Longmans.

Giblin, J. (1986). Maji Maji: Lifting the fog of war. *The International Journal of African Historical Studies*, 19(1), 99-138.

Hyden, G. (1980). *Beyond Ujamaa in Tanzania: Underdevelopment and an uncaptured peasantry*. University of California Press.

Idara Mbalimbali za ASP. (1974). *Afro- Shirazi Chama Cha Ukombozi*. Shirika la Upigaji Chapa Zanzibar.

Illife, J. (1967). *A Mordern History of Tanganyika.* Cambridge University Press.

Iliffe, J. (1979). *Tanganyika under German rule, 1905–1912*. Cambridge University Press.

Illife, J. (1998). *East African doctors: A history of the modern profession*. Cambridge University Press.

Institute of Curicullum Development. (1980). *East Africa from 1850 to the present: Secondary History Book Two*. University Press.


FOR ONLINE READING ONLY

Ishumi, A. G. M. (1976). *Education and Development in Africa: The case of Tanzania*. East African Publishing House.

JMT. (2022). *Muungano wa Tanganyika na Zanzibar: Chimbuko, Misingi na Maendeleo*. Ofisi ya Makamu wa Rais. Mkuki na Nyota.

Juma, A.S. (2007). *Zanzibar Hadi Mwaka 2000.* Rafiki Publishers.

Kaniki, M.H. Y. (1980). *Tanzania under colonial rule.* Longman Group Limited.

Kimambo, I. N., & Temu, A. J. (1971). *Historia ya Tanzania, Sehemu ya Kwanza*. East African Publishing House.

Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji Mji Mkongwe. (2019). Tuutunze Mji Mkongwe. Medu Press.

Mapunda, H. (1980). *Historia ya mapambano ya Mtanzania.* Tanzania Publishing House.

Mapunda, H. (1976). *Historia ya Mapambano ya Mwafrika*. Tanzania Publishing House.

Mapuri, O.R. (1996). *The 1964 Revolution: Achievements and Prospects*. TEMA Publishers.

Mushi, A.K.P. (2011). *History and Development of Education in Tanzania.* East African Publishing House.

Nyerere, J. K. (1967). *Elimu na ujamaa*. Oxford University Press.

Nyerere, J. K. (1967). *Freedom and development: Uhuru na maendeleo*. Oxford University Press.

Okello, D. O., & Yahya, R. (1996). *Health sector reforms in sub-Saharan Africa: Lessons of the last 10 years*. World Health Organization.

Okoth, A. (2006). *A History of Africa 1915-1995,* Vol 2. East African Publishers.

FOR ONLINE READING ONLY

Shivji, I. G. (1976). *Class struggles in Tanzania*. Heinemann Educational Books.

Taasisi ya Elimu (1994). *Historia shule za msingi: Jamii za Watanzania hadi mwaka 1880*. Taasisi ya Elimu.

Taasisi ya Ukuzaji Mitaala. (1989). *Historia shule za msingi: Jamii za Waafrika tangu 1880*. TPH.

Wizara ya Elimu ya Taifa. (1976). *Historia ya Tanzania baada ya Mwaka 1880: Kitabu cha Tatu Darasa la Sita.* Wizara ya Elimu ya Taifa.

FOR ONLINE READING ONLY

Shadrack